Kikao cha Pili – Tarehe 12 Machi, 2015

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika: (Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Naomba Kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria kufuta Sheria ya Baraza la Sanaa na Muziki namba 6 ya mwaka 1983 na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa na maonesho namba 1 ya mwaka 2009 na kutunga Sheria mpaya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka hati mezani ya maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 5

Sababu za Mabadiliko ya Majina ya Vyeo vya Maafisa Tawala wa Wilaya na Mikoa

Mhe. Abdalla Juma Abdalla (kny) Mhe. Saleh Nassor Juma: - Aliuliza**:**

Kuna taarifa kwamba Serikali katika marekebisho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ina mpango wa kubadilisha majina kwa vyeo vya Afisa Tawala Wilaya *(District Administrative Officer (DAO))* na Afisa Tawala Mkoa *(Regional Administrative Officer (RAO))* badala yake waitwe Katibu Tawala Wilaya, katika ngazi ya Wilaya (*DAS*) na Katibu Tawala Mkoa kwa ngazi ya Mkoa (*RAS*).

Je, kuna sababu gani za kitaalamu zinazopelekea Serikali kubadilisha majina ya vyeo hivyo viwili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya mwaka 2014 ambayo imepitishwa na Baraza lako Tukufu inawatambua Wasaidizi wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwa ni Makatibu Tawala badala ya Ofisa Tawala kama ilivyokuwa katika Sheria Namba 1 ya mwaka 1998.

Mhe. Spika, sababu ambayo imepelekea mabadiliko hayo ni kuwatofautisha watendaji hawa ambao ni Wasaidizi wa Wakuu wa Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Maofisa wengine wa kisekta ambao wamo katika Mikoa na Wilaya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja dogo sana kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wazanzibari hili neno la Sekretari hatujalizoea na tumezoea Afisa Tawala baada ya Katibu Tawala. Je, haoni kwamba kuendelea kuiga kwa sababu haya maneno huwa yanatumika Bara zaidi RAS na DAS wakati na sisi ni waswahili zaidi kuliko hawa wenzetu walioanzisha mamnbo ya RAS na DAS, haoni kama itaonekana kwamba ni kuburuzwa katika mambo ya Lahaja, wakati sisi mambo ya Lahaja za kiswahili zimebobea zaidi huku kuliko Tanganyika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwanza sababu ya msingi ni sharti la Kisheria ambalo Baraza hili tayari tulipitisha.

Lakini la pili nilipokuwa najibu swali mama nilisema kwamba Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya tunawapa jina hili kwa sababu ya kuwatofautisha na maofisa wengine wanaofanyakazi katika Mikoa na Wilaya; kuna Maofisa Kilimo, Maafisa wa Maji, Maafisa wa Ardhi. Hawa Makatibu Tawala ndio viongozi wa wale Maafisa wengine katika Mikoa na Wilaya na hili sidhani kama tunaiga kwa sababu sasa hivi katika mfumo wetu wa kiutawala katika Wizara tuna Katibu Mkuu, tuna Naibu Katibu Mkuu tuna Wakurugenzi, tuna Makamishna, tuna na Maafisa. Kwa hiyo, si suala la kwamba tunaiga, ni mfumo wetu wa kiutawala unatambua hivyo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri amejitahidi kutoa jibu kwa ufasaha kabisa kasema kuwa tunawaita Makatibu Tawala na kadhalika ili kuwatafautisha na Maafisa wengine.

Naomba kujua kwa sababu ninavyojua kuna kitu Tawala ukimwita Katibu Tawala tayari kashatafautika na Maafisa wengine na ukimwita Afisa Tawala kwa vile kuna neno Tawala vile vile keshatafautika na Maafisa wengine wa kilimo na kadhalika. Kuna umuhimu gani hasa ulisababisha mpaka Afisa ikaondoka na ikawekwa Katibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, Tawala ni Sekta, Kilimo ni Sekta tulichotafautisha hapa sio Sekta. Tulichotafautisha hapa ni dhamana, kwa hiyo Katibu maana yake ni kiongozi wa wale Maofisa. Kwa hiyo, yeye ni Katibu Tawala maana yake anawaongoza wote wale Maafisa ambao wako ndani ya Mkoa wake na ndani ya Wilaya yake.

Kwa hiyo hapa tulichotafautisha ni kuondoa neno Afisa na kuweka neno Katibu na wale kubakia Maafisa kwa sababu wao ukisema huwezi kumwita yule Katibu Kilimo kwa sababu tayari kuna Katibu Mkuu Kilimo. Kwa hiyo tulichotafautisha hapa ni ile sekta huyu ni Katibu Tawala sio Afisa. Ahsante.

Nam. 16

Vyanzo vya Mapato katika Huduma ya Afya

Mhe. Ali Salum Haji: - Aliuliza**:**

Kutokana na ufinyu wa bajeti katika kuendesha huduma mbali mbali katika hospitali zetu.

Je, Wizara ina mpango gani kuanzisha vyanzo vya kuingiza mapato mfano; Bima ya Afya au utumiaji wa '*electronic'* katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Spika, ahsante sana kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa na afya njema na kujumuika sote pamoja katika kutekeleza kazi tuliotumwa na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli ufinyu wa bajeti unapelekea huduma za afya katika hospitali kutolewa katika kiwango kisichoridhisha kutokana na uhaba wa vifaa mbali mbali ikiwemo dawa na vitendea kazi.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na hali hiyo, tayari Wizara ya Afya imeshaanza mchakato wa mpango wa kuanzisha Bima ya Afya. Hatua zilizofikia kwa hivi sasa Mhe. Spika, ni Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), Shirika la Bima Zanzibar

na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Tayari imekamilisha ripoti ya awali ya kuangalia uwezekano wa uanzishwaji wa mfuko maalum wa Bima ya Afya kwa hapa Zanzibar.

Hatua inayofuata ni kufanya Utafiti ambao unajulikana kama *Actuarial Study* ambao utasaidia kufanya maamuzi sahihi ya namna ya uendeshaji mzima wa Mfuko wa Bima ya Afya utakaofanya kazi kwa hapa Zanzibar. Aidha, kumalizika kwa utafiti huo kutapelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ambayo baada tu ya kupitishwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar Sheria itawasilishwa hapa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya Waheshimiwa Wawakilishi kuipitisha Sheria hiyo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakubalina na kauli ya Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa ujumla Wizara ya Afya ina mapungufu ya kifedha. Lakini naomba kumuuliza kwamba hivi karibuni nilikuwa katika Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani na nilishuhudia mwenyewe kwamba mgonjwa mmoja aliyehitaji damu ya *Group O* chupa moja ilishindikana Pemba nzima, mimi mwenyewe nikadiriki kumpigia Katibu Mkuu Unguja nisimpate, nikampigia Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja nisimpate.

(a) Hivyo naomba kujua chupa moja ya damu iliyokosekana Pemba pia ni ukosefu wa fedha au ni uzembe wa Wizara ya Afya.

(b) Hivyo sababu hii ya ukosefu wa fedha ambayo imekuwa ikizungumzwa na wizara yake ndiyo sababu tosha ambayo inasababisha mapungufu haya au ni sababu ya kutokuwa makini katika vipaombele vya wizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba nimthibitishie Mhe. Hija Hassan Hija kwamba damu yote inatolewa bure haiuzwi.

Mapungufu ambayo huwa yanatokea baadhi ya wakati katika damu ni ile *Blood Group O* ambayo inakuwa na mapongufu kwa sababu hawa *Blood Group O* huwa wanaitwa *Universal Donor* na sio wengi sana, katika *Population* ni asilimia ndogo sana.

Kwa hiyo, kama kutakuwa na mapungufu yanatokezea ni *Blood Group O* lakini kwa kuwa hilo ni kundi maalum tayari kuna orodha ya wote wanaochangia damu hiyo ya *Blood Group O* ambao wanajulikana na Wizara pamoja na Vituo mbali mbali vilivyokuwepo vya damu hata Pemba kwa sababu kuna vituo maalum ambavyo vimepewa vifaa kupitia msaada wa *Centre for Disease Control* kwa ajili ya kuhifadhia damu hiyo, basi huwa mara nyingi tunahakikisha kwamba *Blood Group O* inakuwepo katika *Storage* hasa pale wagonjwa wanapohitaji kundi hilo maalum la *Blood Group* hiyo.

Kwa taarifa yake Mhe. Hija Hassan Hija mara nyingi inapotokezea tatizo kama hilo halihusiani na fedha wala ufinyu wa bajeti katika wizara. Kwa sababu tayari idara hiyo ya damu au Benki hizo za damu tayari zina bajeti yake mbali na zina wafadhili wake ambao wanatusaidia kuendesha tukishirikiana na Serikali ya watu wa Marekani. Kwa hiyo, hilo halihusiani kabisa na bajeti linapotokezea ni pale *Blood Group* fulani imekosekana, basi huwa mgonjwa ama wale watu wake wa kumuhudumia mgonjwa ama wale watendaji wa ile Idara yenyewe huwa wanahangaika kutafuta damu ile.

Mpaka jana wakati tunafanya mapitio ya kazi mbali mbali za wizara tumepata taarifa ya Benki ya Damu kwamba sasa hivi *Blood Group* zote zinapatikana katika Benki zetu za damu na damu zote ni salama kwa sababu zimeshapitia uchunguzi wote wa kufanyiwa kwa kina. Kwa hiyo, naomba nimthibitishie kwamba hiyo damu ipo na hakuna tatizo lolote linalotokana na ufinyu wa bajeti katika eneo hilo, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Hospitali ya Mkoani kuna tatizo la uwekaji wa damu kutokana na kuwa umeme kuwa mdogo, mgonjwa anapofika anatakiwa damu inabidi mpaka damu ikachukuliwe katika Hospitali ya Wete. Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni hili ni tatizo kwa wananchi wetu wanapotokezewa na madhara ya kupatikana kwa damu. Lakini je, suala hili na wewe unalichukuliaje.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli Mhe. Spika, kuna tatizo upande wa Pemba kutokana na umeme kuwa mdogo, zile *freezers* maalum za kuhifadhia damu huwa umeme ukipungua zinajizima ndivyo zilivyoundwa. Tatizo hilo kweli na huwa mara nyingi tunapata taabu. Ndiyo maana hivi sasa tunajaribu kuratibu mfumo wa umeme mbadala kwa baadhi ya vitengo maalum ambavyo vinahitaji umeme uliokuwa upo sawa, yaani haupungui kuweza kuhifadhia.

Pili, jitihada tuliyofanya kuna mawasiliano kadhaa ambayo tumeshafanya na wenzetu wa Shirika la Umeme (*ZECO*), shirika linatoa umeme kwa hapa Zanzibar na mimi mawasiliano hayo nimebahatika kuyaona ya barua, baina ya Katiba Mkuu na Meneja Mkuu, ninafikiri anaitwa yule wa *ZECO* kwa ajili ya kujaribu kupata umeme ambao sawa.

Jitihada ya tatu iliyochukuliwa mpaka sasa hivi ni kununua *stabilizer* kwa hizi *freezers* maalum za damu ambapo umeme unapopungua basi ile *stabilizer* inasaidia ku-*stabilize* ili yale mafriji yaweze kuendelea na kazi kwa ajili ya kuhifadhia damu.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na kukubali kuwa Wizara yake inao ufinyu wa bajeti, jambo ambalo linasababisha kutokutekelezeka shughuli zake kama alivyokaridia.

Mhe. Spika, kwa sababu moja kati ya matatizo makubwa kweli kweli yaliyoikabili Wizara hii ni kupeleka wagonjwa nje ya nchi, jambo ambalo linagharimu pesa nyingi sana. Kwa taarifa niliyonayo Mhe. Spika, ni kuwa Wizara hii inadaiwa pesa nyingi sana kwa wagonjwa waliopelekwa nje ya nchi kwa matibabu ambalo ni jambo la lazima, hili kusababisha Wizara pia kuwa na madeni makubwa zaidi ya ufinyu wa bajeti. Mhe. Spika, kwa kuhofia hali mbaya ikaja ikajitokeza huko usoni kwa madeni, haoni Mhe. Naibu Waziri ipo haja hasa ya Wizara hii kufanya mpango mkakati ambao utauwezesha kufanya shughuli zake kiilivyo kwa kutumia pesa kuliko huu mpango ulioelezwa katika karatasi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante sana, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli Mhe. Spika, tumekuwa tukipeleka wananchi kwa kuanzia Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa hapa Tanzania kwanza na inaposhindikana au tunapopata *referral* ya hapo basi huwa tunawapeleka nje ya nchi. Ni kweli kuwa tuna mikataba mitatu ambayo tumefunga na wenzetu nchini India kupitia hospitali tatu. Hospitali ya kwanza ni Miote, hospitali ya pili ni Manipal kwa hivi sasa pamoja na *branches* zake. Sasa ni kweli pia kwamba tuna deni ingawa Mhe. Mjumbe amesema fedha nyingi sana. Sasa naomba hizo fedha niziweke sawa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ambayo tunaishukuru sana kuwa kila baada ya muda tunalipa na ile mikataba yetu inaturuhusu tunadaiwa kwa kutumia zile huduma.

Kwa hivyo mpaka hivi sasa mpaka jana tunadaiwa kama US dola 815,000 mpaka jana. Lakini katika mwezi huu tayari tulifanikiwa kulipa kama Dola 200,000 na mwezi uliopita na tunaendelea hivyo hivyo. Lakini naomba pia nimthibitishie Mhe. Mjumbe kwamba mpaka hii leo tumefanikiwa kupunguza idadi ya asilimia kama thalathini ya wagonjwa wetu waliokuwa wanahitaji matibabu ya kwenda nje hapo awali, sasa hivi wanapata matibabu yao hapa. *(Makofi)*

Matibabu hayo yametokana na kufunguliwa na vitengo vipya kama kile Kitengo cha Nuria *surgery* kwenye jengo jipya lililokuwepo pale, hapo awali wagonjwa wote wenye matatizo ya mgongo ama wanaohitaji operesheni za mgongo au mishipa ya fahamu ilikuwa tunawapeleka nje. Sasa wagonjwa wote hao wanashughulikiwa hapa hapa, kwa hivyo tumepunguza punguzo kubwa sana la wagonjwa wetu kupeleka nje ya nchi.

Upande wa pili ni wale watoto wenye vichwa vikubwa, wanaitwa vichwa maji wanaojaa maji kwenye vichwa. Hapo awali watoto wale wote tulikuwa tukiwapeleka nje ya nchi. Sasa ninashukuru kusema kwamba matatizo hayo yote, sasa hayana haja ya kwenda nje ya nchi, yote yanashughulikiwa hapa hapa Zanzibar.

Matatizo ya tumbo ndani, kutazamwa kwa kamera na kufanyiwa operesheni kwa kamera, matatizo yote ya tumbo sasa hivi yanafanyika hapa hapa, tumepata mtaalamu wa Kichina ambaye pia anafundisha wataalamu wetu wa hapa na kwa hivyo na huko tumepunguza. Kwa hivyo tumepunguza kama asilimia thalathini tayari, lakini kwa kuja ni *step* ya hatua kwa hatua tunayokwenda. Kwa kuja jengo jipya hilo la Nuria, Mwenyezi Mungu akitujaalia litakapokamilika wagonjwa wote wenye matatizo ya figo na wanaohitaji *dialysis* pia nao tutawapunguza watakwenda hapo kupata huduma, maradhi yote hayo ya watoto wadogo, mambo ya moyo na mengineyo pia tutapunguza.

Kwa hivyo, mwisho wa siku tutabakia labda na asilimia kama kumi hadi ishirini yote hayo yatakapokamilika ambao watahitaji kupelekwa kwa huduma za ziada kwenda nje ya nchi ama kwenda nchini India.

Kwa hivyo, hili suala ni la hatua kwa hatua na hizi hatua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein inaendelea kupiga hatua katika sekta ya afya pamoja na ufinyu wake wa afya, lakini hizi huduma tunaendelea kuongeza ili tuweze kupunguza fedha nyingi zinazotumika nje ya nchi.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Na. 12

Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya (UUVWW) PEMBA

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:

Kwa kipindi kirefu sasa, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto Pemba inamiliki kiwanja katika eneo la Tibirizi ambacho kinakusudiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Wizara hiyo. Hata hivyo, ujenzi bado haujafanyika na Wizara imekuwa ikitumia gharama ya Tshs.18,000,000/- (Milioni Kumi na Nane) kwa mwaka kwa ajili ya kulipia gharama za kodi katika jengo ambalo wanalitumia sasa.

a) Je, kuna sababu gani zinakwamisha kuanza kwa ujenzi wa ofisi hizo.
b) Wizara ina mikakati gani itakayofanikisha kuanza kwa ujenzi huo.
c) Ni lini Wizara itakamilishiwa ujenzi wa jengo la Ofisi ili Wizara iweze kukwepa gharama za kodi na hatimae fedha zitumike kwa shughuli nyengine.

Mhe. Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto) - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla sijamjibu naomba kuanza nitangulize maelezo yafuatayo. Kwanza ni kweli Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana na Wanawake na Watoto inamiliki kiwanja katika eneo la Tibirinzi ambacho kilikusudiwa kujenga Afisi ya Wizara Pemba, lakini kutokana na sababu za kimazingira Wizara ililazimika kutafuta kiwanja chengine katika eneo la Gombani kwa ajili ya kujenga afisi hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

(a) 1) Sababu zilizokwamisha kuanza ujenzi wa ofisi kwa wakati ni pamoja na kubadilika kwa eneo la kujenga ofisi ambapo taratibu za kutafuta mtaalamu mwelekezi ilibidi zifanywe upya.

2) Uamuzi wa Serikali wa kujenga jengo kubwa zaidi ya ofisi litakalochukua Wizara tatu ambapo ilibidi mtaalamu mwelekezi kuchanganua na kuhakikisha anaingiza mahitaji ya kila Wizara katika michoro ya jengo hilo.

3) Uhaba wa fedha ambao ulisababisha kuchelewa kulipwa kwa mtaalamu mwelekezi ambaye naye ilibidi achelewe kuanza kazi kutayarisha michoro na nyaraka za zabuni.

b) Mhe. Spika, ujenzi wa jengo la ofisi hii unasimamiwa na Wizara ya Fedha ambayo ina mikakati ya kuweka bajeti ya ujenzi katika jengo hilo hatua kwa hatua. Mtaalamu mwelekezi ameshapatikana na kuanza kazi na taratibu za kutangaza tenda za ujenzi zinaandaliwa.

c) Mhe. Spika, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ofisi hiyo kunategemea mkataba wa ujenzi kati ya Serikali, mkandarasi pamoja na hali ya upatikanaji wa fedha.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Ulipaji wa kodi wa milioni 18 kwa mwaka ni sawa na milioni moja na laki tano. Je, katika kufikia mapato ya kodi ya jengo hilo wataalamu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati walishirikishwa.

Mhe. Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto) Mhe. Spika, suala hili kama nilivyosema linaratibiwa na Wizara ya Fedha, kwa hivyo ninadhani Wizara ya Fedha watakuwa katika nafasi nzuri ya kusaidia kujibu suala hilo na Mhe. Waziri wa Fedha madhali yupo naomba kwa ruhusa yako atusaidie kidogo kujibu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, miradi yoyote ile ya ujenzi ambayo tunayoifanya ndani huwa tunawashirikisha wataalamu wetu wa ndani. Hata hili vile vile ujenzi wa hili jengo tumeanza kuwashirikisha na tutawashirikisha kikamilifu jengo litakapoanza kujengwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Kaimu Waziri wa Wanawake na Watoto, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Kaimu Waziri amekiri kwamba kilikuwepo kiwanja pale Tibirinzi na kwa sababu na mimi nilikuwemo katika hiyo Kamati ya Wanawake na Watoto ya Baraza la Wawakilishi na nilikwenda kukiona ni kiwanja kizuri na chenye kiwango sana ambacho kimekaribiana na Hoteli ile kubwa pale Tibirinzi anapofikia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pale ZSSF.

a) Na kwa kuwa kile kiwanja ni kizuri na wamekiacha na wakenda Gombani karibu kilomita mbili kutoka ni *country side* ya mji wa Chake-Chake. Je, kiwanja hiki mumekitelekeza tu kukiacha kwa sababu kina gharama kubwa pale au mumekiuza ndiyo mukanunua hicho.

b) Kwa kuwa shilingi milioni 18 kwa mwaka ni fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii kukodi na kila mwaka unatoa shilingi milioni 18 kukodi kwa Afisi ya Wanawake na Watoto na kwa kuwa kuna ile hoteli ya Hifadhi pale ambayo anafikia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pale, ina sehemu kubwa na ina nafasi kubwa na haina wageni ile hoteli siku hizi, ile hoteli haipati wageni zaidi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akija pale akapata kupumzika kidogo, haina wageni.

Sasa hamuoni kwamba ingekuwa vyema tuitumie ile hoteli kuweka hiyo Afisi ya Wanawake na Watoto badala ya kutoa shilingi milioni 18 kwa mwaka mpaka hapo mutakapojenga, kuendelea kutumia shilingi 18 wakati hoteli imekaa tu ile. Si matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma (Kny: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto): Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

1) Kwanza nilijibu kwenye swali langu au jibu langu mama kwamba tatizo linalosababisha la kutokujenga eneo lile la Tibirinzi ni kutokana na hali ya kimazingira ya pale, ardhi ya pale hairuhusi ujenzi wa eneo hiyo ambao tunaotaka kujenga. Sote ni mashahidi eneo la Tibirinzi ile hali ya ardhi na udongo wa pale

ulivyo unachokijenga chochote siku ya pili tu pale kimeanza kuleta athari. Kwa hivyo wakati mwengine ni shida inaanza shida, lakini shida huanza faraja.

Mhe. Spika, tumeamua twende Gombani kwa sababu kuna neema kubwa, naona aliyeniuliza swali hanisikilizi sasa inakuwa shida halafu kuja kumfahamisha tena lakini ninaendelea. Mazingira ya Gombani ni mazuri zaidi kwa ujenzi.

2) Mhe. Spika, ni kweli tunatumia pesa lakini tunatumia kwa sababu haja sasa hivi kwa sababu hatuna jengo jengine na wala siyo pesa nyingi kiasi hicho ukilinganisha na kodi zinalipwa katika maeneo mengine. Tuna ushahidi sisi pana majumba ambayo wanakaa viongozi wetu tunalipa pesa mamilioni kwa mamilioni kwa mwaka. Sasa hilo siyo tatizo kwamba tunalipa pesa hizo kwa sababu hatuna, tungekuwa na jengo letu tusingeweza kufanya hivyo, na ndiyo maana yake Serikali ikafika wakati tukaamua jengo moja tulijenge ofisi tatu ndani yake; Wizara ya Fedha, Wizara ya Kazi na Wizara ya Uwezeshaji tutakuwemo kwenye jengo hilo hilo moja. Mwenyezi Mungu atujaalie inshaallah na michoro tayari kila kitu tayari na mtaalamu ameshafanya kazi yake, kilichobakia sasa hivi siku si nyingi tutaanza kazi.

Mhe. Spika, ahsante.

Na. 46

Zanzibar Kuandaa Mashindano ya *CECAFA*

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:

Kwa kuwa Zanzibar imeshawahi kuandaa mashindano mbali mbali ya *CECAFA* katika miaka ya nyuma lakini kwa muda mrefu sasa Zanzibar haijaweza kuwa mwenyeji wa mashindano yoyote yanayosimamiwa na *CECAFA* na kukosa kuwapa fursa tena wapenzi wa mchezo huo wa mpira wa miguu kuyaona tena mashindano hayo.

a) Je, Serikali ina mpango gani kwa kushirikiana na *BTMZ* na *ZFA* kuwa mwenyeji wa mashindano hayo yanayosimamiwa na *CECAFA*.

b) Kukosekana kwa Zanzibar kuwa mweyeji wa mashindano hayo hapa Zanzibar si kunaanzisha kuuwa vipaji vya wachezaji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 46 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, mashindano ya Shirikisho la Soka la Afrika Mashariki na Kati (*CECAFA*) mara zote huandaliwa na wanachama wa shirikisho hilo na wala hayaandaliwi na Serikali au Mabaraza ya Michezo. Mhe. Spika, hapa Zanzibar mwanachama wa shirikisho hilo ni *ZFA*. Hivyo, ZFA itakapokuwa tayari itaandaa mashindano hayo bila ya kusubiri mipango ya Serikali au Baraza la Michezo.

b) Mhe. Spika, siyo kweli kwamba kukosa kuwa mwenyekiti wa mashindano hayo kunauwa vipaji vya wanamichezo wetu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, mbali na majibu ya Mhe. Naibu Waziri nimesikitika sana na majibu yake hasa pale aliposema kwamba *ZFA* itakapokuwa tayari itaandaa mashindano hayo bila ya kusubiri mipango ya Serikali au Baraza.

Mhe. Spika, tukikumbuka mwaka 2003 wakati ule Wizara hii ya michezo ilikuwa katika Wizara ya Elimu chini ya Mhe. Haroun Ali Suleiman iliandaa mipango mizuri na mikakati mizuri ya kuweza kuandaa mashindano ya *CECAFA* ya *under twenty* ambapo Zanzibar tukawa mabingwa wa mashindano hayo.

Je, kuendelea kuwaachia *ZFA* ambao hawana uwezo wa kuendesha mashindano kama haya, siyo kuwakosesha Wazanzibari kuyaona mashindano hayo.

b) Mhe. Spika, kukosa Zanzibar kuendesha mashindano haya kuwa wenyeji wa mashindano haya, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba siyo kukosa kuendeleza vipaji vya Wazanzibari, lakini vipaji vyovyote vya wanamichezo vinakua pale ambapo hushiriki katika mashindano mbali mbali.

Je, kuendelea kutowakuwaunga mkono hasa mashindano kama haya. Si kukuza vipaji vyetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninakushukuru na kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Nassor Salim Ali maswali yake mawili kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake jukumu la kuandaa mashindano kwa vyama vya michezo vyote vilivyopo Zanzibar ni suala la vyama vyenyewe. Vipo vyama mbali mbali hapa vinaandaa mashindano ya kimataifa, mfano Chama cha Judo mara kwa mara ama kinaenda au kinaleta timu mbali mbali za Afrika Mashariki na Kati kuja kucheza hapa bila ya kuhimizwa na wizara. Chama chenyewe tu kikishakuwa kimejipanga vizuri hakina migogoro yoyote, basi kinaendelea na shughuli zake kinaandaa.

Kwa hivyo, jibu ni hilo hilo kwamba *ZFA* ikishakuwa imejipanga vizuri, ina uwezo mzuri wa kifedha, uongozi wake umekaa bila ya kuwa na mgogoro, ina kalenda yake imejipangia basi itaandaa mashindano na ikiomba msaada kutoka Baraza la Michezo au Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa uwezo wetu wa kifedha tutawasaidia. Kwa hivyo, hilo ni jukumu lao.

Mhe. Spika, kukosa kuandaa mashindano hayo hakuuwi vipaji, vipaji vipo vingi nchini na ndio maana vijana wetu wengi Wazanzibari wanachukuliwa na vilabu mbali mbali vya Tanzania Bara na hata nje, ili kuhakikisha kwamba wanakwenda kucheza michezo. Ingekuwa hakuna vipaji basi wasingekuja hapa, lakini kwa sababu vipaji vimekuwa ndio maana vilabu vya Bara ambavyo vinashiriki ligi kuu wamekuja hapa kuona kwamba kuna vipaji na wanachukua vijana wetu kwa ajili hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii ya leo kuweza kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri aliyekaa sasa hivi. Pamoja na maelezo yake mazuri sana na Mhe. Naibu Waziri ameeleza kuwa vyama vyenyewe ndio vinaweza vikaandaa mashindano ya kimataifa katika sehemu zao.

Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi chama chetu cha riadha kikiandaa mashindano ya kitaifa, je wizara yako itasaidia hapo pahali ambapo panapotakiwa?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Makame Mshimba akiwa ni Makamu Rais wa chama chake kwa namna ambavyo anashirikiana na Baraza la Michezo na wizara katika kupanga mikakati ya kuona kwamba mchezo wa riadha hapa Zanzibar unapiga hatua. Kwa kweli analisaidia sana Baraza na wizara.

Kwa hivyo, ninachomuhakikishia kuwa aendelee na mikakati hiyo na kwamba pale ambapo chama chake kitaamua kuandaa mashindano ya kimataifa, basi tutakubaliana na tutashirikiana na Baraza la Michezo na Wizara ili kuona ni namna gani mashindano hayo yanaweza kufanikiwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni lazima tukubaliane kwamba Chama cha Mpira (*ZFA*) na dunia nzima ndio chama ambacho kinakuwa chanzo cha kununua vipaji vya wananchi na wasaidizi wetu.

Mhe. Spika, kwa Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10 mfululizo, mimi humu ndani ya Baraza hili tumekuwa tukishuhudia migogoro ya *ZFA* na kwa vyovyote vile ndio chanzo cha kudumaza mpira wa miguu hapa Zanzibar.

(a) Kwa msingi huo, kama hilo ni kweli na kama hilo waziri anakiri ni kwa nini sasa serikali haiamui kufuta *ZFA*, na badala yake dhamana ya mpira kupelekwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili vijana wetu wakacheza mpira wa kiwango kama ilivyokuwa miaka ya 2000.

(b) Hivi karibuni mpira hapa Zanzibar umesita kwa sababu ya migogoro ambayo haina msingi wowote na vilabu vingi vimeingia hasara, hasa vilabu vya daraja la kwanza Unguja na Pemba. Je, serikali itachukua dhamana sasa kuwalipa fidia wale walioingia hasara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na yeye kwamba *ZFA* ina mgogoro na ndio maana mgogoro wao umekuwa mkubwa kiasi ya kwamba sasa wako mahakamani. Sasa hilo halina ubishi kwamba *ZFA* wana mgogoro mkubwa na wameshindwa kusuluhishana wenyewe kama chama na hatimaye wamefikishana mahakamani.

Kwa hivyo, masuala yakiwa mahakamani Baraza hili haliwezi kuyaingilia sana ndani, kwa kuwa tunakubaliana na hilo kuwa wana mgogoro. Tunasubiri mahakama ifanye maamuzi yake. Sasa hatuwezi kwamba chama kiko mahakamani tuanze kusema tunakifuta, hapana tusubiri maamuzi ya mahakama, halafu tutafanya maamuzi kama serikali.

Mhe. Spika, kuhusu vyama ambavyo ligi yake imesimama na hasara ambazo wamepata. Tutashauriana na Baraza la Michezo baada ya kesi kumalizika tuamuwe tutafanya nini. Sasa hivi siwezi kusema nitafanya lolote na sijui kesi itamaliza vipi. Kwa hivyo, tusubiri kesi itakavyomaliza, Jaji atakavyoiamua basi Baraza la Michezo lipo na wizara ipo tutafanya maamuzi wakati huo.

Nam. 14

Wananchi Kuchelewa Kupata Hati za Viwanja

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi hufika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuchukua hati za matumizi ya viwanja kwa ajili ya ujenzi na kinachobaki ni kwa waziri kuweka saini yake ambapo huchukua miaka mingi kupata hati hizo kutoka wizarani.

(a) Je, wizara haioni kuwa kuchukua muda mrefu kuwapa hati wananchi ni kurudisha nyuma huduma za maendeleo kwa wananchi

(b) Je, wizara haioni kuwa kuchelewa kuwapa hati ya matumizi ya ardhi wananchi kunawapa hasara ukizingatia gharama za ujenzi kila siku zinapanda.

(c) Je, unawaambia nini wananchi ili hati zilizobaki wizarani waje wachukue wenyewe ukizingatia kupata hati hizo ni haki yao ya msingi

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 14 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba kutanguliza maelezo yafuatayo kabla ya kujibu swali (a) (b) na (c).

Mhe. Spika, moja kati ya marekebisho tuliyoyafanya wizarani

UTARATIBU

(*Hapa Mhe. Mjumbe hasikiki vizuri, lakini alikuwa anaomba Mhe. Naibu Waziri aongeze sauti wapate kusikia vizuri).*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Waziri akijibu swali wengi huku hatusikii vizuri.

Mhe. Spika: Anajitahidi ili sauti iwafike wote. Mhe. Naibu Waziri jitahidi ili sauti iwe inasikika kwa wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 14 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba kutanguliza maelezo yafuatayo kabla ya kujibu swali (a) (b) na (c).

Mhe. Spika, moja kati ya marekebisho tuliyoyafanya wizarani ni kuweka utaratibu wa kutoa hati kwa mpango maalum, ili kuondosha mambo yafuatayo ambayo husababisha kuwepo kwa migogoro mingi ya ardhi.

Mhe. Spika, kutia saini hati bila ya kumjua unayemtilia saini kama ndio jina sahihi au ni jina bandia.

Mhe. Spika, kutia saini hati bila ya kujua kuwa hicho kiwanja kipo kweli au kiwanja hicho ameshapewa mtu mwengine. Ili kuepusha haya wizara hutenga siku maalum na kuwaita wale ambao hati zao ziko mizani na kutiwa saini na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa majibu kama hivi ifuatavyo.

(a) Hakuna uchelewaji wa utiaji saini hati kwa utaratibu huu ikiwa yule mwenye hati, anakuwa makini na kafika ofisini pale anapoitwa.

(b) Mhe. Spika, hivi sasa hati ambazo huletwa ofisini kwangu ni hati za hivi karibuni na kwa utaratibu huu nyingi zimeshasainiwa, isipokuwa za wale walioitwa na wasiohudhuria ofisini.

(c) Mhe. Spika, wizarani kwangu hakuna hati isipokuwa ambazo wenyewe huitwa na hawajajitokeza na wanapojitokeza huthibitisha kuwa ni zao na hutiwa saini hati hizo.

Mhe. Spika, utaratibu huu umeleta mafanikio makubwa na wananchi wengi wanashukuru na wanasifu kuwa umepunguza manung'uniko na kuondoa kabisa utaratibu wa kutoa kiwanja kimoja dhidi ya mtu mmoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, napenda niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amejibu kwamba hakuna ucheleweshaji wa kutia saini hati miliki za hawa wenye viwanja, lakini hivi karibuni tu Mhe. Waziri amesaini hati miliki hizo juzi tu ambazo tayari ni karibu miaka mitatu nyuma bado hazijatiwa saini, mpaka ni juzi tu ndio zimetiwa.

Je, Mhe. Waziri atapenda kukiri kwamba kuacha matumizi ya viwanja kwa muda wa miaka mitatu kwa kosa la kusaini tu, viwanja ambavyo vingetumika kwa uwekezaji ambapo uwekezaji huo ungeweza kuingizia mapato serikali kwa kiasi kikubwa, na kukiacha kiwanja hicho kwa miaka mitatu hajasaini. Je, haoni kwa kufanya hivyo kwamba ni kuikosesha serikali mapato. *That is (a)*

(b) Kwa kuwa mwekezaji pengine ameomba hati miliki ya kiwanja na akakaa muda mrefu,wakati mwengine anaweza kuvunjika moyo na kurudi kuwekeza katika nchi nyengine. Haoni kwa kufanya hivyo wizara ni kuwarudisha nyuma wawekezaji na kuikosesha nchi mapato.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni kwamba tangu tumefika kwenye wizara hii, jitihada ya kuona kwamba hati zinatiwa saini tumeichukua. Napenda kumuambia tu kwamba kuanzia mwaka 2012 ambapo niliingia pale wizarani, katika kipindi hicho kweli nilikuta hati za zamani

ambazo hazijatiwa saini kwenye kipindi hicho na niliziita kwa utaratibu maalum kabisa ambao niliupanga kwa makusudi ili kuthibitisha kwamba hatutowi *double location* katika viwanja hivi.

Tarehe 18 niliwaita watu 105, walichomoza watu 95 watu 10 hawakuja, katika kundi hilo zinaweza kuwemo hizo hati za zamani. Tarehe 20/12/2012 niliwaita watu 78 walichomoza watu 60, watu 18 hawakuja. Tarehe 15/05/2013 niliwaita watu 166, walijichomoza watu 136 na watu 30 hawakuja. Tarehe 04/09/2013 niliwaita watu 88, wamejichomoza watu 45 na watu 43 hawakuja. Tarehe 09/12/2013 nimewaita watu 81, wamejichomoza watu 39, watu 42 hawakuja. Tarehe 28/08/2014 niliwaita watu 103, wamejichomoza watu 99 watu wanne hawakuja hapa hali ilikuwa nzuri. Tarehe 10/01/2015 ya mwaka huu niliwaita watu 114, walijichomoza watu 55, watu 59 hawakuja.

Mhe. Spika, katika hizi zinaweza zikawemo hati za zamani ambazo wenyewe hawajaitwa, sijui kama wapo au hawapo. Wanapokuja tunazitia saini, huu ndio utaratibu tunaoufuata pale wizarani. Kwa hivyo, hatucheleweshi wanajicheleweshe wanapoitwa hawaji. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri mwenyewe. Mhe. Spika, swali langu liko hapa moja.

(a) Mhe. Waziri nikupongeze kutokana na utaratibu ambao ulioufanya hivi sasa na kwa kuwa huko nyuma na hasa katika maeneo ya kwetu ya Jimbo la Kitope, kulitokea tatizo la *double location* ambalo lilitufanya mpaka leo na kuelekea kesi zikawa mahakamani na tukashindwa kufanya jambo la maendeleo.

(b) Mhe. Spika, kutokana na utaratibu wako ambao unaoufanya wa kuwaita wananchi. Je, Mhe. Waziri huoni hivi sasa ukatafuta utaratibu uliokuwa mzuri, ukaanzia wilaya au mkoa ili ukarahisisha kazi hizo na ukaweza kuwapata kwa wakati.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, huo utaratibu wa kwenda kwenye wilaya tayari nimeshauanza na nimeshaanza kwa Makunduchi ambako nako pia niliwaita watu na hawakuja. Vile vile nakwenda Pemba siku hizi, hati za Pemba siku hizi haziji Unguja nazifuata mimi huko huko Pemba na nakwenda kuzisaini huko huko, kwa sababu nataka hawa wanaohusika niwaone huko huko.

Mhe. Spika, nataka Baraza hili lielewe kwamba katika utaratibu huu tunagundua mambo ya ajabu kabisa huwezi kuamini, unawaita watu waje anakuja mtu hata hajui kama yeye kaitiwa nini pale. Anakaa mbele yako unamuuliza ehee, wewe bwana kiwanja chako kiko mahala gani. Anasema kwani kuna kiwanja, mimi sijaomba kiwanja. Tena mbona jina lako limefika hapa na kuna picha yako. Mimi sijui, lakini mimi sitaki kiwanja. Utaratibu huu umesaidia sana, ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 19

Mradi wa Kupambana na Kichaa cha Mbwa

Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Aliuliza:-

Katika miaka ya 1990 Zanzibar iliathirika sana na matatizo ya kichaa cha mbwa na watu wengi waling'atwa na mbwa na kuathirika . Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Jumuiya ya Kimataifa ya kuwalinda wanyama (*world Society for the Animals (WSPA))*, iliopo Uingereza tayari wameonesha nia ya kupambana na matatizo ya kichaa cha mbwa.

Je, mradi huu umefikia hatua gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi nambari 19 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa huathri zaidi wanyama aina ya paka na mbwa, wanyama wengine wenye damu ya moto pia nao huathirika na ugonjwa huu.Binadamu huathirika na ugonjwa huu husababishwa na virusi ambao hauna tiba.

Ni kweli katika miaka ya 1990 ugonjwa wa kichaa cha mbwa uliathiri mbwa wengi na watu wengi walitafunwa na mbwa na kuathirika katika kisiwa cha Unguja na kwa Pemba ugonjwa huu uliingia mwaka 2008.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ikishirikiana na washirika wa maendeleo, hususan Shirika la Kuwalinda Wanyama (*WSPA*) na Shirika la Afya Duniani (*WHO*), limechukua jitihada kadhaa za kupunguza athari za ugonjwa huu kwa wanyama na binadamu.

Mhe. Spika, kwa upande wa wanyama kampeni ya kuwachanja mbwa na paka hufanyika kila shehia Unguja na Pemba mara moja kwa kila mwaka hupatiwa chanjo hiyo. Hii inapelekea kupungua kwa ugonjwa kuwapata wanyama wanaofugwa. Inakuwa ni vigumu kuwachanja wanyama wanaozurura na sio wenyewe. Hii ni changamoto kwetu katika kuondoa huu ugonjwa wa kichaa cha mbwa katika visiwa vyetu hivi viwili.

Mhe. Spika, kwa upande wa binadamu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani, limeanzisha vituo vya kutoa chanjo kwa waathirika wanaotafunwa na mbwa katika kisiwa cha Pemba. Kila wilaya imewekewa kituo kimoja cha chanjo, vituo hivyo ni kama ifuatavyo.

Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba Mkoani, Hospitali ya Chake Chake, Wete na Vitongoji *Cottage* ya Micheweni na kwa upande wa Unguja zoezi hilo linatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha 2015.

Mhe. Spika, naomba tu ikumbukwe kuwa suala hili au ugonjwa huu umepungua sana na kesi moja moja tu ndio zinazojitokeza katika kisiwa chetu cha Unguja pamoja na Pemba.

Mhe. BikameYussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Kwanza nichukuwe fursa hii kuipongeza wizara yake kwa juhudi kubwa aliyochukua katika kupunguza kwa asilimia kubwa tatizo hili. Lakini hata hivyo Mhe. Waziri mwenyewe amekiri hapa kuwa kwamba bado kuna changamoto za wafugaji wa wanyama hawa, kuwa baadhi ya wafugaji hawajaona umuhimu wa kuwapeleka wanyama wao hawa katika vituo vya kupata hizi chanjo.

Na kwa kuwa wafadhili wametoa pesa zao nyingi na pia mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuliondoa kabisa tatizo hili, sasa Je, Kupitia changamoto hizi Wizara yako imejipanga vipi na kuwapa mafunzo wafugaji hawa ili kujua umuhimu wa chanjo hizi zinazoendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Kwanza tuchukue shukurani zako lakini wizara yangu inajipanga sasa ili kutumia wataalamu wake wa ndani tuweze kupita kijiji hadi kijiji, na hasa naomba nichukue fursa hii kuliambia Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wawakilishi watusaidie kwenye majimbo yao ili kuona basi wafugaji wanapata hamasa zaidi ya kuweza kuchanja wanyama wao, ili kuondoa athari kubwa ambayo itatokeza hapo baadae. Ikumbukwe wakipata wanyama basi na binaadamu wako karibu sana kupata ugonjwa huo hatari.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize suala moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba hiki kichaa cha mbwa kinawapata wale wanyama wote wenye damu moto na kwa kuwa katika upande wa *costal plain* ya kisiwa cha Pemba katika maeneo ya Vitongoji/Makaani, sehemu za kwao Mheshimiwa Hija huku Muwambe na Micheweni kumekuwa na ongezeko kubwa la mbwa ambao wanaathiri sana mifugo yetu, na kwa kuwa katika sehemu hizi za hapa Forodhani vile vile kuna ongezeko kubwa la paka kiasi ambacho linaathiri sana biashara yetu ya utalii kutokana na wale watalii wanapokwenda pale usiku kununua pizza wanazungukwa sana na mapaka.

Na kwa kuwa hivi juzi tu nimefanya *house budget survey* ilifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuhoji kuna ng'ombe wangapi, kuna paka wangapi, kuna mbwa wangapi. Je. Mhe. Waziri anaweza kuniambia kwa Zanzibar hii tuna paka wangapi, na wangapi wamefanyiwa chanjo hiyo, aidha tuna mbwa wangapi na wangapi wamepatiwa chanjo hizo, *that is* (a).

(b) kwa kuwa hawa wadudu ni wengi; paka na mbwa kuwaua paka sio rahisi lakini ni lini Serikali itafanya *biological control* ya kuwapunguza wale paka pale bila kuwapiga risasi. Na lini Serikali itatusaidia sisi wakaazi wa ardhi ya Makaani wafugaji kule kutupatia magobore kuweza kuwamaliza wale mbwa pori ili wasitumalizie mifugo yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Kwanza niseme tu suala lake la paka wangapi na mbwa wangapi ni suala la kitakwimu naomba unipe nafasi ili niweze kuwapata kitakwimu na nitakujibu kwa maandishi.

Hili suala la pili nadhani tumeanza katika Jimbo la Wawi sehemu ile ya *mortuary* kuwapunguza wale mbwa wengi wanaoathiri pale na mifugo ya pale, lakini hata hivyo hili la Forodhani nadhani tutalichukua suala lako ili tuweze kulifanyia kazi kwa haraka zaidi.

Nam. 56

Ujenzi wa Kituo cha Usarifu Mazao (Kizimbani):

Mhe. Salma Mussa Bilal (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza **:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema ilianzisha mradi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo ya usarifu wa mazao Kizimbani, tangu mwaka 2008 chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea ya Kusini kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la nchi hiyo *KOICA*. Hata hivyo, ni muda mrefu sasa ujenzi wa kituo hicho umesita hali ambayo imepelekea kituo hicho kutofanyakazi na kutofikia lengo lililokusudiwa.

(a) Je, ni lini ujenzi wa kituo hicho utakamilika.

(b) Kwa kuwa vitendea kazi vya kituo hicho vimeshaletwa nchini na vimekaa muda mrefu bila ya matumizi yoyote na baadhi yake vimeshaanza kuharibika. Je, Mheshimiwa Waziri haoni hali hiyo ni hasara kubwa kwa Taifa.

(c) Kwa kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili inaonekana kushindwa kuendeleza ujenzi wa kituo hicho. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja kubwa kwa jengo hilo kukabidhiwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ambayo kwa kiasi kikubwa inahitaji na itafaidika nalo kupitia taasisi yake ya viwango *ZBS*.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 56 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mradi wa *KOICA* wa kujenga uwezo juu ya usarifu wa mazao Tanzania ulitekelezwa kwa pamoja kati ya Wizara ya Kilimo na Maliasili Zanzibar. Chuo Kikuu cha Kilimo – Sokoine Morogoro na Shirika la viwanda vidogo vidogo Tanzania *SIDO*. Ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao – Kizimbani ni moja ya kipengele kikuu cha mradi ambao ulianza mwaka 2008 lakini ujenzi wa kituo cha mafunzo ya usarifu wa mazao ulianza mwaka 2010. Kwa mujibu wa Mpango kazi wa mradi, kazi ya ujenzi wa kituo ilitarajiwa kukamilika baada ya miezi sita (Februari 2010 hadi Oktoba 2010). Hata hivyo, Mkandarasi hakukamilisha kazi hiyo na alikimbia na kulitelekeza jengo hilo likiwa limeshaezekwa mwezi Februari mwaka 2012.

Mhe.Spika, Baada ya kuona ujenzi umesimama Wizara iliwasiliana na *KOICA* na kupewa maelezo kwamba, mkandarasi amekimbia na wao wasingeweza tena kuendelea na ujenzi huo kwa kwasababu muda wa utekelezaji wake kwa mujibu wa taratibu zao umeshapita. Kilichofuata ni *KOICA* iliipatia Wizara michoro pamoja na nyaraka muhimu za kukabidhi jengo hilo pamoja na mashine na vifa vyengine.

Mhe.Spika, Wizara ilidhamiria kukamilisha kazi za ujenzi ili kituo hicho kitumike kama ilivyokusudiwa na ilifanya tathmini ya kazi iliyobakia ili kujua mahitaji ya fedha zitakazohitajika hadi kukamilika kwa ujenzi. Kazi iliyobaki ilikadiriwa kufikia shilingi 500,000,000 za kitanzania na Wizara ilifanya juhudi za kuwasiliana na washirika wengine wa maendeleo ili kusaidia juhudi za Serikali za kukamilisha ujenzi huo.

Hadi sasa Wizara bado haijafanikiwa kupata mshirika wa maendeleo wa kukamilisha kazi iliyobakia. Hata hivyo, Wizara iliendeleza kazi ya ujenzi kwa kutumia fedha za ndani na kiasi cha jumla ya shilingi milioni moja na sabiini za kitanzania zimeshatumika kufanya yafuatayo:-

- Kutia milango 15 ya pamoja na kuweka *security grills* katika milango mitano ya nje.
- Kuweka madirisha ya aluminium pamoja na *vents*
- Kuweka mfumo wa maji safi na maji taka *sewage system* katika jengo.
- Kununua *transforma* mpya na kuunga umeme katika jengo.
- Kuweka tiles, katika sehemu ya ukumbi wa mkutano, darasa, maktaba, *office*, jiko na vyoo.
-

Juhudi bado zinaendelea za kutafuta washirika wa maendeleo kusaidiana nao kukamilisha kazi za ujenzi wa kituo hicho.

Mhe. Spika, Wizara inakubaliana na hoja ya kwamba baadhi ya vitendea kazi kemikali, mipira ya mikono na vifaa vya muda mfupi ambavyo hutumika kwa mara moja vilivyoletwa kwa ajili ya matumizi ya kituo hicho vimeshamalizika muda wake, lakini mashine zote ziko salama. Wizara pia imeshawasiliana na *KOICA* kwa kuleta mafundi wa kuja kuzifunga mashine hizo.

Mhe. Spika, Kama tunakumbuka vyema Baraza lililopita Mwakilishi wa Baraza Mhe. Jaku ulisema hatukupaswa sisi Wizara ya Kilimo na Maliasili kuwapa matrekta yaliyonunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Idara ya Vikosi. Iweje leo mashine zilizonunuliwa na Wizara ya Kilimo kupitia kwa wafadhili wa Kilimo kwa malengo makhsusi ya kutoa elimu kiwa wanafunzi, wajasiri amali na wakulima, kupendekeza kwamba jengo hilo kukabidhiwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Ingawa jumla ya kiasi cha fedha shilingi Milioni mia tatu (300,000,000) bado zinahitajika kukamilisha kazi hizo si vyema kukabidhi jengo hilo kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sababu zifuatazo:-
Malengo ya Wizara juu ya matumizi ya jengo hilo bado yapo pale pale ambapo kituo kimekusudiwa kuwa ni sehemu muhimu ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo – Kizimbani na wakulima.

i. Malengo ya Baadae ya Chuo ni kutoa mafunzo katika ngazi ya *Degree* katika fani mbali mbali za Sayansi ya Kilimo na Chakula, hivyo kuwepo kwa kituo hicho ni muhimu katika kufikia lengo malengo hayo.

ii. Kituo hicho pia kimeainishwa kuwa ni kituo cha Kitaifa cha kutoa elimu kwa Wajasiri Amali hasa kwa upande wa Usarifu wa Mazao na Kilimo na Biashara.

Mhe. Nassor Salim Ali. Ahsante sana Mhe. spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri jibu lake namba mbili alisema kwamba vitendea kazi mipira ya mikono, vifaa na mufa mfupi ambavyo hutumika kwa mara moja vilivyoletwa kwa ajili ya matumizi ya kituo hicho vimeshamaliza muda wake na wamewasiliana na kampuni hii ya *KOICA*, kuja kuleta mafunzi ambao watazifunga mashine hizo.

Je, ni lini mafundi hao watakuja kuzifunga mashine hizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, wenzetu hawa wa KOICA walitupa taarifa kwamba tuwasiliane nao ili waje kufunga vifaa hivyo, na tayari Wizara ya Kilimo imeshatoa barua na pia kuwasiliana nao kwa vipimo ili kuja kufunga vifaa hivyo, kwa hivyo wakati wowote wakati wao tumeshawapa taarifa watatupa taarifa wao siku gani watakuja lakini bado mpaka sasa hawajatupa taarifa sisi tumeshapeleka taarifa yetu.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza suala moja dogo la nyongeza.

Katika majibu yake alisema kwamba kuna mkandarasi kakimbia kuna sababu zozote ambazo zimemfanya mkandarasi huu kukimbia, na ikiwa hakuna sababu ni jitihada gani ambayo watachukuliwa mkandarasi huyu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Kwa kuwa mkandarasi huyu waliingia mkataba pamoja na *KOICA* sisi hatukuwa na mawasiliano naye, lakini mkandarasi huyo sababu zilizomfanya kukimbia wanazijua *KOICA*. Lakini hata hivyo kuna hila ya maneno kwamba mkandarasi huyu wakati alipofanya hisabu ya ujenzi wa jengo lile alipiga hisabu ambayo alikadiria labda itamridhisha, lakini baada ya kuona lile jengo na kuona vile lilivyo halikumridhisha kutokana na hisabu aliyopiga, inasemekana ndio sababu aliyokimbia mkandarasi huyu.

Kwa hivyo suala lake jengine kuhusu hatua sisi hatuwezi kumchukulia hatua kwa sababu sisi sio tuliyeingia naye mkataba.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Wanawake na Watoto wanayo sehemu ya kuweka mashine hizo na kwa kuwa wao wana mradi wa wajasiriamali; Wizra inaonaje ikishirikiana na Wizara ya Wanawake na Watoto ili kuwapa wao wakafunga katika chuo walichonacho ili zikaweza kufanya kazi kwa kuepuka kuja kuharibika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo ni wepesi wa kuombwa na kutoa kwa vitu ambavyo vinahusika, sisi mashine hizi tulinunua tukajenga jengo lile na tukaliweka katika Chuo cha Kizimbani kwa sababu pale tunajua ni mahali ambapo pa Chuo kwa hivyo Chuo ni sehemu moja ya kupatiwa mafunzo na mashine hizi tukimaliza jengo zinakwenda pale kwa kupatiwa mafunzo, na hawa wanawake na watoto nao wana wajasiria mali.

Kwa hivyo ni vizuri kwa kuwa sisi tuna sehemu ambayo ni nzuri na sehemu ambayo tumeweka chuo hao wajasiria mali wao wakaja pale, nina wasi wasi kwamba wao hata mashine hizi tukiwapa watakuwa mahala pazuri pa kuziweka hawana kama sisi ambapo tunapo pale Chuoni ambapo pahala *centere*, kwa hivyo mimi nadhani wanawake na watoto wajasiriamali wao wawalete pale itakuwa pahala pazuri pa kuchukua mafunzo, kuliko kuchukua mashine hizi tukawapa wao, hatujui wataziweka pahala gani.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.
(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, naomba kutoa hoja ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.
Mhe. Spika, moja katika jitihada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein ni kuona kwamba migogoro ya ardhi inapungua au inaondoka kabisa, pengine inaweza ikawa hii migogoro ya ardhi ikawa inasababishwa pengine na utaratibu wetu wa kisheria kwa mtu mmoja kumpa nguvu zote, na ikawa yeye ndio anayetoa *release*, ndio anayetoa hati, ndiye anayetoa kila kitu pengine ndio inaweza ikawa ndio sababu ya kusabisha migogoro ya ardhi. Kwa hivyo Serikali imeona kwamba ni vizuri kurejesha Kamisheni ya Ardhi ambayo sasa itakuwa si mtu mmoja anayeamua kutoa ile *release* ya ardhi, hati na mambo mengineyo kwenye matumizi ya ardhi.

Kwa sababu hiyo ndio maana mbele ya Baraza lako tukufu naleta Mswada huu wa kuwasilisha kurejesha tena au kuanzisha upya Kamisheni ya ardhi ambayo itakuwa na Bodi na itashughulikia na Waziri atabakia kupokea mapendekezo kutoka kwenye Bodi katika kuzisaini hizo hati na mambo mengineyo.

Mhe. Spika, Mswada huu una lengo la kuanzisha Sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa rasilimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo kwa taifa, kwa lengo hilo Mswada huu unapendekezwa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Sheria hii pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, Mswada huu sehemu ya kwanza inaanza kwa jina fupi, ufafanuzi na kuanza kutumika kwa sheria hii.
Sehemu ya pili imeelezea kuanzishwa kwa Kamisheni, kazi zake na uwezo wake.

Sehemu ya Tatu inahusika na Muundo wa Kamisheni, kuanzishwa kwa Bodi ya Kamisheni, wafanyakazi wa Kamisheni, muundo wa bodi, muda wa utendaji kazi wa Bodi, kazi za Bodi, uwezo wa Bodi, uteuzi wa Katibu Mtendaji na sifa zake, Secretariet, vikao vya Bodi na ripoti za Bodi.

Sehemu ya Nne inazungumzia masuala ya fedha za Kamisheni ikijumuishwa na upatikanaji wa fedha za Kamisheni, bajeti na ukaguzi wa hisabu za Kamisheni pamoja na ripoti ya mwaka.

Sehemu ya tano ambayo ndio ya mwisho inatoa maelezo yanayohusiana na makosa na adhabu, uwezo wa Waziri wa kutunga kanuni, kufanya marekebisho ya Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Namba 8 ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, nategemea Wajumbe wameupata Mswada huu na wameusoma kwa muda mrefu na naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Asante sana Mhe. Waziri na hoja imeungwa mkono, sasa mjadala uanze. Naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi Kuhusu Mswada wa Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kny/Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Kwanza kabla ya kusoma naomba nitoe mkono wa pole kwa kifo cha Mhe. Salmin Awadh Salmini, kwa familia yake na kwa wananchi wote wa jimbo la Magomeni, Mwenyezi Mungu atupe subira sote kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa, Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi, Mungu ailaze roho yake Peponi. Amina

Mhe Spika, sasa naomba niendelee kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Sifa zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Kwani ni yeye ambae ametuwezesha kukutana tena leo hii tukiwa na afya njema na uwezo wa kuwatumikia wananchi wetu, hivyo hatuna budi kumshukuru juu ya neema hii aliyoturuzuku.

Mhe. Spika, pili napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, katika kuuchambua Mswada na kwa kuzingatia matakwa ya kanuni zetu, Kamati ilipata nafasi ya kuwaalika wananchi na Taasisi mbali mbali katika kushiriki kutoa maoni yao kwa lengo la kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi na ukizingatia kwamba Mswada huu walengwa wakubwa ni wao, katika kushughulikia ardhi. Hivyo pia sina budi kuwashukuru na kuwapongeza wadau wote waliochangia katika uchambuzi wa Mswada huu kwa namna moja au nyengine, michango yao imesaidia sana Kamati yetu kuweza kufikia lengo.

Mhe. Spika, pia napenda nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kuupitia na kuuchambua Mswada huu. Bila shaka mashirikiano yao yamefanya kazi hii iweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo nitashindwa kuwashukuru Wajumbe wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa umoja wao na bidii yao kubwa katika kuujadili na kuupitia mswada huu muhimu kwa nchi yetu na naomba kuwatambua wajumbe hao kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Marina Joel Thomas	Mjumbe
5.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	Mjumbe
8.	Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu

9. Ndg. Saad Othman Saad Katibu

Mheshmiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba nijielekeze kwenye dhumuni la kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Mswada huu una lengo la kuanzisha Sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa rasilimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo kwa Taifa letu kwa kuanzisha Kamisheni ya Ardhi itakayosimamia masuala yote yanayohusu ardhi.

Mhe Spika, Kamati yangu inapongeza uamuzi huu wa Serikali wa kuamua kuja na Sheria ya kuanzisha Kamisheni ya Ardhi kwani ni dhahiri kuwa masuala ya usimamizi wa ardhi yatakuwa chini ya mwamvuli mmoja nao ni kamisheni na kuondasha utaratibu uliopo sasa wa kuwa na Idara mbali mbali zinazosimamia ardhi, na kila moja kufanya kazi kwa upande wake.

Ni imani ya Kamati kwamba kwa kuanzishwa kwa kamisheni hii migogoro inayohusu ardhi itapungua kwa kiasi kikubwa kwani kutakuwa na usimamizi mzuri wa Kamisheni utakaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria hii, lakini pia kwa kusimamia utekelezaji wa Sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za Kamisheni kama ambavyo zimeorodheshwa katika kifungu 4(2) cha mswada huu ni pamoja na kusimamia masuala yote yanayohusu usajili, upimaji na ramani na matumizi bora ya ardhi. Hivyo ili wananchi waweze kufahamu na kuelewa kwa kina shughuli hizo zinazofanywa na Kamisheni Kamati inashauri ni vyema elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi, kwani kama wengi wetu tunavyoelewa kwamba migogoro ya ardhi huchangiwa pia na kutokuwa na uelewa mzuri wa masuala yanayohusu ardhi miongoni mwa jamii zetu.

Mhe. Spika, Kamati yangu baada ya kuupitia na kuuchambua kwa kina mswada huu umependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuuboresha zaidi mswada huu muhimu, miongoni mwa marekebisho hayo ni kufutwa kwa Kifungu cha 4(2)(p) kinachosomeka “kutekeleza kazi na uwezo uliotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria hii”. Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba Kamati yangu inaamini kuwa Sheria ya matumizi ya Ardhi haijatoa uwezo wowote kwa Kamisheni hii, kwani Kamisheni hii ndio kwanza inaanzishwa na kazi na uwezo wake umetajwa katika Sheria hii tutakayoipitisha na sio vyenginevyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia imependekeza marekebisho katika kifungu cha 5(a) kwa kufuta maneno ‘kutoka katika miamala mbalimbali’ na badala yake kuweka maneno ‘zinazohusu ardhi’. Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka wazi kwamba miongoni mwa uwezo uliopewa Kamisheni chini ya Sheria hii ni kukusanya kodi na ada zinazohusu ardhi tu, kinyume na kifungu kinavyosomeka hivi sasa kinaweka mwanya wa Kamisheni kukusanya ada na kodi kutoka miamala mbali mbali bila ya kuorodheshwa ni miamala ipi hiyo.

Mhe. Spika, Kifungu cha 9(1) pia Kamati imependekeza kuongezwa maneno “angalau mmoja miongoni mwao atoke katika sekta binafsi” Kamati yangu imependekeza marekebisho hayo ili kumlazimisha waziri atakapoteua wajumbe wa Bodi azingatie kushirikisha sekta binafsi kwani katika ulimwengu wa sasa inasisitizwa kuwa wa ushiriki wa sekta za umma pamoja na sekta binafsi, ili zifanye kazi kwa pamoja katika kuleta maendeleo *(Public Private Partnership).*

Mhe. Spika, mbali na marekebisho hayo niliyoainisha hapo kabla, Kamati yangu pia imefanya marekebisho ya lugha na uchapaji kama yanavyoonekana katika marekebisho niliyowasilisha kwako na nakala kusambazwa kwa Wajumbe wako, hivyo natumia fursa hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wayapitie kwa lengo la kuchangia mswada huu.

Baada ya kuyasema hayo naomba Wajumbe wachangie, waboreshe na hatimae waupitishe mswada huu, kwani ni mswada muhimu katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Spika: Asante sana Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Mawasiliano na Ujenzi, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuanza kuchangia na wengine wajitayarishe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana asubuhi ya leo hii kuweza kunipa mimi kuchangia, Sharifu wa Baraza hili na kuweza kutia barka Mswada huu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Kamisheni ya Ardhi.

Mhe. Spika, ni wakati muwafaka, lakini kabla sijaendelea mtu haki yake uweze kumpa na ndipo anapojijua kama ni mtendaji mzuri au ni mtendaji mbaya na usipomuhalalishia suala hili kwa sababu sisi wajumbe ndio tunaotia *right* ambao ndio tunaona. Kwa sababu sisi ndio tunaoongoza wananchi kupitia Baraza lako tukufu.

Kwanza niwashukuru sana watu wa Kamati kwa kuona hili na kutuletea marekebisho waliyoyaona kwa uono wao uliokuwa kwa mujibu wa sheria na kwa upana kabisa, hilo kwanza niwapongeze sana.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri akisaidiwa na Katibu wake. Kuna vitu Mheshimiwa Wizara haiwezi kuleta sheria kama haikutokea tatizo. Mhe. Waziri ameona hili suala kwamba kuna matatizo ndio maana akatuletea sheria. Ina maana Kamisheni ndiyo itakuwa mkombozi na ndio maana utakuta hii *page* ya mwanzo hapa 290 kifungu cha 3 kuanzishwa Wakala wa Serikali inajulikana kama Kamisheni ya Ardhi.

Mhe. Spika, wizara hii ukimuona Mhe. Waziri hajakonda ni kitu ambacho cha kushangaza sana. Ni wizara ambayo ina matatizo mengi sana. Lakini nimshukuru Mhe. Waziri na Katibu wake hawajakonda, lakini hakuna siku isiyokuwa na matatizo kwenye Wizara hii. Nilimsikia leo asubuhi alivyoeleza hapa, alisema kuwa alitafuta utaratibu na ni kweli. Kwa sababu kila mtu anatakiwa kwenye wizara awe na *formality* ambayo ataondoka nayo na ataacha historia. Alitafuta utaratibu mzuri tu.

Mhe. Spika, huko nyuma kusema ukweli ni kilio kitupu. Wananchi walinyang'anywa kiholela ardhi yao, hakuna sheria na wakati sheria tumezitunga sisi hapa wataalamu wa Baraza lako tukufu Mheshimiwa. Zinapingwa ovyo ovyo tu kwa maslahi ya watu, Mheshimiwa Waziri kaweka sheria nzuri, mimi nitakuwa shahidi kwake tena sana tu.

Mimi nilikuwa Mwenyekiti, niseme ukweli ulivyo ya Wizara hii. Mheshimiwa tulipiga kelele nyingi sana. Mwenyekiti ilinibidi mimi nikae sasa nipambane nigeuke wizara na wakati kitu ambacho sio kizuri. Lakini ilinibidi nifanye kazi hiyo kwa sababu nimeona na naona watu wanavyozudhulumiwa ikanibidi mimi nigeuke Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ramadhan Shaaban hakuniwahi kama angeniwahi angelikula raha kwa sababu angepata Mwenyekiti *smart* anajua huyu sasa hivi hapa angenisaidia. Ningemsaidia kwa sheria, ningemsaidia ufatiliaji, na ukweli wenyewe uko hapo.

Mhe. Spika, hii Kamisheni kwa sababu mimi nina wasi wasi na wasi wangu mimi siku zote huwa nauweza, kuwa tunaunda kitu baadae tunakitia mkono. Sasa mimi huwa nakuwa na mashaka makubwa sana, haya mambo ya kutia tia mikono ndiyo inayoharibu hata zile sheria tena ziondoe mkondo wake.

Mhe. Spika, nitamuomba Mhe. Rais anapokaa na Mawaziri na Watendaji wengine hiki kitu akikemee tena akikemee sana kwa sababu sisi tunapata shida, tunaumiza kichwa, kwa kutunga sheria hatulali usiku na mchana, mtuletee Miswada hii, mnatupa *home work* ya kutokwenda kulala kwa sababu tunatafuta jinsi gani marekebisho ya kuweza kusaidia Serikali iende vizuri kwa jamii.

Mhe. Spika, ikiwa mambo yenyewe kutunga sheria halafu zikaishia kwenye *briefcase,* hazina meno zinaingiliwa ingiliwa tu, kwa kweli itakuwa sio jambo zuri sana. Sasa mimi nasema Mhe. Waziri ametueleza leo utakuta mtu anapewa kiwanja hajui mimi niulize nani mtoaji.

Mheshimiwa ikiwa utafiti huo umeupata Kamisheni hii sasa iwe na sheria na mimi najua tukiipitisha hapa Mhe. Rais ataitia saini mara moja, hawa watu wahusika waliotoa viwanja bila ya mtu kujua wakamatwe mara moja, hicho sio kitu cha maskhara. Haiwezekani anaambiwa mtu fulani ana kiwanja, anaulizwa anasema mimi sijui. Hatuoni hatari hiyo, mimi naomba sana nieleze hivyo.

Mhe. Spika, tukenda kwenye madhumuni ya Mswada huu nimeona mimi *paragraph* Sheria inayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi ya rasilimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo.

Mhe. Spika, hiki kifungu kizito sana, ikiwa leo viongozi wa ardhi ndani wao wanafanya uharibifu tufikirie Mheshimiwa, kweli tutakuwa hatuna uongozi imara. Mswada wote uko hapa, hivi vifungu tena vinasema tu, mimi sina tatizo huko kote tayari nimeshapita.

Niko hapa kwenye madhumuni sasa. Mheshimiwa naomba nitoe ushahidi. Kwanza Mhe. Waziri nataka niseme hivi, tuna matatizo kuwa mtu anafutiwa hati lakini mtu anakuwa hairejeshi ile hati husika anai-*claim* ile hati kwa kusema uongo ili ionekane kama ile hati haikufutwa. Nalo hili Kamisheni naona kitu cha mwanzo kitakachoanza kusimamia ilisimamie suala hili, hapo ndipo panapoanza ugomvi Mheshimiwa.

Kwa sababu wewe unafutiwa hati kwa mujibu wa sheria Waziri ana uwezo wa kufuta hati, keshaiyona kuna matatizo, pengine kuna *double location* pengine hati umepata kinyume na utaratibu, pengine umenyang'anya tu kwa mabavu yako, umenyang'anya kwa pesa zako, umenyang'anya kwa kuwa wewe ni kiongozi. Sasa Waziri inampa sheria wala hana hatia kwa hilo.

Mhe. Spika, kuna watu mpaka sasa hivi wanatumilia hati, wanafanya fojari za saini za Waziri wakati ni kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, nina *document* hapa, *document* hiyo imeshafutwa tangu Mhe. Waziri Shamhuna ameifuta baada ya kuona ni koseo limekutikana, Mhe. Shamhuna kafuta. Lakini aliyefutiwa la kushangaza hakurejesha ile *original*. Sijui mnapokuwa mnafuta Mhe. Waziri mnakuwa mnamwambia na yule mtu ailete ile hati au mnafuta kibubu anakuwa hajui. Ikiwa ni kibubu basi tunafanya makoso, la kama mnampelekea ni kosa kuwa nayo akamatwe. Kwa sababu ni kitu ambacho kinatumia sheria na kina nembo ya serikali.

Mhe. Spika, nasikitika sana kuwa leo mtu amefutiwa hati halafu leo Mheshimiwa inaandikiwa barua ambayo inamuhuri wa serikali, inaeleza kwamba hati ile imerejeshwa ikisainiwa na Mhe. Waziri mwenyewe. Mhe. Waziri ana akili hawezi kusaini *double case* hata siku moja na ndio maana akawa anafanya *study* ya aina hii. Nilimchokoza kidogo tu hapa, nilimwambia suala la Wilaya kumbe ndio ameshapita Wilayani mimi nilifikiri hapiti kwa kutafuta watu, ni Waziri wa Kupongezwa tusiseme uongo. Anakwenda Pemba, kwa sababu hakuna utaratibu huo hata siku moja kwamba Waziri anawafuata watu kukabidhi ardhi zao.

Kwa hivyo, Mhe.Spika, hii Hati hii amefojiwa Mhe. Waziri na mpaka leo iko *silence,* huyu mtu anazisambaza katika vituo vya sheria. Mimi nina wasiwasi Mhe. Spika, lazima kuna harufu ya rushwa kwa sababu saini ukitizama na Hati ambayo iliyotolewa katika *lease* ni vitu tofauti hata yule kipofu atasema *it is wrong*, atakataa tu, atasema hii siyo. Huyu mtu mpaka leo anatumia hizi karatasi, tena nataka niseme.

Mhe. Makamu huyu mtu alikuja kwako amekudanganya, naomba sana huyu mtu Mhe. Makamu wa Pili mkamate mara moja, tena mkamate Mheshimiwa kwa sababu anakuharibia Ofisi yako, wanapokuja wao hawauelezi ule ukweli ulivyo, wanaeleza jambo ambalo wanalolitaka wao, lile lilokuwa *affected* kwa upande mwengine hawalielezi.

Mhe. Spika, hii Kamisheni ina kazi kubwa sana, huyu mtu ame-*forge* Hati hajairejesha *forgery* ya Mhe. Waziri, chuma hiki hapa, hii sio *sign* yake Mhe. Waziri kasoma atatia saini kama mtoto mchanga. Mheshimiwa huyu mtu kaja Ofisi kwako huyu.

Sikulaumu Mheshimiwa wangu una wajibu kusaidia kwa wananchi wako, lakini *the time* uangalie *sides* zote mbili tena karatasi hii alivyokuwa huyo mtu akili hana aliipeleka katika vituo vya Polisi. Kapeleka Kiwengwa, sijui kavipeleka wapi, anazidi kuzisambaza na ana jeuri sijui kaipata wapi, mimi ndicho kitu kinachonishangaza. Mheshimiwa naomba sana, Wizara yako hawa watu waliokuja leo hii naisema tu, lakini kwenye Kamati huko ndio nitakapokuja kuogelea sasa. Huku ndio nitakuja kutoa vielelezo ambavyo wewe mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili utalia, vitu alivyofanya ni *forgery* 100%.

Umefanya kazi Mhe. Makamu wa Pili umejaribu kutaka kumsaidia, lakini sheria haikubaliani nayo. Nimeona hii nitoe tahadhari na kama wao vitengo vya rushwa wananisikia na naomba wanisikilize na wanifate *immediately,* ni suala ambalo sijapata kuona katika nchi. Maana yake unajua sheria zetu Mhe. Spika, mara nyingi sana tunakuwa tuna-*quote* na sheria za wenzetu za Jumuiya ya Madola.

Sasa mimi nikiona sheria imepindwa wakati wenzetu Jumuiya za Madola ukipinda sheria inakuhukuju sheria. Sisi mpaka leo huyu mtu anatembea nazo karatasi za *forgery*. Tena huyu Mheshimiwa ni mtaalamu ambaye niseme anatoka mtu ndani ya Ofisi yako, yule hana utaalamu huo. Kwa sababu angekuwa na utaalamu huo ulivyoidai karatasi akuletee kashindwa kukuletea,yaani ni mtaalam ndani ya Ofisi yako. Mheshimiwa, kwa vile suala hili ni kubwa sana nataka huyu mtu awajibishwe kama huyo mtu atatambulikana, tusilichukulie mzaha hata dakika moja, Kamisheni kazi ianze hapo.

Mheshimiwa, mara nyingi sana tunavyounda katika Kamisheni zetu kama hizi, mara nyingi sana tunakuwa kwanza hatuzifanyii *study*. Sasa mimi nina wasiwasi tutaunda na tutakubali, mimi wa kwanza nitamka tu 100% nitaikubali, sina tatizo nalo. Lakini baadae inakuwa ina matatizo, matatizo yake inakuwa vitendea kazi *sometimes* inakuwa na ofisi na baadhi ya vitu vyengine na mafao ambayo kwa mujibu wa sheria tunawapangia za uendeshaji wa Ofisi zinakuwa tahafifu, nalo hili naomba tuliangalie sana.

Mhe. Spika, kwa kweli hili suala tunawaundia kwa nia nzuri, lakini ile *time* tayari wale watu wanakuwa wana masikitiko makubwa sana.

Mheshimiwa, katika uundaji mimi nikubaliane nao kuwa hili tatizo la Kamisheni nitoe rai moja kubwa sana, anasema Kamisheni itakuwa na kazi zifuatazo; kupendekeza na kushauri utekelezaji wa sera za ardhi au kuishauri Serikali kuhusu *programmes* zote za usajili wa ardhi, sasa Mheshimiwa hapa ndio ninapotaka kusema kutoa ushauri wangu.

Mheshimiwa, wewe una *special programme*, ili kwa kuwa duniani kuna kila baadhi ya *changes*, sio *changes* za hali ya hewa tu hata *changes* za sheria zinakuwa zina-*change*.

Ningeomba sana wajaribu na wao kujaribu kuangalia katika dunia kume-*change* vipi, wenzetu ardhi wanatumia vipi, kuna sheria gani ambayo inaweza ikaishauri Serikali na ikaweza ikasaidia kwa wananchi. Kwa sababu sheria nyingi sisi tunakuwa tunazitoa katika akili yetu na ndio maana unakuta sheria zile saa nyengine zinakuwa, nitakuja kusomesha baadae Mheshimiwa wakati wa Kamati, nitaonesha jinsi gani udhaifu wa zile sheria zinavyokuwa maana yake hazifatwi vizuri sheria. Ukiwa na sheria hiyo ujuwe sheria hiyo hata hapa duniani hakuna.

Sasa hili ningeomba sana kuwe na *special programme* ambayo ili zisiwe zina muda mrefu kwa kuishauri Serikali ili kuonesha utaratibu huo. Ningeomba sana kwa sababu mara nyingi sana Kamisheni inakuja mpaka inasinzia inakuwa, Mheshimiwa, namalizia. Kwa hivyo, Mheshimiwa, niseme hivi kwa mara ya mwisho.

Kifungu (e) kinasema; "Kuainishwe viwango na utaratibu wa usimamizi wa ardhi". Mheshimiwa, hata hivyo viwango sasa hivi naomba sana, wataalam tunao, tena wataalam unao mule mule ndani wanaojua kuweka viwango ambavyo vya kisasa, ni kazi yako Mheshimiwa kuwa-*promote* tu, ni kumtoa mtu katika *department* mmoja aliyokuwa nayo sasa hivi na ukamuweka katika *department* nyengine.

Mheshimiwa, watalaam unao wazuri wala huna haja ya kuwatafuta sehemu nyengine yoyote kuongeza mzigo na Wizara yako. Mheshimiwa, Wizara yako ina watu wengi sana na ni kubwa sana.

Mhe. Spika, ili nisiweze kutumia muda mwingi, mimi nikubaliane na wewe, nikubaliane na Mhe. Waziri na Katibu wake mzuri, nimeikubali hii na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope na sasa hivi watafurahi sana hasa kutokana na sheria hii ya Kamisheni itakuwa ni msimamizi wa sheria wa kugomboa wananchi kwa kufata utarabu.

Mheshimiwa, naomba nisimame hapa, lakini nimalizie aliyefanya *forgery* Mhe. Waziri, Mhe. Makamu huyu mtu asiachiwe, jua lisitue leo akamatwe. Kitu alichokifanya ni *forgery,* anakisambaza kwa mujibu wa utaratibu na kuwadhalilisha wawekezaji wetu ili wanaona mpaka sasa hivi Sheria ya Zanzibar inalega lega.

Mhe. Spika, naomba sana naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa Kamisheni ya Ardhi na naipongeza Serikali kwa kuletwa mswada huu, mswada ambao utasaidia masuala mazima ya usimamizi wa ardhi kuwa katika mwamvuli mmoja na kuwa katika chombo kimoja cha usimamizi. Pia, Kamisheni hii ikianzishwa itasaidia kuondosha utaratibu ambao uliozoeleka wa kila siku kuwa kila

Idara ina mamlaka na masuala mazima ya ardhi. Kwa hivyo, kuwepo kwa chombo hiki kitasaidia kuondosha ile kila mmoja mwenye mamlaka ya usimamizi huo.

Mhe. Spika, chombo hiki pia kitasaidia kupunguza migogoro mbali mbali ya ardhi, tumeshuhudia migogoro mingi ya ardhi ilikuwepo, tumesikia masheha wanazungumza mambo mbali mbali kuhusu migogoro ya ardhi, tumeshuhudia Halmashauri nazo zinazungumza kuhusu masuala ya ardhi na migogoro yake. Lakini Mhe. Spika, kuwepo kwa chombo hiki kitasaidia kupunguza au hata kuondoa kabisa migogoro hiyo ya ardhi. Pia, ukiangalia na wananchi nao wanachangia kwa kiasi fulani, wanavamia maeneo ambayo hayastahiki kujengwa, hayastahiki kufanywa shughuli zozote na ukiangalia hata kwenye vyanzo vya maji wananchi wanavamia tu.

Mhe. Spika, lakini kuwepo kwa chombo hiki kitasaidia sana usimamizi, usajili wa ardhi na kusaidia kupunguza kwa asilimia fulani migogoro ambayo inatokana na ardhi.

Mhe. Spika, kumeelezwa humu majukumu ya Kamisheni ambayo moja ya majukumu ya Kamisheni ya chombo hiki ambacho kitaanzishwa ni kusimamia, kusajili, kuhusu masuala mazima ya upimaji wa ramani pamoja na matumizi bora ya ardhi. Kwa hivyo, hapa ilikuwa niombe tu Serikali kupitia Wizara watoe elimu ya kutosha kwa wananchi.

Kwa sababu ikitolewa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu chombo hiki cha usimamizi wa ardhi ambao Kamisheni itakayoanzishwa wananchi watakuwa wana uelewa. Na ukiangalia saa nyengine wananchi wanasababisha migogoro ya ardhi, pengine kutokana na uelewa tu wao mdogo kwa ajili ya masuala mazima ya ardhi. Lakini wakipewa elimu wananchi hawa kuhusu hiki chombo ambacho kinaanzishwa na pengine kitasaidia kuondoa migogoro hiyo.

Pia, tumeshuhudia mtu mmoja anaweza akachukua sehemu tu kubwa ya ardhi, mtu anakuwa na viwanja vitatu au vinne, mambo mengi yametokea na tumeshuhudia, lakini chombo hicho nahisi kitasaidia kupunguza kiasi kikubwa migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati, sipendi kwenda kwenye vifungu kwa sababu vifungu tumevichangia ndani ya Kamati, kwa hivyo, nilikuwa naomba nichangie kiujumla kwa kuipongeza kwa dhati kabisa Serikali kwa kuanzisha chombo hiki, chombo ambacho kitasimamia masuala mazima ya ardhi, chombo hiki kitakuwa mwamvuli na suluhisho ya matatizo ambayo mengi yametokana na migogoro ya ardhi.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kusema hayo, naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na kwa uwezo wake ametujaalia asubuhi hii tumekutana tukiwa wazima wa afya. Nikushukuru pia kwa kunipa fursa hii ya kusema machache sana juu ya mswada huu.

Nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri na timu yake na nianze kwa kusema pia Mhe. Spika, bado napata tabu na napata tabu kwamba sioni tatizo kubwa kwa Zanzibar hii kwamba tuna mapungufu ya sheria. Mimi ninachokiona tuna tatizo kubwa la *commitment* na kama ninavyoona mimi ni sahihi tutaendelea kujenga vyombo hivi, kutunga sheria hii na ile bado tatizo lipo na litaendelea kuwepo hadi pale tutakapokubali wote kwa pamoja, kwamba sasa basi. Tukifikia hapo kwamba sasa basi na tuanze wapi na tufanye nini kwa yule atakayekataa maamuzi haya sasa yale ya sasa basi.

Mhe. Spika, itakuwa tabu kubwa, wanasema "mtoto akibebwa hutizama kile kisogo cha aliyembeba". Sasa kama atapata wito kwa hali hiyo ama vyenginevyo, lakini tujifunze kutoka hapo.

Mhe. Spika, mimi Mwakilishi nina ardhi isiyopungua hekta 200, Waziri wangu ana mia nne, Katibu Mkuu, mtiririko utakwenda hivyo, wananchi wataendelea kupiga makelele, utaratibu haupo na upo lakini hausimamiwi, wasimamiaji si ile sheria lakini ni watendaji waji-*commit* kwamba sheria ni hii tuisimamie iweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa vinavyopungua eneo lake siku hadi siku, nitaendelea kusema kwamba tuliopo hivi sasa wote waliokula kiapo waelewe kwamba wamebeba dhima na watakuwa na cha kujibu siku ikifika. Tunayoyafanya wala hayapotei yanatunzwa mahali ambapo hata nukta haipotei. Ningewaomba sana Waheshimiwa wakubwa jambo hili tusilifanyie mzaha nakutumia nafasi zetu ikawa ndio chaka ya kuchukuwa haki za watu.

Mhe. Spika, utashangaa pia hati miliki ya taasisi na taasisi ni matatizo tunayoyakuta humu tunamopita na Kamati zetu, hii sasa hivi Kamisheni itakuwa ni wakala wa Serikali, lakini hapo juzi ama jana Wizara na Wizara zote ni za Serikali, utajiuliza tatizo linatokea wapi jamani. Lakini ni pale pale nilipoanzia *commitment* bado na kama hiyo bado itakuwa ile ile wimbo "na bado na bado", tutajenga Kamisheni, sheria na tutafanya nini tatizo liko pale pale. Tufike mahali tubadilike kuwatumikia watu kwa haki, uadilifu na uaminifu, hii safari tutaifika, vyenginevyo bado tutakuwa sisi wenyewe tutajipotezea muda, lakini tukijiongezea matatizo kwa sababu tunabeba dhima, tunaapa viapo halafu tunachokiapia hatukifanyii kazi.

Mhe. Spika, mchangiaji wa mwanzo kamanda Mshimba kwa kweli inasikitika kama inafika mahali mtendaji tu aliyemo ndani ya ofisi husika anaweza akafanya kitu cha namna hii na hadi leo yupo anatetea.
Mhe. Spika, tumekubali kuwaita wenzetu wawekezaji na sio wababaishaji, wanapopata taarifa za namna hii tunafikishwa pabaya kwenye uso wa dunia. Tunapochukuliana haya mambo kiudugu udugu, kirafiki kirafiki, kibamkwe kibamkwe, ni weye na yeye, ni mkweo sawa, ni shemeji, ni weye tu, hii Zanzibar ni Wazanzibari, unatia madoa nchi. Umeamua kumpa mwanao au ni mkweo sawa, lakini usimpe ardhi kwa sababu ya jina hilo.

Mhe. Spika, mtu anatumia mkono wake kughushi na bado yupo, ni aibu. Kamisheni haitabadilisha kitu kama watu hawajabadilika, kwa sababu maji ni yale yale tunabadilisha chombo tu; huyu anachukua kaure, huyu anachukua ndoo na yule analeta mtungi, lakini ni maji ya kisima hicho hicho. Waheshimiwa, hapajakuwa na dawa kwa Kamisheni, dawa ni watu wenyewe kubadilika na tubadilike kuanzia kichwani kwenda chini. Narudia kusema; "mtoto anabebwa anatizama kichogo cha aliyembeba" na "kilemba kikitota usiulize mkuki". Kamisheni hii haijawa dawa, tujitathmini sisi ni kweli tutaoana na kamisheni hii na matakwa yake.

Mhe. Spika, nazungumza lugha nyepesi sana ya Kiswahili, tunapitisha kamisheni hii, tumeipamba kwa maneno mazuri, ningewaomba wale wahusika na wadau wote tuheshimu kauli zetu, maandiko yanabaki, vizazi vya leo na kesho vitakuja kutusuta, ardhi inapotea hii, matumizi mabovu yanayofanywa, wanaoyafanya ni wakubwa, ni viongozi na wana dhamana.

Mhe. Spika, sheha ana mamlaka ya ardhi ya hapa, diwani ni hivyo hivyo, *DC* ana mamlaka yake, Mbunge anasema vyake, *RC* ana lake, kamisheni hii tukipitisha na yenyewe halafu...ilimradi ni vurugu, nani ndiye nani hajuulikani. Haidhuru sheria ipo lakini haifatwi, jamani ndio ninachosema mimi kwamba tatizo si sheria, *commitment* bado. Sasa tukikubaliana wote wadau kuwa sasa jamani tunaanza hapa, tuanze hilo.

Mhe. Spika, vyanzo vya maji nayasema sana ndani ya Baraza lako, vyanzo vya maji ni kwamba ardhi hii ni ndogo yenye mahitaji makubwa ya watu wake, hivyo, tunaitegemea hii hii, hebu tugawane vizuri kila mtu afaidike. Si mtu mmoja ama kundi la watu kujiona ndio wenye haki ya ardhi yote ya Zanzibar hii, penye fukwe wao, ardhi ya kilimo wao, ya kujenga wao, basi wahamisheni hao wengine watafutieni pakukaa. Nasema hivi kwa sababu wengine wamo humu ndani wajisikie tu kwamba wanachokifanya si sahihi hata kidogo. Wengine watakaa hapa watapiga makelele, hatupigi kelele ila tunaambiana sisi ndio wenye dhima hii, tukifika siku ya siku isije kusutana mimi hakunambia huyu, Malaika wanakuona na wanaandika na binadamu wenzako tunasimama tunakwambia. Sasa sikio ndio hilo, tunasikia wote lakini kila mtu na maamuzi yake.

Mhe. Spika, mimi nachukua nafasi ya kusema kwa nafasi yangu, haya ninayoyasema yapo yanafanywa, *open space* zote tatizo, kila mahali panauzwa, kamisheni Mhe. Waziri utakuwa nayo mwenyewe, lakini imani yetu ni kwamba haya tunayoyalalamikia kwamba sasa basi. Watakaojaaliwa msimu ujao kurudi ndani ya nyumba hii waje waanze mengine, tuwape matumaini tunaowaita kuja kuwekeza ndani ya ardhi ya Zanzibar, tuwape matumaini wazalendo kwamba hii ardhi ni mali yao, lakini lazima ilete tija na faida kwa nchi hii isiwe ni vurugu hili.

Mhe. Spika, nilisema niseme machache na najitahidi niseme machache hayo hayo niliyoahidi kwa kukumbusha tu ardhi yetu ni chache mno tunahitaji mipango bora na mizuri ya kuipangia matumizi ardhi hii. Mheshimiwa, tujue mahali pakujenga ni wapi na tukubaliane na atakayejenga mahali sipo sheria ichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, vyanzo vya maji viheshimiwe haiwezekani mtu aseme watu ni wakaidi hawasikii, watu sio wakaidi, watu wanasikia na watu wanaelewa, lakini ni kila mmoja kuchukua nafasi yake.

Mhe. Spika, kesho na keshokutwa mipango yetu ya mipango miji hiyo ardhi ndio hii hii tunaongezeka kwa kasi kubwa, tunahitaji ardhi hii kwa shughuli zetu zote. Mhe. Waziri, ningekuomba sana na timu yako na *Inshaallah* na kamisheni hiyo mpya tunayoitarajia waanze sasa kujenga matumaini ya Wazanzibari, kuondoa sasa migogoro iliyoshamiri ya ardhi. Lakini na sisi kada yetu na juu yetu tuone kwamba wenzetu wasiokuwa na kada kama sisi wana haki ndani ya ardhi hii ndio pao hawana pengine.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi nina imani na kamisheni hii kama itataka ushauri tunaoutoa, Mhe. Waziri, akisimama sasa kwamba ndiye wa mwanzo atakayesimamishwa kuulizwa na kujibu watakaokosa haki zao za ardhi yao, angalau basi tuseme sasa tunakwenda safari mpya na tukitia nia hiyo Mwenyezi Mungu atasimama na sisi.

Mhe. Spika, baada ya hayo, mimi nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kabla ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema, lakini la pili, nimshukuru Mhe. Waziri na kumpongeza kwa kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu suala la ardhi katika nchi yetu ya Zanzibar imekuwa ni tatizo na imekuwa ni gumzo kila pembe na imefikia pahala ikawa hakuna ufumbuzi juu ya suala hili zima la ardhi na hajuulikani hasa ni nani mwenyewe mwenye ardhi, kwa sababu kila mtu alipokuwa anachukua mamlaka yake katika suala la kugawa ardhi atakavyo. Ukija huku mara utasikia masheha wamegawa ardhi, mara ofisi za mikoa zinahusika, mara sijui maafisa wa kilimo nao wanaingilia kati.

Kwa hiyo, ilikuwa haijuulikani hasa hili suala nani mwenyewe hasa. Sasa kuja kwa mswada huu, imani yetu kwamba suala hili linaweza likapata ufumbuzi na ile migogoro na ghasia ambazo zilikuwa zikijitokeza basi zinaweza zikatoweka kabisa na nchi yetu ikapata amani katika suala hili.

Mhe. Spika, suala la ardhi mpaka majuzi tu nimepata kusikia katika vyombo vya habari, nimemsikia Mkuu wa Wilaya ya Magharibi namna alivyokwenda katika eneo lake na kuwakuta watu tayari wameshajenga katika maeneo ambayo hayastahiki. Sasa hivi maeneo ambayo Serikali ilikuwa imetenga kwa dhamira ua kwa malengo maalum basi imekuwa ni kimbilio la wananchi katika kuvunja sheria na ardhi ile kuitumia pasipo na utaratibu. Kwenye vyanzio vya maji watu wameingia mpaka katika maeneo ambayo hayastahiki.

Vile vile, watu sasa hivi wameingia mpaka kwenye kambi za jeshi maeneo ambayo yametengwa kwa shughuli maalum za kiulinzi. Sasa hii ni hatari kwa nchi yetu, sasa unakuwa unabaki unajiuliza inakuwa kuwaje watu tangu wanaanza kupima na kujenga misingi nyumba zinasimama mpaka zinajengwa,lakini taasisi zinazohusika inakuwa imefungia macho yale masuala na haionekani na hatimae sasa tunakuwa tunatumia nguvu dakika za mwisho na kuleta athari na manung'uniko kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, hayo ni baadhi tu ya maeneo…

(Hapa kipaza sauti hakikusikika)

Mhe. Spika, naomba niendelee, sasa sijui nianze mwanzo maana yake yale yatakuwa yamepita hewani, naomba muongozo wako.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa sababu kumbukumbu zangu zilikuwa hazisikiki katika vyombo vinavyostahiki.

Mhe. Spika, nilikuwa nazungumzia suala zima la migogoro na nimejaribu kutaja baadhi ya maeneo, lakini pia, nimempongeza Mhe. Mkuu wa Wilaya kwa jitihada anazozifanya kwa kwenda katika maeneo ambayo wananchi walijenga pasipokuwa na kufuata utaratibu, nasema hii kadhia ilikuwa ni ya muda mrefu na tulikuwa tunajiuliza hasa nani mwenye ardhi hapa Zanzibar mpaka watu wakaanza kutafuta majina na kusema kwamba ardhi ya Zanzibar imekuwa ni shamba la bibi, kila mtu ana haki ya kwenda kulima na kwenda kuvuna anavyostahiki.

Mhe. Spika, sasa kutokana na Mhe. Waziri kutuletea mswada huu imani yetu yale matatizo na migogoro yanaweza yakatoweka kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilikuwa nataka niongezee ni suala alilozungumzia Mhe. Mshimba, hapa suala la *forgery* ya saini katika *document* ambayo yeye Mhe. Mshimba, anayo.

Mhe. Spika, hili suala ni la hatari, nasema hii ni *document* moja tu ambayo Mhe. Mshimba, ameweza kuikamata na kuileta hapa mbele ya Baraza, lakini tuna imani kwamba kuna nyingi ambazo mtu huyu inawezekana ameshazifanya. Sasa niombe Mhe. Spika, kupitia chombo chako taasisi zinazohusika juu ya suala hili la *forgery*, basi walifuatilie suala hili na kulifanyia kazi na kupata ufumbuzi juu ya tatizo ambalo limejitokeza.

Mimi alinileta kidogo nikajaribu kuangalia tu kidogo hapa kwa haraka haraka, hii saini kama utakuwa mchunguzi, mimi si mchunguzi wa saini lakini kwa haraka haraka ukiiangalia tu kwamba saini iliyotiwa na iliyofojiwa zina tofauti kubwa sana na hutaki kujiuliza masuala pindi unapoiangalia.

Mhe. Spika, kingine ambacho ninataka nikizungumzie kabla sijaingia katika mswada. Sasa hivi kumejitokeza tatizo kubwa sana katika nchi yetu ambalo hata Mhe. Asaa, alijaribu kuligusia sana, suala la kujengwa maeneo ya *open space*. Maeneo haya waliyoyatenga waliyatenga kwa dhamira nzuri sana, kuna maeneo ya kuchezea watoto, kuna maeneo ya kufanya shughuli za mitaani pindi linapotokezea tatizo na kuna maeneo ya kiusalama pindi linapotokezea janga lolote wananchi kuweza kukimbilia pahala na kutulia katika lile janga ambalo linaweza likatokezea kwa muda ule.

Mhe. Spika, sasa maeneo haya kila siku kukicha basi utakuta maeneo haya yanajengwa na la kushangaza zaidi wajenzi wa maeneo haya sio wale watu wa kawaida tu, ni watu ambao wanakuwa ni mashuhuri na watu ambao wana nyadhifa katika nchi hii.

Maeneo yote ya wazi ukifuatilia utaambiwa lile la fulani, lile fulani na lile la fulani, sina haja ya kuyataja, lakini kama Mhe. Waziri akiyataka akiniambia nimuandikie punde tu hapa nitamuandikia wala muda sio mrefu maeneo ambayo yalikuwa ya wazi na yalikuwa na shughuli maalum za kutumia, lakini sasa hivi maeneo hayo yamekuwa yakijengwa. Kwa hivyo, ni suala ambalo kwa kweli linawea kutupa mashaka katika nchi yetu kwamba tutafikia pahala tutakuwa hatuna eneo la kufanya shughuli yoyote la kihuduma kwa wananchi kutokana na hali halisi ya ardhi kugaiwa kiholela katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo, naomba nichangie mambo kama matatu tu sio mengi katika mswada huu ulioletwa mbele yetu.

Mhe. Spika, nataka niingie katika ukurasa wa 291, kifungu kidogo hapo juu kabisa kimeandikwa kamisheni itakuwa na kazi zifuatazo. Sasa mimi nilikuwa nataka nizungumze tu katika kifungu cha (b) na (c).

Mhe. Spika, huu mswada umekuja katika lugha ya Kiswahili na Kiswahili ni kipana na Kiswahili kina nyanja nyingi na kila mtu anakifahamu. Sasa kinanipa mashaka pale palipoandikwa kwamba kifungu (b) kinasema;

"Kuishauri Serikali kuhusu *programmes* zote za usajili wa ardhi Zanzibar".

Kwa bahati Mhe. Haroun, leo ametoka lakini angetusaidia, lakini mimi tu kwa uswahili wangu mdogo, nahisi kwamba tungeandika kuwa "kuishauri Serikali kuhusu taratibu zote za usajili wa ardhi Zanzibar".

Pia, ukiangalia katika kifungu (j) vile vile kimeandikwa;

"Kutekeleza na kukuza *programmes* za elimu zinazohusu matumizi ya usimamizi wa ardhi kwa madhumuni ya kujenga uelewa kwa umma na kutambua umuhimu wa kulinda na kuendeleza ardhi".

Sasa pia ningeomba tujaribu kutafuta lugha ya Kiswahili, Kiswahili chepesi mlichokitumia hapa mimi nahisi ingekuwa sio vibaya kama tungeandika kutekeleza na kukuza taratibu za elimu zinazohusu matumizi ya usimamizi. Hiki ilikuwa ni Kiswahili changu mimi, lakini kama kuna Kiswahili kingine ambacho kinaweza kutumika basi ni vyema tukaandika Kiswahili fasaha kuliko kuwa tunaandika Kiswahili na Kiswa*nglish*.

Mhe. Spika, ukurasa wa 293, imeanzia 292 kuhusu Muundo wa Bodi. Muundo wa bodi katika kifungu cha 2(a) ili nafasi aliyopiwa Mhe. Waziri imeandikwa hapa wakati waziri anateua Wajumbe waliotajwa katika hii aya ya (e) atalazimika na kuzingatia sifa zifuatazo:

Imeandikwa tu Mzanzibari, utaalamu na uzoefu angalau wa miaka saba katika fani ya ardhi; uwekezaji, mazingira, utawala, uchumi au sheria. Mimi ningeliomba suala moja kutoka kwa Mhe. Waziri, hili naomba atusaidie sana hasa, pamoja na sifa zilizotajwa basi miongoni mwa watu watatu ambao Mhe. Waziri amepewa mamlaka ya kuteuwa kuwa Wajumbe wa Bodi basi angesema kwamba angalau nafasi moja awe mwanamke ili kuangalia *gender*.

Mhe. Spika, sasa hivi ulimwengu tuliokuwanao tunajaribu sana kuona kwamba wanawake nao tunawapa kipaumbele katika kila nyanja zinazostahiki katika kutumikia nchi yetu. Sasa nafikiri Mhe. Waziri angetuainishia kidogo kwamba miongoni mwa sifa hizi pia alikuwa atuandikie angalau miongoni mwao mmoja basi awe mwanamke ili tupate na wanawake kuingia katika bodi yetu hii ili kuweza kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo nataka nilizungumzie katika mswada huu ni katika ukurasa wa 295, kifungu cha 20 kuhusu Posho kwa Wajumbe wa Bodi. Naomba ninukuu kifungu hiki.

Kifungu cha 20 kinasema kwamba;

"Wajumbe wa Bodi watalipwa kutoka katika bajeti ya Kamisheni, posho na malipo mengine kama waziri kwa kushauriana na waziri anayehusika na masuala ya fedha atakavyoamua".

Mimi nataka ufafanuzi nije nisaidiwe kidogo sijafahamu, hii kama waziri imekusudiwa vipi? Kama waziri maana yake kama stahiki za waziri anazolipwa au kama waziri kivipi. Sasa kidogo kifungu hiki kinanipa mashaka sana. Mhe. Waziri atapokuja kutoa majibu basi atatusaidia hiki kima cha kulipwa Wajumbe wa Bodi hii kama waziri imekusudiwa kitu gani.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii nikatoa mchango wangu mdogo katika mswada huu wa kuanzishwa Kamisheni ya Ardhi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa kuleta mswada huu wa kuanzisha kamisheni hii ya ardhi wakiwa wana malengo mazuri kabisa, lakini pia, nataka nichukue fursa hii kuipongeza Kamati nayo kwa marekebisho yao waliyoyafanya katika kupitia mswada huu na mimi naungana nao.

Mhe. Spika, sheria ni nzuri na sheria sisemi kuwa imekuja wakati muwafaka, kwa sababu tumeshuhudia migogoro mingi tu ya ardhi ambayo imejitokeza katika kisiwa chetu hiki na mpaka leo mingine haijapatiwa ufumbuzi. Sasa sisemi kuwa kwa asilimia mia moja mswada huu umekuja wakati muwafaka.

Mhe. Spika, tunajua kwamba kisiwa chetu cha Zanzibar ardhi tuliyonayo ni ndogo, lakini hiyo ndogo iliyopo inatumika vibaya sana. Katika migogoro mingi ya ardhi ni kuchukuliwa ardhi na kuuzwa kiholela kitu ambacho wanaofanya mambo haya wanajulikana, lakini hatua za kisheria hazichukuliwi. Kwa sababu ni wao kwa wao na hawawezi kushtakiana wala kuchukuliana hatua yoyote ile.

Sasa imefika pahali matumizi ya ardhi Zanzibar yamekuwa mabaya na wala hayana mfano, imefika pahala mpaka watu kuuza eka kitu ambacho si ruhusa mtu kuiuza eka, lakini kwa asilimia kubwa sasa hivi eka zilizogawiwa basi watu ikiwa ni rasiliamli yao kubwa na wamefika pahali eka hizo kuuzwa. Kama hawauzi wao waliogaiwa basi masheha na wakuu wa mikoa ndio washirikishaji kikamilifu kwa matatizo ya kuuza maeneo hayo ya eka.

Mhe. Spika, katika mswada huu sehemu ya Madhumuni na Sababu. Mhe. Wazirim ametueleza kuwa lengo la kuanzisha sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa rasilimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo ya Taifa. Kama Mhe. Waziri hili ndilo lengo lake kubwa basi aje hapa atueleze kwanza ardhi zilizochukuliwa bila ya mpangilio au bila ya watu kuwa na ukabidhi wa ardhi zile wa kisheria.

Je, katika kusimamia hili waziri atwambie kuwa atachukua hatua gani katika kuzitafuta ardhi hizi na kuzirudisha zikawa ni mali ya Serikali kwa wale wote waliochukua ardhi kinyume na sheria, kama lengo lake kakusudia madhumuni na sababu ni hiyo.

Mhe. Spika, katika matumizi ya ardhi siku zote masuala haya tunazungumza kuna watu wananyang'anywa ardhi bila ya sababu za msingi, kupewa watu waliokuwa ardhi zile hawana matumizi nazo. Kipindi kimoja niliuliza hapa kuna maeneo kadhaa ambayo kuwa wananyang'anywa watu kwa ajili ya kutumia ardhi ile kwa kilimo na kupewa watu ardhi zile hawana matumizi nazo ya msingi, alimradi apewe tu, wanyang'anywe watu wanaotafuta rizki na kwenda kupewa mtu aliyekuwa Mwenyezi Mungu kamjaalia uwezo wake, akachukuliwa kuwekwa pale kwa ajili tu ya kuwa mtu fulani ni mkubwa wa pahala fulani.

Kwa hiyo, matumizi haya ya ardhi yamekuwa yakitia unyonge sana kwa wale waliokuwa ni watu masikini na kufikia pahali kuwa wao kuona katika nchi hii hawana haki.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri, aje atwambie kuwa haya yote amekusudia kuyarekebisha vipi mambo haya, kuzitafuta zile ardhi ambazo zilichukuliwa na watu ambazo hawana shughuli nazo.

Mhe. Spika, kifungu cha 5 kuhusu Uwezo wa Kamisheni. Mimi niungane na Kamati kwa Mhe. Waziri kuja kutupa ufafanuzi wa kifungu hiki cha 5(a) ambacho amesema kuwa Kamisheni itakuwa na uwezo ufuatao: Kukusanya ada na kutoa kodi katika miamala mbali mbali, hii miamala bora angetuwekea ufafanuzi ili ikaweza kutambulika kuliko kutia neno kama hili lililokuwa hatulijui ufafanuzi wake ukoje.

Suala jengine kifungu cha 9 katika Muundo wa Bodi. "Bodi itaundwa na; (a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais; (b) Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi; (c) Katibu Mkuu mwenye dhamana na masuala ya Mamlaka za Mikoa; ndio hao halafu kuna (d) Naibu Mwanasheria Mkuu na (e) Wajumbe wengine watatu wanaoteuliwa na waziri. Mimi nipendekeze hapa kuwa miongoni mwa Wajumbe watatu wataoteuliwa na waziri basi angalau Mhe. Waziri atuwekee ufafanuzi kuwa na mwanamke mmoja awemo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine kuna hii bodi, kwa sababu ardhi ina matumizi mengi, inatumika kwa masuala ya kilimo, lakini ardhi hiyo hiyo inafanyiwa kazi na ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo ni ofisi ya mazingira; kuna hawa watu wa *ZIPA* wanaoshughulika na uwekezaji. Sasa katika bodi hii naona bado hakuna watu hao wanaotajwa kwa ajili ya kushughulikia na wao katika masuala mazima haya ya usimamizi huu wa masuala ya ardhi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija anifahamishe ili na mimi nifahamu kwa nini watu hawa pengine kutoka mjumbe mmoja kwenye wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini kuna wawekezaji hawa pia humo hutokea migogoro, ambapo pengine watu wa mazingira na hawa wa *ZIPA* hawajakubaliana wakafika pahali ikatokea migogoro katika wawekezaji. Sasa ni sababu zipi ambazo pengine wajumbe hawa hawakuingizwa katika eneo hili.

Mhe. Spika, pia, kuna Kanuni za Bodi ambazo kifungu cha 2 kuhusu Kamisheni katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa masharti ya fedha zilizopatikana itatumia fedha hizo kwa malipo yote posho, misharaha, gharama za kazi na malipo mengine yatakayojitokeza ikijumuisha matumizi makuu.Fedha ya vianzio vya kamisheni vitakuwa kifungu (b) ada, kodi ya ukodishwaji wa ardhi na tozo zitazokusanywa na Kamisheni. Hizi kodi za ardhi Mhe. Waziri, hebu akija anifahamishe pengine sijafahamu vizuri, kodi hizi zitatokana na wale wawekezaji wakubwa wakubwa tu au zitatokana na wakodishwaji wa aina gani ambao watatozwa hizo kodi.

Mhe. Spika, mimi niseme kuwa...Samahani kuna suala moja nilikuwa nimeshalisahau katika ule Muundo wa Bodi. Kuna kifungu cha 2(b), utaalamu ambao wakati waziri anateuwa wajumbe waliotajwa katika aya (e) atalazimika kuzingatia sifa zifuatazo; awe Mzanzibari na utaalamu na uzoefu angalau miaka saba katika fani ya ardhi. Pia, naomba Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi hapa huyu mtaalamu anayetakiwa na uzoefu wa miaka saba katika fani ya ardhi ni mtaalamu gani.

Mhe. Spika, kwa sababu mimi nimeshawahi kusema hapa kuwa bado tuna watoto wetu wamo ndani ya vyuo mbali mbali na wao pia hufika pahali wakatafuta ajira. Sasa kusema siku zote katika sheria kuwa wataalamu wanaotakiwa wawe na uzoefu usiopungua miaka saba, miaka mingapi wa fani ile, hatuoni kuwa na hawa wanaotoka kwenye vyuo wanafika pahali nao wanatafuta hizi ajira? Kwa sababu gani iwe lazima uzoefu unaotakikana uwe wa miaka saba.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono, lakini Mhe. Waziri akija maelezo yangu aje anipe ufafanuzi ili nipate kuelewa zaidi. Ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kupata fursa ya kutafuta machache niliyonayo kuhusu mswada huu wa kuanzishwa kwa kamisheni ya ardhi.
Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii kukutana hapa katika shughuli zetu za kawaida za kazi zetu. Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nimpongeze sana waziri kwa kuleta mswada huu mbele yetu na tukaanza kuujadili.

Mhe. Spika, Zanzibar kabla ya Mapinduzi, ardhi ilikuwa inamilikiwa na watu binafsi, wakati huo kila *centimetre* moja ya ardhi ilikuwa ina mwenyewe kama iko mjini, kijijini, shamba au msituni. Ushahidi wa hayo kama mtu atakwenda kwenye msitu kutaka kulima lazima atatokea mtu amhoji kwa wakati huo kuwa nani aliyekupa ruhusa ya kulima hapa kwa sababu ni sehemu yangu.

Mhe. Spika, baada ya Mapinduzi, mfumo wa kumiliki ardhi Zanzibar kwa kima fulani ulibadilika. Rais wa Kwanza wa Zanzibar alitangaza kuwa ardhi ni mali ya Taifa, kwa hivyo, sehemu kubwa ya ardhi ikagawiwa kwa wananchi waliobahatika kupewa eka tatu, tatu, wengine walipata mashamba kwa kule Pemba ya mikarafuu, wengine mabonde ya kulima, alimradi walipewa eka tatu, tatu kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao mbali mbali. Kwa hivyo, sehemu zilizobakia ikawa wanamiliki watu wenyewe na nyengine ikawa ni sehemu za Serikali kwa shughuli za kiserikali.

Mhe. Spika, ardhi yetu ya Zanzibar ina mambo kadhaa muhimu na kama tukiendelea kutumia vibaya ardhi tutaharibikiwa, tumeshaanza kuharibikiwa tutaendelea kuharibikiwa na mambo yetu.

Mhe. Spika, ardhi ina sehemu ya vianzio vya maji, ina sehemu ya mabonde ya kilimo, ina sehemu nyengine kadhaa za wazi na zile ambazo zinaruhusiwa kisheria kufanya ujenzi wa nyumba, mahoteli, uwekezaji na kadhalika. Lakini kwa kukosa mpango mwema wa matumizi ya ardhi hatuoni wapi pa maji, wapi pa kulima, wapi pa kujenga, tunachanganya mambo.

Sehemu za maji tunazifanya kuwa ni sehemu za kujenga, mabonde ya kilimo tunayageuza sehemu za kujenga. Hivyo, hatimaye baada ya muda mfupi ujao kama hali hii tutashindwa kuidhibiti Zanzibar badala ya kuwa zamani watu wanatafuta mafuta wanapata maji, sasa wanatafuta maji wanapata chumvi kwa sababu ndio iliyopo baharini, chumvi haipotei na ardhi yetu tayari inaanza kumegwa na chumvi au bahari kutokana na uharibifu wetu wa mazingira katika sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, si hasha iko siku itakuwa maji yetu ya kunywa ni yenye chumvi zaidi kuliko yale maji matamu na mazuri tulioyazowea hapo kabla.

Mhe. Spika, tunaanzisha Kamisheni ya Ardhi tukitarajia kuwa itaweza kusaidia kurekebisha, kupunguza, pengine kuondoa matatizo mbali mbali ya ardhi yaliyopo hivi sasa.

Mhe. Spika, kamisheni hii ilipoanzishwa ni wakala wa Serikali, kwa hivyo, ni Kamisheni ya Serikali. Kwa hivyo, itatarajiwa ifanyekazi kubwa, ngumu na muhimu ili kuweza kuondoa matatizo na migogoro mbali mbali inayotukabili katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kamisheni hii kwenye muundo wake nimeona kuwa kamisheni ina muundo kuna Idara ya Ardhi, Idara ya Ukaguzi na Upimaji, Idara ya Mipango Miji na vijiji na ikatajwa kuwa Mhe. Rais anaweza kuongeza Idara nyengine ambayo inafaa.

Mhe. Spika, hasa hii kamisheni inaonesha kuwa ina idara hizi tatu kwa hivi sasa, lakini ni chombo kipi ambacho itazikusanya hizi idara kuonesha kuwa ina uongozi kwa sababu hapa hii kamisheni haijaonekana kuwa kuna Uongozi wa Kamishenim inaonekana tu kuwa kuna Idara za Kamisheni na Kamisheni yenyewe sijaiona iko wapim pana idara zake tu, pengine kama sijasoma Mswada wote Mhe. Waziri atanijibu vizurim atanambia tu kuna katika Mswada huu, hii sehaemu iko pahali kadhaa. Lakini hii kamisheni imeundwa tu kwa hizi idara, sijaona kuwa kuna Mwenyekiti.

Ningeomba Mhe. Waziri hili hatimae tuweze kuliona na imekuja zimetajwa kazi zake mwanzo kabla ya hiyo kamisheni yenyewe haijatajwa pengine ingekuwa vyema, kwanza ikaja ule Muundo wa Kamisheni tukaona kuwa kamisheni yenyewe ndiyo hiyo na baadae ikafata zile kazi zake, lakini zimekuja kazi mwanzo kabla ya ile kamisheni yenyewe.

Mhe. Spika, lakini hii kamisheni ina kazi kadhaa ambazo zimetajwa hapa. Mimi nitazitaja chache kati ya kazi hizo na kujaribu kutoa maelezo na kuomba ufafanuzi zaidi. Kazi za Kamisheni zimetajwa katika ukurasa wa 290 hadi 281, nitaanza kazi moja ya kamisheni hii kifungu (d) inasema;

"Kusimamia mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi Zanzibar".

Zanzibar inaonesha kuwa tunao Mpango wa Taifa wa Matumizi ya ardhi yetu. Lakini kwa kuwa tumeunda kamisheni ili isimamie ina maana huo mpango wa Taifa sasa hivi hauna usimamizi. Kwa hivyo, kamisheni hii tunaipa kazi kubwa na nzito ya kusimamia matumizi ya ardhi yetu. kuwe na mipango mizuri na maelekezo mazuri namna ya kuweza kutumia ardhi yetu kwa manufaa yetu wenyewe.

Mhe. Spika, niende katika kifungu (h) kinasema;

"Kusimamia masuala yote ya Ukaguzi na Upimaji Zanzibar".

Hasa huu Ukaguzi na Upimaji, Idara hii katika idara zilizotajwa. Sasa hii isingelikuwa kazi kwa sababu ni idara, miongoni mwa Idara za Kamisheni hii ni moja katika idara. Lakini hapa imetajwa ni kama sehemu ya kazi. Lakini ningeliomba Mhe. Waziri anisaidie pale ambapo atakuja kuleta majumuisho ya shughuli hizi.

Mhe. Spika, niende katika kifungu (i);

"Kuratibu kazi za Taasisi zote zinazohusiana na ardhi na kuwa kiungo cha mawasiliano baina ya Taasisi hizo na Serikali".

Mhe. Spika, Kamisheni hii tunaipa kazi kubwa na nzito, kwa sababu ardhi yetu inatumika au inatumiwa na taasisi mbali mbali ambazo tayari wanamiliki au wamepewa ardhi hiyo kwa kutumia na sasa tunataka kamisheni iweze kusimamia na iwe ni kiungo kwa wanaotumia ardhi hiyo na Serikali.

Mhe. Spika, sasa ardhi yetu niseme tutaigawa kiholela sana tushajenga katika ardhi kiholela mno tumeacha na kuruhusu vyanzo na mabonde kutumika kinyume na taratibu zinazohusika. Hasa kuanzisha kwa kamisheni ili kuweka mambo yaende vizuri kwa upande mmoja ni kuanzisha migongano na mivutano na watu ambao wamemiliki ardhi hizo na kuzitumia vile ambavyo ni kinyume na taratibu ya kutumia hiyo sehemu.

Niseme kuwa kwa kiasi fulani Serikali kukaa kimnya kutuwaachia wananchi hata kwa sehemu mtu ya kwake mwenyewe atajenga pahala ambapo si pa kujenga, akalima pahala ambapo si pa kulima na akaweka kitu chochote kule ambapo sio chake na Serikali ikawa inamtizama tu na hatimae ikamgeukia ikamwambia hapa sio pa kufanya hiki, ila ni kufanya hiki, ni kuongeza migogoro baina ya taasisi husika na mtu husika anaefanya kazi ile. Kwa hivyo, tunaipa taasisi hii tunayoianzisha kazi kubwa na itabidi iwe na kazi za ziada ya kufanya hii taasisi.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kuzungumza kidogo ni kifungu (k).

"Kuzipitia Sheria za Ardhi zilizopo na kupendekeza kufanya marekebisho".

Kama kuna sheria zote za ardhi ambazo zitakuwa haziendani na muundo wa hii kamisheni, kwa hivyo, ningeomba wizara husika ifate sheria hizo ili zifanyiwe marekebisho ziende na zikubaliane na sheria hii ambayo leo tunakaa hapa kuitunga kwa ajili ya kupata uongozi bora wa nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu (n) kinasema;

"Kushauri na kusimamia Maendeleo ya Uhifadhi wa Ardhi".

Mhe. Spika, Ardhi Zanzibar inabidi watu wapate elimu ya kutosha, sasa hivi tuna upimaji wa ardhi sehemu mbali mbali. Watu kwa kuwa huko nyuma mara tu baada ya Mapindizi walinyanganywa na Serikali au Serikali ilichukuwa hiyo ardhi, leo kwenda tu Maafisa wa Ardhi kujaribu kupima, watu wanaweza wakakataa au wakaficha sehemu zao kwa ghofu kuwa Serikali inarudi kule kule nyuma.

Mhe. Spika, kabla sehemu fulani haijafanyiwa upimaji rasmi watu wa maeneo yale wapewe taaluma na elimu waelimishwe kuhusu umuhimu wa sehemu zao kupimwa kwa kisheria, vyenginevyo watu wataingia ghofu kuonesha kuwa hapa ni miliki yangu naomba nipimiwe, wataona kuwa ni ujanja wa Serikali kwa sababu Serikali imeshachukuwa sehemu nyingi za mali za watu.

Kwa hivyo, watu wengine zaidi wenye umri zaidi wa wangu kama wako wanaweza wakawa na ghofu wakiambiwa kuwa sehemu yako kesho inataka kupimwa, watakuwa na ghofu nao juu ya huu upimaji.

Kwa hivyo, inabidi elimu ya kutosha itolewe ili watu waelewe kuwa huo ndio utaratibu wa kiserikali kuweka mpango mzuri wa matumizi ya ardhi yetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na Mswada huu tumeupitia vizuri naunga mkono hoja na natoa ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mchana huu kuwepo katika Baraza lako hili kwa ajili ya kuendeleza shughuli zetu za kawaida.

Pili, nachukuwa nafasi kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Ardhi kwa kutuletea Mswada huu uliopo mbele yetu ambao kwa kiasi fulani utasaidia sana ikiwa utatekelezwa kama ulivyokuusudiwa kuuweka mji wetu wa Zanzibar kuwa na mazingira mazuri ya kuondoa migogoro ya ardhi na hata kuweka mipango miji na vijiji vizuri.

Mhe. Spika, nampongeza tena Mwenyekiti ambaye aliwasilisha ripoti hii kwa ufasaha na kwa vizuri sana.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nianze mchango wangu kwenye ukurasa wa 297 kwenye madhumuni na sababu.

Mhe. Spika, Madhumuni na Sababu ya Mswada huu una lengo la kuanzisha sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa rasimali ya ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo kwa Taifa.

Mhe. Spika, hii ni azma njema kabisa na azima hii kwa kweli kama itasimamia kama ilivyokusidiwa hapa basi hapana shaka kwamba Zanzibar itajikita sana katika maendeleo kwa kuitunza ardhi yake na kuitumia ardhi yake kama ipasavyo.

Mhe. Spika, ardhi ni kitu muhimu sana, Zanzibar ni kisiwa na ni kisiwa ambacho ardhi yake ni ndogo na kama ardhi tutaitumia kiholela bila ya kuizingatia matumizi yake basi siku za mbele watoto watakaofuatia hapo mbele watakuwa ni watu wazima na wao watakuwa na watoto baadae watakuwa watuwazima watakosa maeneo mazuri ya kuishi kwa sababu ardhi itakuwa tumeigema vibaya sana, tumeitumia vibaya sana sisi tulipo hivi sasa.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri suala hili kulisimamia vyema na kamisheni hii itakapoundwa kusimamia ardhi yetu kwa vizuri ili kizazi kitakahockuja kikutie mazingira mazuri ya Zanzibar kwa ajili ya kuhifadhi ardhi yetu vizuri.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 291, Sehemu ya Pili ambayo imeanza ukurasa wa 290, Sehemu ya Pili kuhusu Kamisheni ya Ardhi, lakini nitakalolizungumza hapa lipo katika ukurasa wa 291, kifungu cha 4(1) (d) kinasema hivi:-

"Kusimamia mpango wa Taifa wa matumizi wa ardhi Zanzibar".

Mhe. Spika, Ardhi yetu Zanzibar tunaitumia vibaya, kwa hivyo, kuwepo kwa kifungu hiki kitasimamia vizuri kuitumia ardhi. Ardhi yetu hivi sasa ukizingatia utakutia kwamba hatuna maeneo tuliyoyatenga madhubuti kwa ajili ya kilimo, majenzi na mambo mengine na kadhalika. Sehemu za kilimo zinatumiwa kwa majenzi na viwanja vya michezo.

Kwa hivyo, kamisheni itakaposimamia Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, bila shaka itaweka vizuri matumizi ya ardhi katika kila sehemu inayohuska.

Mhe. Spika, naomba wizara iwe na mipango maalum ya kutoa taaluma kwa wananchi kwani kutoa taaluma ya matumizi ya ardhi ni kitu muhimu sana, vyenginevyo, tutajishtukia kwamba ardhi yetu tunaitumia kiholela na mwisho wake ni kuendeleza migogoro badala ya kuendeleza ufanisi wa matumizi bora ya ardhi.

Hivi sasa kutokana na kutosimamia vizuri ardhi tunaiona miji yetu jinsi ambavyo tunaijenga, kwa kweli tunajenga kiholela hata tukitaka kutengeneza barabara basi tunashindwa kutengezwa barabara kwa ufanisi ila tuvunje majumba ya watu, tunavunja majumba kwa gharama kubwa na barabara zinakuwa finyu, hii ni kutokana na kutokutumia vizuri rasilimali yetu ya ardhi kwa majenzi.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 292 katika Sehemu ya Tatu, Uongozi wa Kamisheni, kifungu cha 2(c), Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Nakusudia kusema kwamba idara hii inaweza ikafanya kazi zake vizuri pale ambapo watafuata taratibu na sheria za nchi ambazo watazisimamia kwa ukamilifu.

Mhe. Spika, katika vijiji kuna watu wana mashamba makubwa ambayo wanayamiliki wenyewe, lakini kwa kukosekana na mipango miji na mipango ya vijiji, watu hawa wanaachiwa nafasi ya kukata viwanja wenyewe viwanja ambavyo wanakata kiholela kama inatokea athari ya kuunga kwa moto katika mji huo basi hata lile gari la zima moto linashindwa kufika kutokana na kupanga miji vyetu vibaya.

Kwa hivyo, hapa nimuulize Mhe. Waziri, ana mpango gani Mhe. Waziri, Idara hii ya Mipango Miji na Vijiji kuiwezesha kutoa taaluma tosha kwa wanaomiliki ardhi katika maeneo ya vijijini kupata uwezekano wa kukata viwanja vya kujenga ambavyo vinakuwa na ufanisi wa kuweza kupitisha magari ambayo yanaweza yakatoa huduma pale inapotokea taathira yoyote au kukata barabara ambazo kwa kiasi fulani watu watapata usumbufu wa kuingia katika miji hiyo.

Kwa kuwa kila mmoja ana ardhi yake anakata kivyake vyake. Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kutoa taaluma tosha na kuwashirikisha watu wa Idara hii na wale walio na maeneo yao binafsi ili vijiji vikaweza kujengwa vizuri na vikaepukana na matatizo ambayo yanaweza yakatokea pale ambapo ardhi itakuwa inajengwa vizuri.

Mhe. Spika, kwa kweli ardhi tutakapoitumia vibaya basi mwisho wa siku tutakuwa sisi ni wenye kulaumiwa na kizazi kitakachokuja. Kwa hivyo, ni juu yetu tuliopo katika madaraka hivi sasa kuitumia ardhi yetu vizuri ili kizazi kitakachokuja kikutie maendeleo ya ardhi yao yanasimamiwa vizuri na yanasimamiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa ufupi sana niseme kwamba mchango wangu huu leo huu utoshe na nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Tunakushukuru. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Wanu Hafidh Ameir, baadae Mhe. Rufai Said Rufai na hatimaye kama muda utakuwepo Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hapa kwa mara nyengine tena leo hii tukijadili Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pili, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache kabisa katika kuuchangia Mswada huu. Kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini pili pongezi zaidi ziende kwa watendaji kwa kazi nzuri wanayoifanya kumsaidia Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla ili kuona kwamba yale mambo ambayo hayaendi sawa, yanakaa sawa na watu wanapata haki zao kama inavyostahiki.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa ambao wametangulia kuzungumza, wamelalamika kuhusu matumizi mabaya ya ardhi, wamelalamika kuhusu migogoro ya ardhi, lakini pia, wamelalamika kuhusu maeneo ya wazi ambayo yanatumika kiholela bila ya utaratibu maalum ambao umepangwa. Lakini Mswada huu tunaamini kwamba mambo haya yote yataenda kuweka sawa na Kamisheni ikianza kazi zake haya malalamiko hayatokuwepo tena.

Mhe. Spika, sasa niingie katika Mswada wenyewe. Kwa kuanzia naomba niunge mkono hoja ya Mhe. Ali pamoja na hoja ya Mhe. Bikame Yussuf Hamad ambao wote wawili wamezungumzia kwamba katika kifungu cha 9, ambacho kinazungumzia Muundo wa Bodi. Kifungu cha 9 (e) ambacho kinampa sifa za Wajumbe ambao Waziri azingatie. Basi na mimi niungane na wenzangu wale kuona kwamba kati ya sifa ambazo Waziri ambazo anatakiwa azingatie jinsi iwe *among* hizo sifa Waziri anatakiwa azingatie.

Mhe. Spika, na nalisema hili kwa sababu ninashangaa sijui kwa nini Wizara inapitikiwa, jana niliwakumbusha kwamba tunakoelekea huko kwenye hamsini kwa hamsini haya mambo hawatakiwi kuyasahau. Na Mswada ambao tumepitisha jana ya Wizara hii hii pia kulikuwa na marekebisho kama hayo kwamba Wajumbe Mswada haukuwa na kifungu kama hicho, lakini Wajumbe wengi walipendekeza kwamba basi pale na Miswada kama hii inapoletwa na katika nafasi kama hizi jinsia lazima izingatiwe.

Mhe. Spika, kidogo ninashangaa kwa sababu ya kumbukumbu kuhusu Mwanasheria wa Wizara hii ya Ardhi ni mwanamke, sasa ninataka nimkumbushie tu kwamba hivi vita dhidi ya *gender balance* lazima ianzie huko chini, ikija huku juu sisi tunamalizia tu. Kwa hivyo, ni vyema wanapotunga hii Miswada yao, basi wao kama wanawake au kama wanawake wengine ambao wanajumuishwa katika kutunga hii Miswada, basi hili suala wawe wanalizingatie huko na sisi huku likija tutakuwa tuna *rubber stamp* tu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ninataka kulichangia ni ukurasa wa 295 ambapo nilikuwa ninataka kuweka mtiririko mzuri tu wa hivi vifungu. Katika Sehemu ya Tano ambapo panazungumziwa masharti ya fedha, kifungu cha 22 (1) kinazungumzia katika Mswada kimeandikwa Kanuni za Bodi, lakini marekebisho ya Kamati yamekuja na marekebisho kwamba kifungu hichi kisomeke; "Fedha za Kamisheni".

Mhe. Spika, mimi nina marekebisho yangu au nina *suggest* yangu tofauti kwamba ninapendekeza kifungu hiki kisomeke kama Akaunti ya Kamisheni, kwa sababu ukiangalia ile *content* ya kwenye kifungu pale inapoanza ina-*introduce* kwamba kutakuwa na akaunti maalum ambazo zitaingizwa fedha. Na baadae ukiangalia vifungu vya mbele ndiyo unaona vifungu ambavyo vinazungumzia kuhusu fedha. Kwa hivyo, nilikuwa nina-*suggest* kwamba *marginal note* ya hiki kifungu kisomeke kama Akaunti ya Kamisheni.

Halafu ukija katika kifungu cha 3 ambacho kwenye Mswada ni kifungu cha 22 (3), nilikuwa ninapendekeza kwamba kifungu hiki kiwe cha 23 na *marginal note* ndiyo "Fedha za Kamisheni". Kwa sababu ukiangalia kifungu cha 22 kama nilivyosema mwanzo kwamba kinaonekana zaidi kina-*introduce* kuwa kutakuwa na Akaunti ya Kamisheni.

Lakini kifungu cha 22 (3) ndiyo kinazungumzia hasa hizo fedha za kamisheni. Kwa hivyo, nilikuwa napendekeza kifungu cha 22 kisomeke; "Akaunti ya Kamisheni", lakini kifungu cha 22 (3) ambacho kilivyo hivi sasa kiwe

marginal note yake iwe fedha za kamisheni na halafu *content* yake kama inavyooneshwa inasomeka kama kawaida fedha na vianzio vya kamisheni vitakuwa hivyo hapo ambavyo vimetajwa.

Lakini *point* yangu nyengine ni kwamba ukiangalia kifungu cha 22 (2) kinazungumzia kamisheni katika kutekeleza majukumu yake na kwa mujibu wa masharti ya fedha zilizopatikana itatumia fedha hizo kwa malipo yote, posho, mishahara, gharama za kazi na malipo mengine yatakayojitokeza ikijumuisha matumizi makuu.

Mhe. Spika, kifungu hiki ambacho kilikuwa ni cha 22 (2), nilikuwa naomba kishuke chini kiwe kifungu cha 23(2), kwa maana ya kwamba itakuwa tumetanguliza fedha zenyewe kwa mtiririko ule ambao nime-*suggest*, itakuwa tumetanguliza fedha zenyewe halafu ndiyo tunaweka masharti na utaratibu wa matumizi ya fedha hizo.

Mhe. Spika, nafikiri nimeeleweka na katika Sehemu ya Sita nilikuwa na marekebisho kidogo kwenye kifungu cha 26 kinasema; "Makosa na Adhabu". Kifungu kinasema;

"Mtu yeyote au chombo na bila ya sababu".

Mhe. Spika, hiki chombo nilikuwa napendekeza kwamba iwe taasisi ama idara, kwa sababu ukisema chombo haraka haraka inakujia kama chombo sijui vespa, baiskeli, *boat*, gari. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kwamba baada ya chombo kisomeke kwamba; "Mtu yeyote au taasisi ama idara bila ya msingi kimezuiwa au kimeekwa..." na kama inavyoendelea.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Mswada huu na naomba Mhe. Waziri atakapokuja anitolee maelekezo yale ambayo nimeyagusia.

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunakushukuru. Naomba nimkaribishe Mhe. Rufai Said Rufai, akifuatiwa baadae Mhe. Mgeni Hassan Juma, muda ukiruhusu tumsikilize Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu kupata nafasi hii ya kutoa mawazo yangu katika Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Yanayohusiana na Hayo, ili tuweze kukiweka chombo hichi kuweza kuitumia vizuri ardhi ndogo tuliyonayo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Zanzibar ni watu tunaoishi katika visiwa na miongoni mwa visiwa vidogo ni visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kama ardhi yetu ni ya visiwa basi bila shaka kwamba ardhi hiyo ni ndogo na inahitaji matunzo ya hali ya juu. Wote ni mashahidi tumeona wimbi la watu wanavyovamia maeneo ya ardhi mbali mbali Unguja na Pemba na wote ni mashahidi tunavyoona maji ya bahari yanavyovamia katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kama hatukuweka sheria za ufuatiliaji wa hali ya juu, uvamizi huu wa binadamu utaendelea na kuathiri na kukipa hasara kizazi kinachokuja kukosa maeneo ya maishi na kuendeleza shughuli zao nyengine za kuwaletea maisha.

Mhe. Spika, nitoe pongezi zangu rasmi kwa Mhe. Waziri pamoja na Wizara yake kuliona hili kwamba ni jambo linalohitaji kuekewa kudhibiti ili tuweze kukitunza kile kidogo tulichonacho, ili kilete maslahi kwa wananchi na kazazi kinachokuja baadae.

Mhe. Spika, katika sheria hii mimi nitaanza mchango wangu katika sehemu hii ya pili inayozungumzia Kamisheni ya Ardhi. Katika kamisheni kwenye kifungu cha 4 kumeekwa "Kazi za Kamisheni". Kazi hizi siyo kidogo, imeanza (a) hadi (q). Lakini kupitia kuziona hizi kazi za kamisheni ni nyingi tena nzuri. Lakini pia, nilikuwa nimshauri Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kazi hizi zilizoekwa hapa, ninahisi kwamba kuna jambo moja ni muhimu kuwepo katika kazi za kamisheni.

Mhe. Spika, kazi yenyewe ni utoaji wa elimu kwa wananchi wetu. Nimejaribu kuangalia sana suala la elimu hapa sikuliona na kitu taaluma ni jambo linalosaidia kazi kwa taasisi yoyote kwa shughuli yoyote pale wananchi wake

wanapopata elimu ile. Tatizo la mambo ni kukileta kitu kikakosa kueleweka, tuweke sheria sijui ngapi, lakini wananchi wanapokosa taaluma, basi sheria hiyo itakuwa haithamini wala haitokuwa na nguvu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo, ningelimshauri sana Mhe. Waziri tuongeze kifungu cha elimu katika kazi hizi za kamisheni. Katika kamisheni itakuwa na kazi zifuatazo, mimi nianze na suala la (e) pale inasema kwamba;

"Kuwainisha viwango na utaratibu wa usimamizi wa ardhi".

Mhe. Spika, hii kazi moja nzuri kwa sababu kama ardhi yetu hatukuweka katika viwango, basi tutakuwa hatujafanya jambo la msingi. Ardhi inazidiana maeneo kwa maeneo. Kwa hivyo, kuna maeneo ya kilimo. Kama tutaanza kama wananchi hivi sasa walivyo kwamba maeneo ya kilimo ndiyo yanavamiwa kwa kujengwa majumba, watu wanasahau kwamba kila mtu anahitaji kuishi, wengine ni wafanyakazi na wengine ni wakulima. Mkulima anapolima anakuja kumuuzia mfanyakazi, pesa pale inazunguka na kila mmoja anapata maslahi yake.

Lakini kama hatukuweka hivi viwango kwamba ardhi ya eneo fulani, hili ni *special* kwa wakulima. Ardhi ya eneo fulani ni *special* kwa wafugaji basi itakuwa tayari tushaweka mambo ambayo yataleta ufanisi katika kuiheshimu na kuitunza hii ardhi ndogo ambayo tunayo. Kwa hivyo, hili ni jambo muhimu na la kulitunza na kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, inawezekana kwa utaratibu tulionao huko nyuma, mtu anaweza kuuziwa ardhi ambayo haina kiwango, lakini akauziwa kwa bei kubwa. Lakini ile ardhi ambayo ina kiwango mtu akapewa kwa bei ndogo. Kwa hivyo, hapa tutakuwa hatukuwatendea haki wananchi wetu katika kutumia faida na raslimali aliyotupa Mwenyezi Mungu hivi visiwa vyetu. Kwa hivyo, kuweka mambo fulani vitaweza kuwasaidia wananchi wetu na wale wananchi wengine wanaokuja kuekeza katika ardhi hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hili niseme kwamba ni jambo la busara na linahitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kazi hizi ukija (f), pale kuna kupendekeza kinasema;

"Hatua za kuhakikisha kwamba Sera ya Serikali zinajumuisha maendeleo ya ardhi katika kusimamia matumizi sahihi ya ardhi".

Mhe. Spika, duniani kote watu wanapoanzisha mambo yao, kitu cha kwanza kinachoangaliwa ni sera. Jambo lolote lile kama halikuwekewa sera basi hatma yake litaleta migogoro na migogoro haileti tija. Hatma yake inakuwa mwenye nguvu mpishe, mnyonge mnyongeni. Kwa hivyo, kitu sera ni kitu muhimu sana na kama sera tulizonazo haziendi na wakati tulionao, ni vyema Mhe. Waziri na Wizara yake wakazipitia sera zote za ardhi na kuweka marekebisho ili kuifanya ardhi yetu ya Zanzibar iwe inakwenda na wakati huu wa leo tulionao. Kulikoni tukawa tunaandaa sheria, lakini sheria hii haiendi sambamba na Sera za Serikali zilizopo.

Mhe. Spika, itakuwa hapa hatujafanya jambo la msingi la kuinusuru hii ardhi.

Mhe. Spika, katika matumizi ya ardhi ni jambo ambalo tumeliona wote, ndiyo karibuni tu hapa pakawekwa kwa sababu bado Zanzibar tunahitaji maendeleo ya haraka, tumo katika kutengeneza mabarabara, viwanja vya ndege na mambo mengine. Katika kutengeneza mambo haya ni lazima *materials* yake yatoke kwenye ardhi. Kwa hivyo, tunahitaji mawe, udongo na mchanga. Sasa katika kuhamisha mambo haya, mule tunamochukua yale *materials* tunabakisha mashimo, au mabwawa, hatuna mpango wa kurejesha maeneo yale tukarudisha udongo mwengine ili kuifanya ardhi ile iweze kutumika kwa mambo mengine kama ya kilimo na shughuli nyengine zozote zile. Sasa hapo itakuwa bado matumizi haya ya ardhi tunatumia vibaya kwa kutoijali ardhi yetu na kufanya marekebisho pale ambapo tumetumia. Sasa kama Kamisheni inapewa majukumu mazito na ni majukumu yanayohitaji kipaumbele kusaidiwa kamisheni, ili kuhakikisha hii ardhi tuliyonayo tunaifanyia matumizi sahihi na tunaijali ardhi yetu ndogo tuliyonayo

Kwa hivyo, mimi mara nyingi nasema Mhe. Spika, sheria ya haya maandishi, sheria inahitaji usimamizi na kitu chochote kinachokosa usimamizi, basi mambo yale yatabakia karatasini lakini hakuna kinachoendelea. Kwa hivyo, suala la usimamizi ni suala la kupewa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda kama vile tulivyoipangia, lakini unapokosa usimamizi hatujui tumlaumu nani na hili ni tatizo kubwa hapa Zanzibar la kutokuwa na usimamizi.

Mhe. Spika, kwa mfano, Baraza liliwahi kutunga sheria ya kuwataka wenye vyombo vya moto kuvaa ma-*helmet*. Sheria hii siku mbili au tatu ikafanyiwa kazi, lakini sasa hivi haifanyi tena kazi imetulia kwa kukosa usimamizi. Sio hiyo tu, ni sheria mbali mbali. Kwa hivyo, tunapokosa kusimamia sheria zetu, basi uharibifu wa ardhi na mambo mengine utakuwa upo wa hali ya juu na ardhi hii ndogo itabidi kizazi kinachokuja, waje waone kwamba wenzetu waliopita ardhi waliitumia vibaya na hatima yake wao wamekosa maeneo ya kuishi.

Mhe. Spika, ujengaji wa nyumba kiholela ovyo ovyo. Tunashuhudia katika maeneo yetu mbali mbali, watu wanajichukulia ardhi wanazotaka wao hakuna kipimo, wanajenga wanavyotaka wao na hatima yake maeneo mengi ya kuzalisha sasa hivi yanakuwa ni maeneo ya wanaoishi watu. Kwa hivyo, kama hatukulisimamia hili, bila ya shaka ardhi hii ndogo na chache itaathirika na hatima yake tukose maeneo ya kuishi.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha (h) kinachosema kwamba kusimamia masuala yote ya ukaguzi na upimaji Zanzibar. Mhe. Spika, nilipokisoma kifungu hiki ndipo nilipopata wazo kwamba kitu elimu kinahitaji sana kuwepo katika kazi hizi za ndugu zetu hawa wa Kamisheni.

Idara ya Upimaji ilifanya kazi kubwa ya kupima maeneo mbali mbali kwa Pemba na Unguja, lakini kukosekana kwa taaluma baadhi ya maeneo baada ya kwisha kupimwa wananchi wa maeneo hayo walivamia na kuondosha vikuta vile na mambo mengine yote ya upimaji. Kwa hivyo wamerudisha nyuma maendeleo ya ardhi katika maeneo hayo. Kikubwa ninachoona ni kwamba kulikosekana taaluma. Kwa hivyo, katika kusimamia huku masuala ya ukaguzi, Kamisheni ni kazi moja kubwa na hii Kamisheni kama itakuwa legelege, basi haitafikia kuweza kusimamia shughuli zake.

Katika mapendekezo ya kupatikana hawa watu wa Kamisheni, ningeshauri sana Kamisheni iwe na watu ambao ni vijana. Kijana ana uwezo wa kutumia nguvu zake, kutumia vyombo vyengine atakavyokabidhiwa, kulikoni kuja kuunda Kamisheni ambayo kazi yake ni kukaa ofisini. Kazi hii ni kubwa, ni ngumu na ni nzito. Kwa hivyo, asilimia kubwa ya Kamisheni iwe ni vijana ambao damu yao bado ni mbichi wanaweza kusimamia masuala mazima ya ardhi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, kuna kifungu hiki cha kazi za Kamisheni (k) kinazungumzia kwamba kuzipitia sheria za ardhi zilizopo na kupendekeza marekebisho.

Mhe. Spika, hiyo ni kazi nyengine kubwa, tuna sheria nyingi za ardhi, lakini sheria hizo nyengine zimeshapitwa na wakati, hazikidhi haya ya leo kabisa na ni sheria hizi kama Kamisheni itaifanyia kazi, basi ni vyema Mhe. Waziri suala hili alipe kipaumbele ili sheria ambazo haziendi na wakati wa leo, basi zichukuliwe hatua na zifutwe na ziweze kuletwa hapa Barazani na kufanyiwa marekebisho ili tuweze kwenda na hali halisi ya dunia ya leo.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kifungu hiki cha 4(2) sheria inasema kwamba wakati waziri anateua wajumbe waliotajwa katika aya (e) atalazimika kuzingatia sifa zifuatazo.

Mheshimiwa niipongeze sana wizara kuliona hili na kumpunguzia waziri wetu majungu na kuonekana kwamba waziri amefanya upendeleo, wamechagua watu wa familia yake amewapa nafasi hizi. Kwa hivyo, kuwekewa sifa hizi kwamba hao atakaowateua waziri basi kwanza azingatie uzanzibari wao, jambo la muhimu sana. Kwa sababu ni Wazanzibari walio na haki kubwa kabisa kufanya kazi hizi ni Mzanzibari mwenyewe, pale ambapo Zanzibar hatuna mtaalamu au mtu huyo basi tunaweza tukatafuta kwa wenzetu.

Kwa hivyo, kuwa Mzanzibari hapa nashukuru na napongeza sana kwamba wamefanya suala zuri, lakini sio Mzanzibari tu, huyo atakayemteuwa Mhe. Waziri awe na utaalamu na uzoefu angalau wa miaka saba katika fani ya ardhi, uwekezaji, mazingira, utawala uchumi au sheria.

Mhe. Spika, ni jambo la maana sana, nadhani vidomo domo vya watu hapa vitakatika, kwamba waziri hakuchagua ndugu yake, waziri amefuata utaratibu wa sheria, lakini niungane na wale wenzangu waliosema kutafuta mtu ambaye keshakuwa na uzoefu wa miaka saba ndio ateuliwe, na Zanzibar kila siku tunasomesha ndugu zetu na hawa nao wanahitaji kuajiriwa nchi hii hii. Sasa kuweka sheria muda wote huo ni kuwafanya vijana wakose ajira serikalini.

Mimi nasema miaka saba ni mingi, kwa uchache Mhe. Spika, angalau basi wasipunguwe miaka mitano, angalau, lakini kuweka miaka hii ni kumfanya kijana asubiri hata akija kuipata hiyo kazi pengine keshazeeka, muda wa kufanya kazi serikalini hamruhusu tena kwa kuweka sheria kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, hili tutakuwa hatuwatendei haki vijana wetu ambao wana jitihada ya kuiendesha nchi yao. Kwa hivyo, kujiwekea masheria kwa muda mrefu kuwalazimisha waliopo wasiondoke, hili tutakuwa hatuwatendei haki vijana wetu. Mhe. Spika, niseme kwamba katika sifa hizi alizopewa Mhe. Waziri nazipongeza sana kwamba atafanya kwa mujibu wa sheria inavyomuelekeza.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 10 kuna muda wa bodi hapa. Sasa hapa nije katika kifungu (d) ambacho kinasema kwamba;

(d) "Kuteua Wakuu wa Vitengo kwa mujibu wa masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma".

Hapa ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anipe haya masharti kidogo, inawezekana kibinadamu nimeyasahau, ili niweze kuyajua haya masharti ya kuwapata hawa Wakuu wa Vitengo vya Bodi, nadhani kuna wajumbe wenzangu pia tatizo hili wanalo katika kuperuzi hii sheria limewakwaza na wao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja nipate maelezo ya kina katika suala hili.

Mhe. Spika, nikiendelea nikiwa niko karibu na kumaliza hoja yangu hii, nije katika kifungu cha 17 cha sheria hii, kinachosema kwamba muhuri wa bodi. Kinasema kwamba muhuri wa bodi utathibitishwa kwa kuweka saini ya Mwenyekiti, Katibu au maafisa wowote wa bodi, kama bodi itakavyowateua kutekeleza jukumu hilo kwa niaba yake. Naomba niseme kwamba hii sheria ni nzuri sana, inaondosha ukiritimba, inaondosha kumuweka mungu mtu, kumuweka mtu mmoja tu kwamba kila jambo ndio yeye tu, kama hayupo bwana fulani basi hapana litakalokuwa.

Mhe. Spika, tumeona jitihada za Mhe. Waziri asubuhi alipotueleza hapa katika swali lililoulizwa, jinsi anavyowaita watu na kuwatilia saini maombi yao, lakini na kama hapa hii sheria ilimbana kwamba Mwenyekiti tu atie saini. Kwa kweli tungekuwa hatukuwatendea haki wananchi wetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa utaratibu huu nadhani Mheshimiwa lawama, manung'uniko na fitna zitaondoka kwa sababu watendaji wa kuwashughulikia wananchi watakuwa wapo na wanakifu kuondosha matatizo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana pamoja na Baraza lako kwa kunivumilia, nashukuru kwa hilo. Kwa hivyo, nasema naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana, naomba nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma, kama muda utakuwepo tumsikilize Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia machache katika mswada ambao umeletwa na Mhe. Waziri wa kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma ambaye katujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu zilizotuleta hapa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana waziri pamoja na watendaji wake wote ambao wameshiriki katika kuuleta mswada huu hapa Barazani, kwa ajili ya kuweza kupitisha sheria hii ambayo ilikuwa kukosekana kwake kumesababisha kasoro nyingi sana ndani ya utendaji unaohusiana na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, mimi nitaungana na wenzangu wote ambao wamechangia kusema kwamba wakati kwa kweli umefika wa kuweza sasa kuwa na Kamisheni ambayo itaweza kupanga matumizi bora ya ardhi yetu.
Mhe. Spika, nikisema hivyo nina maana kwamba ardhi ya Zanzibar tunafahamu sote ya kwamba ni ndogo, lakini vile vile ukuaji wa idadi ya watu ambao wanaishi Zanzibar unaongezeka kila siku na tunajua kwamba ardhi ndio rasilimali kubwa ya nchi yetu. Kwa hivyo, matumizi bora ya ardhi kwa kweli yanahitajika sana ili kuweza kutumia ardhi vilivyo, lakini vile vile ardhi hii iweze kutumika kwa sasa na kwa kizazi kinachokuja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili linatufanya tuone kuwa Kamisheni ina umuhimu mkubwa, kwa sababu ndio itakuwa msimamizi mkubwa, lakini itaweza kutuwekea mipango mizuri, itaweza kutuandalia mikakati itakayoweza

kuendeleza ardhi yetu kwa matumizi mazuri, lakini itaweza vile vile kuajiri wataalamu ambao watakuwa na uwezo wa kupanga mipango hiyo, lakini itaweza kudhibiti matumizi ya ardhi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba mengi yamezungumzwa na wenzangu, kuna mengine ambayo nakubaliana nayo na kuna mengine ambayo siyaungi mkono na nina sababu zangu, lakini nitaanza katika ukurasa wa 292, na ninakwenda moja kwa moja katika suala zima la Bodi ya Kamisheni.

Mhe. Spika, bodi kama tunavyojua tunaweza kusema ndio *centre* ya usimamizi mkuu wa Kamisheni. Mhe. Spika, hapa nimeona kwamba tunaanzishiwa bodi ndani ya Kamisheni hii, ambapo bodi hiyo itakuwa na kazi maalum kwa ajili ya usimamizi wa hiyo Kamisheni yenyewe.

Mhe. Spika, moja katika sifa ambayo imeelezwa kwamba itakuwa ni sifa za wajumbe wa bodi akiwemo pamoja na Mwenyekiti wake, kwamba inasema katika kifungu cha 2, wakati waziri atateua wajumbe waliotajwa katika aya hii, atalazimika kuzingatia sifa zifuatazo. Pamoja na sifa zote zilizokuwemo, kuna sifa (b) inayohusiana na elimu ya wajumbe hao wa bodi.

Mhe. Spika, kumekuwa na uzoefu wa kuwa tumezoea kwamba awe na Shahada ya Kwanza. Mhe. Spika, kwa mawazo yangu mimi, naona sasa hivi umeshafika wakati wa kuondokana na Shahada ya Kwanza, na kwa sababu Mhe. Spika, tunao wataalamu wengi hapa Zanzibar ambao wana ujuzi na sifa kama hizi ambazo tunazizungumza wapo katika Shahada ya Pili.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba bodi zinahitaji watu wenye taaluma kubwa, na Shahada ya Kwanza Mhe. Spika, bado sasa hivi imeshakuwa ni kigezo kidogo cha kushika nafasi kama hii.

Mhe. Spika, mimi kwa bahati nzuri umeniteua kuingia katika bodi kadhaa na nimeona kwa wenzetu wale wanaoingia ndani ya bodi zile wana utaalamu gani, wana weledi gani na wana uzoefu gani, na hili ni muhimu sana sasa hivi tuanze kulifikiria, Shahada ya Kwanza ni kigezo kidogo kuwa kama Mwenyekiti au Mjumbe wa Bodi, tunao wataalamu. Tunashukuru kwamba, lakini kuna watu ambao wazoefu na wengine ni wastaafu ambao wamepata elimu ya kutosha ya kuweza kuwa wajumbe ndani ya bodi hizi.

Mhe. Spika, vile vile niungane na wenzangu waliozungumzia suala la *gender*. Mhe. Spika, *gender* ni muhimu sana kulizingatia, na mimi naamini vile vile kwamba pamoja na sifa hizo za elimu, wako akina mama ambao wana sifa hiyo hiyo ya kuwa na Shahada ya Pili, lakini vile vile wana uwezo mzuri na weledi wa kuingia ndani ya bodi hiyo.

Mhe. Spika, mwanamke ndiye mtumizi mkubwa wa ardhi, mwanamke ndiye anayejishirikisha sana na masuala ya kilimo, lakini mwanamke huyo huyo ndiye anayetunza nyumba. Majumba yetu mengi ambayo yamejengwa yanatunzwa na akina mama, kuna kila aina ya sababu kusema kwamba katika bodi hii ya Wajumbe basi tupate nusu kwa nusu Wajumbe wanaume na Wajumbe wanawake ili na wao waweze kutoa mchango wao katika kujenga Taifa lao.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba katika kazi za bodi katika kifungu cha 11(f) kinazungumzia suala la kuidhinisha bajeti ya Kamisheni ikijumuisha vyanzo vya fedha na matumizi, hapa ningeomba sana pafanyiwe marekebisho kidogo na isomeke kama ifuatavyo.

Ni kuidhinisha bajeti ya Kamisheni na kupokea ripoti za matumizi na vyanzo vya fedha, kwa maana kwamba bodi sio kazi yake tu kupanga au kuidhinisha bajeti lakini na kazi yake vile vile kuangalia matumizi ya fedha yaliyotumika ndani ya Kamisheni. Kwa hivyo hivi ilivyokaa kidogo inaleta utata.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka niliseme ni suala zima la mafunzo ingawa katika utaratibu wetu wa kuandika mambo mbali mbali ambayo yanatakiwa bodi iyafanye inaonesha dhahiri kwamba bodi itakuwa ina kazi kubwa, na niliposema kwamba panatakiwa sifa zaidi ya shahada moja, lakini vile vile kunatakiwa kuwe na mafunzo endelevu ndani ya bodi zile.

Mhe. Spika, bodi hizi zina majukumu ya kuangalia manunuzi, matumizi ya Kamisheni ikiwa bodi hizi zitakuwa hazina uwezo huo wa kujua masuala mazima ya namna matumizi yanavyoendeshwa ndani ya kamisheni bodi hizi zinaweza kupitisha mambo ambayo yatakuwa hayafai, lakini wanatakiwa wawe na uwezo wa kujua penye harufu ya

rushwa na haya hayapatikani kama Wajumbe wa bodi hii watakuwa hawana uwezo wa kuyaona hayo. Mhe. Spika, ningekuomba kitengwe kifungu maalum katika bodi hizi pamoja na watendaji wako ili kujua pale ambapo patakuwa na jambo lolote linaloonesha kwamba kutakuwa na kasoro ndani ya utendaji wa kamisheni bodi wawe na uwezo wa kuliona.

Mhe. Spika, kutokana na hayo hayo ambayo nimejifunza katika bodi za wenzetu nimeona namna wenzetu wanavyopata mafunzo mbali mbali ya kuweza kusimamia taasisi zao, na hilo ni muhimu sana ambalo kwa huku kwetu linakuwa gumu kutendeka, lakini hilo linafanyika ikiwa taasisi yenyewe itakuwa ina fedha za kutosha za kwenda kutafuta mafunzo kwa ajili ya watumishi wao pamoja na Wajumbe wa bodi.

Mhe. Spika, makosa ambayo tumeyafanya nyuma hatutaki kuyarejea na ndio maana leo hii tunaleta hii sheria, makosa hayo yameathiri na athari yake itaendelea kuonekana lakini kubwa linalokuja sio lililopita. Ningeomba sana hili ambalo ninalizungumza hapa suala zima la kuwezesha Wajumbe wa bodi pamoja na watendaji ni suala muhimu Mhe. Spika, nakuomba sana kuwepo na kifungu maalum cha kuweza kuona kwamba Wajumbe hawa wanapewa uwezo wa kuendesha bodi hiyo.

Mhe. Spika, ardhi ndio rasilimali ya Taifa hili kwa kizazi kinachokuja, upangaji wake, matumizi yake pamoja na mengine yote ambayo yataleta manufaa kwetu sisi na kizazi kijacho inategemea sana na mipango ambayo tunaipanga leo. Mhe. Spika, nakuomba kwamba Kamisheni hii iondoe yale matatizo yote au iweze kukidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar kwenye masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ndogo ya kuweza kuchangia lakini niipongeze sana kwa sababu mengi sikuweza kuyazungumza humu, kwa sababu mswada huu na Sheria hii kwa kweli inakidhi haja isipokuwa ni masuala madogo madogo ambayo naamini kwamba Waziri anaweza kuyafanyia kazi, lakini Mhe. Spika, ningekuomba tena kama walivyokuomba wenzangu kwamba utekelezaji wa sheria hii ndio unao umuhimu mkubwa kuliko haya maandiko tuliyonayo katika meza zetu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nitajitahidi sana hizi dakika kumi na tano ziweze kukidhi haja. Mhe. Spika, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea kuwa hai mpaka hivi sasa, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru wewe Mhe. Spika, angalau na mimi kunipatia hizi dakika kumi na tano nikaweza kutia tia nyalio kidogo katika hii hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na timu yake pale kwa kuweza kutuletea kitu hichi. Huu mswada huu umechelewa sana Mhehimiwa, ulikuwa uje zamani sana, kwa kweli katika hili nalazimika kumpongeza kwa sababu Mawaziri wengi wameshapita kabla ya yeye na hawajawahi kutuletea kitu kama hichi, basi kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wapiga kura wa Jimbo la Wawi kule tunachukua fursa hii kumpongeza Waziri pamoja na benchi lake la ufundi pale kwa kuweza kuleta mkombozi. Maana huu mswada huu mimi nachukulia kama mkombozi wetu sisi wakulima wadogo wadogo kule maweni.

Mhe. Spika, kimsingi mimi nimeangalia vitabu pale *freedom and unity by Julius Nyerere*, nimeangalia vitabu vile vingi vingi huku nyuma ujamaa na kujitegemea, vile vile kwa mujibu wa Mwalimu Nyerere, kuna sehemu Mwalimu kaelezea wazi kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne katika mambo hayo ikiwamo ardhi. Sasa katika miaka hii ya kuanzia pale 1964 baada ya Mapinduzi mpaka kufikia mwaka 1977 hapa tulikuwa tunakwenda vizuri sana, kwa sababu sisi wakwezi na wakulima wa nchi hii tulikuwa tukitumia ardhi vizuri mno chini ya uongozi wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyokuwa ikiongozwa awali na Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na baadaye Mzee Aboud Jumbe 1977. Tuliweza kuitumia vizuri sana ardhi na Chama cha Afro Shirazi chini ya Katibu wake Mkuu mahiri sana marehemu Mzee Thabit Kombo Jecha Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi na yeye vile vile.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi katika miaka ya 1970 pale wakati nipo Sekondari skuli pale *Fidel Castro Secondary School form one to six* nilikuwa pale baba yangu alikuwa Mzee Nassor bin Juma alikuwa hafanyi kazi ya Serikali, kazi yake kubwa ilikuwa ni kulima katika ardhi ya maweni pamoja na kuchimba chimba mawe kule Makaani na

hatimaye kupata ada ya kuweza kunisomesha mimi mtoto wake ambaye sasa ni Mwakilishi makini na mahiri katika Jimbo langu la Wawi. Aliitumia ardhi kwa sababu Afro Shirazi ilikuwa na Mipango mizuri sana ya kusimamia ardhi Mheshimiwa, ninasikitishwa sasa ile ardhi ambayo Mzee Nassor bin Juma aliyekuwa akitumia ardhi ile kule kunisomesha mimi, sasa ardhi ile inakatiwa watu mapande wengine wana viwanja vitano, wengine sita, wengine saba mtu mmoja huyo. Mzee Nassor hajiwezi tena lakini hata wazee wengine hawawezi tena kukaribia ardhi ile kwa shughuli za kilimo kwa shughuli za kuchimba mawe, alimradi tunakuwa *slaves of fear within our country*.

Sasa naamini kwamba na huu utumwa wa hofu; kwamba ardhi sisi tulipindua mwaka 1964 hapa kupata uhuru wa nchi hii na kutumia rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na ardhi, leo Mheshimiwa uhuru wa kutumia ardhi, mipango ya kutumia ardhi katika nchi hii haipo inasikitisha sana sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nimo katika ile kamati yako ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Ofisi za Viongozi wakuu wa Kitaifa, nikiwa Makamo Mwenyekiti wa kamati ile tumetembelea kule maeneo ya Nyanjale, tumetembea maeneo ya Kaskazini wanaanika madagaa jamaa kule, kila pahala wanasumbuliwa kila pahala waanikaji madagaa ndani ya ardhi yao wanasumbuliwa badala yake wanaachiliwa Wataliano wawekeze, mambo kama yale sisi wana Mapinduzi inatusikitisha kwa sababu sio dhamira ya Mapinduzi kuleta Mtaliana na kumuacha mkwezi na mkulima.

Sasa mimi naamini Mswada huu Mheshimiwa nimeangalia na baada ya kuangalia hapa katika sehemu ya pili ya Mswada huu kazi za Kamisheni, nimetupa macho Mheshimiwa katika kifungu namba tatu hapa anasema kifungu namba tatu kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu naomba uniruhusu kidogo ninukuu Mheshimiwa Spika.

Kifungu kinasema "*Kazi za Kamisheni itakuwa na kazi zifuatazo;* kaeleza kadhaa lakini mimi nakuja hapa katika kifungu cha pili (J) anasema: *Kutekeleza kukuza program za elimu zinazohusu matumizi na usimamizi wa ardhi"* Nakatisha hapo katika kunukuu kwangu Mheshimiwa.

Mhe. Spika, mimi zamani kabisa wakati nasomesha skuli nilikuwa nasomesha skuli moja kule Mwanza baada ya kuacha chuo wanaita *Bwiru cares* hata Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza hili hiyo shule aliwahi kusoma, na mimi bado kidogo nimsomeshe pale *Bwiru Cares* Bi Mgeni pale. Sasa ilikuwa nikitoka *weekend* mimi nilikuwa nachukuliwa na wahindi matajiri zangu wananileta pale Dar es Salaam nakwenda fukweni fukweni mule kwa Wakojani jamaa zangu wa Kipemba napata pata samaki wananikaushia samaki.

Baada ya siku narudi zangu Mwanza kwenda kusomesha na kukamata chaki kule ardhi ile yote sasa inapewa watu hawathubutu kuivunja Wakojani kwa kuweka Dago. Ardhi yote ile tulikuwa tukienda kwenye kisiwa kile wanaweka pale Wakojani hawathubutu kufika tena, kile kisiwa kidogo kiliopo kabla ya Unguja hiki kutoka Pemba kile unakiona pale.

Mhe. Spika, almuradi ardhi wanapewa wageni wananufaika sasa sisi tumepindua kwa ajili gani hapa, nadhani tulipindua kwa ajili hiyo. Mimi Mhe. Waziri nakupongeza sana na naomba huu Mswada tuupitisheni na Rais tumuombe ukifika tu ausaini, tutakuja kuwa kama *Hong Kong* hapa sisi, kule Hong Kong wana ardhi imekuwa *very limited,* wanaishi katika *stationary booth along the coast* wanaita shampu. Mtu anatoka kwenye ardhi anakuja zake kulala kwenye boti isifike huko lazima ardhi ya kilimo ijulikane ni hii, ardhi ya mambo ya watalii tuwape angalau kidogo tu sisi tupewe nyingi wakaazi wa hapa ili tuweze ku- *earn a living,* mimi na wenzangu wakati naanzisha Chama cha Wananchi CUF pale *Star light* mwaka 1990 tulikuwa tunaandaa katika kuimarisha hiki chama.

Mimi na wenzangu bwana Ali Haji Pandu, akina Mloo tulikuwa tunakaa pale tunaangalia jinsi wakati tunatayarisha ule utajirisho, *investment,* tukaangalia sisi vya kumuwezesha moja katika jambo ambalo utajirisho ufanywe ni kumuwezesha Mzanzibari kuweza ku- *earn a living* kwa yale mazingira yanayomzunguruka ikiwemo hiyo ardhi, huo ndio utajirisho kama mlikuwa mna tatizo kubwa na utajirisho, kumfanya Mzanzibari aweze kuishi kwa mujibu wa yale mazingira yanayomzunguka ikiwemo ardhi, bahati, hewa aweze kuishi vizuri huo ndio utajirisho.

Tukaona ardhi haitumiki vizuri na Serikali ilikuwa imeshaanza kushindwa 1992 mimi na wenzangu tukaanzisha hichi chama chama cha Wananchi CUf. Wale wenzangu ilikuwa kina aliyekuwa Jaji Mkuu hapa Mzee Ali Haji Pandu, Marehemu Mloo na tukasema tukitoka hapa tuanzishe hichi chama basi tutaweza kuingiza utajirisho tunaweza kuleta matumizi mazuri ya ardhi.

Lakini baada ya kuanzisha tu Chama yakaja yale mambo ya utalii ardhi yote ikavamiwa, sasa Mheshimiwa mimi naamini kwamba sheria hii Kamisheni hii ya Ardhi basi itatusaidia sana kutupatia ukombozi na kuweza kutupatia maisha kutokana na hii ardhi pamoja na matumizi mazuri ya ardhi, *population density* ya Wazanzibar inaongezeka sana, hivi sasa tuko 1.3 kesho kutwa tutakuwa *two* milion kijipande hichi hichi lazima ardhi tuitumie vizuri.

Mheshimiwa mimi wakati nasoma *Vitongoji Primary School* kila mwisho wa mwezi tulikuwa tunapelekwa *pick nick* katika *beach huku along the beach* tunaogolea tunakuja juu, tunaangalia kwenye ufukwe sasa hakuna nafasi tena kuwapeleka wanafunzi wetu, *beach* zote zimepanua na uwekezaji yale si matumizi mazuri ya ardhi, lazima na wazalendo wawe na nafasi ya kufanya shughuli zao katika *coastal areas*. Kesho kuna mashindano ya Kombe la Dunia ya *Beach soccer* hii mipira ya ufukweni hii, sasa sisi Zanzibar tuna fukwe nzuri sana kabisa kabisa lakini inasikitisha kwamba hakuna timu ya mpira ya ufukweni kwa sababu ardhi hatuzitumii vizuri. Leo tunashindwa na Tanganyika kesho wanashiriki kombe la Dunia timu za ufukweni sisi hatushiriki kwa nini kabisa kabisa Mheshimiwa!

Mimi nadhani katika hili Mhe.Waziri ujitahidi sana kwanza tupitishe huu Mswada tukishaupitisha Mswada Mhe. Waziri uanzishe hili *file board commission* ili iwekwe katika kujali ardhi, ardhi ya viwanda ijulikane, ardhi ya ndugu zetu waliopo pale Maruhubi pale sasa hivi pale wamewekeza Wazanzibari zaidi ya elfu tatu wamepata ajira pale Maruhubi, ya kuanika madagaa tu wao. Na pale Maruhubi panataka kujengwa bandari karibuni hivi. Leo wale hawana pa kwenda sasa hivi sasa siku zote Waziri hamjawapatia sehemu za kwenda kuanika madagaa yao, munawaondosha pale eti munataka kuwaleta sehemu ambayo haina ufukwe kwa sababu wale lazima wapate pembezoni mwa bahari ndio shughuli zao zilivyo.

Mhe. Spika, mimi nadhani matumizi ya ardhi ni muhimu na muwajali watu wa pale Maruhubi muwapatie nafasi nzuri, wale ndio walipa kodi wa nchi hii, wale wanalipa kodi ndio hizo tunazolipwa sisi mishahara, kodi wanazolipa wale almradi kila jambo wale. Sasa leo tunawadharau sisi tumetembelea Kamati muda mwingi na tumeshaishauri serikali pale iwapatie mahala pazuri wale waweze kuanika madagaa. Hali kadhalika kule Nyanjale mumempa jamaa eti anakwenda kuanzisha mpira wa gofu wakati wakwezi na wakulima wana ajira zao pale, nyinyi munampa anaanzisha gofu yule si kuwadhalilisha Wazanzibari? Mimi naamini Mzee Karume angekuwa hai na Thabit Kombo hapa pasingekalika kwa mambo kama yale kwa jinsi walivyokuwa na imani na watu wao wale.

Sasa mimi nadhani tu Mheshimiwa sikusudii labda kusema Serikali haina imani, Serikali ina imani kwa sababu imeleta huu Mswada, Mswada tuupitisheni wale wazee wa Janjani wapewe ardhi, Maruhubi wapewe ardhi waanike madagaa, na sisi Makaani tujue kwamba tunachimba mawe na kupanda tungule kule Makaani, watu wa Vitongoji, watu wa Wawi ili maslahi ya nchi yapatikane na ardhi sio muikite katika mambo ya utalii pekee.

Kwa sababu ya muda Mheshimiwa na mimi huwa sipendi sana ninaposimama ukanambia muda umenimalizikia, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu naunga mkono huu Mswada, na nashauri nyinyi Waheshimiwa huu Mswada muupitishe kusudi Mhe. Rais ausaini na baadaye utukombolee ardhi. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Saleh tunakushukuru kwa mchango huu na mchango wako unatufikia kumaliza muda wa leo kipindi cha mchana huu. Nawashukuru Wajumbe wote na sasa niahirishe kikao hichi hadi Saaa 11.00 jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11. 00 Jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mpaka hivi sasa kwenye orodha niliyoikuta waliobakia wachangiaji wa asubuhi tuna Waheshimiwa watatu akianzia Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Ismail Jussa hajafika na baadaye Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Sasa kama yupo anayetaka kuchangia na baadaye Mwanasheria hana, kama anataka kuchangia alete tuweze kujipanga uzuri, laa kama tukimaliza Mhe. Mwanaidi namwita Mhe. Waziri ili tuanze majumuisho. Kwa hiyo nafasi nampa Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii na mimi nikapata nafasi ya kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea Mswada huu wa Kamisheni ya Ardhi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kusema kweli mimi sitokuwa na mchango mkubwa isipokuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri na kutoa maoni yangu katika Mswada huu. Nitaanza katika kifungu cha 6 chenye muundo wa Kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi cha 6 (2) kinasema:

> "Bila ya kuathiri kifungu kigodo cha (1) cha kifungu hiki, Kamisheni itakuwa na idara zifuatazo:
>
> (a) Idara ya Ardhi,
> (b) Idara ya Ukaguzi na Upimaji,
> (c) Idara ya Mipango Miji na Vijiji."

Mhe. Naibu Spika, mimi hoja yangu nataka Mhe. Waziri atakapokuja pale kwenye marekebisho waliyofanya Kamati kwenye kuongeza msajili wa ardhi nilikuwa nataka nipate maelezo kwa sababu Idara ya Ardhi naona inajitosheleza wenyewe ina naibu wake, inajitegemea wenyewe na mrajisi na yeye naona pia inajitosheleza wenyewe na ina Mkurugenzi wake, sasa naona hapa kwenye marekebisho imechanganishwa. Kwa hivyo nataka nipate ufafanuzi ili nipate kufahamu nijue kuna tatizo gani.

Mhe. Naibu Spika, nitaendelea kifungu cha 17 kuhusu muhuri wa Bodi. Kifungu hichi kinasomeka muhuri wa Bodi utathibitisha kwa kuweka saini ya mwenyekiti, katibu au maafisa wowote wa Bodi kama Bodi itakavyoteua utekelezaji jukumu hilo kwa niaba yake.

Mhe. Naibu Spika, hapa kwenye maneno haya yanayosema au maafisa wowote wa Bodi mimi naona kipengele hichi hakijakaa vizuri, kwa hivyo naomba kiandikwe maofisa watakaoteuliwa na Mwenyekiti au afisa atakayeidhinishwa na Bodi pamoja na Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, mimi hoja zangu ni hizo mbili. Baada ya kusema hayo naunga mkono Mswada huu.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kwa uwezo wake kwa kutuleta hapa tukakutana.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo tu kwa sababu Wajumbe wengi wamekwishachangia na kusisitiza juu ya ardhi yetu ya Zanzibar. Na mimi nitachangia kidogo katika ukurasa wa 291 kifungu cha 2(a) naomba kukariri.

> Kifungu cha 2(a) "Kushauri na kusimamia maendeleo ya uhifadhi wa ardhi"

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ndogo lakini kutokana na hali ya utumizi wa ardhi uliokuwa umekosa mipango basi nchi yetu imekuwa na majengo mengi ambayo yamejengwa kiholela ambayo yamejengwa ndani ya sehemu ambazo hazistahiki, kwa mfano kutokana na maendeleo ambayo yaliyokuwa yamefanywa ujenzi huo, sehemu nyingi zilizojengwa majumba ambazo ni sehemu za maji, yale maji hivi sasa hayapati kupitia kutokana na usimamizi mbaya wa ardhi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo Mswada huu wakati itakapoundwa Kamisheni ya Ardhi, mimi naishauri serikali kwamba sehemu zilizobakia ziwe zinajengwa katika miundo ya mipango miji. Kwa sababu kuna miji imejengwa hata yakitokea matatizo ya raia kupitisha magari kwenda kuchukua kama wagonjwa basi hakuna nafasi za kupita.

Mhe. Naibu Spika, naiomba Wizara isimamie na ihakikishe kwamba sheria hii ya usimamizi wa ardhi katika nchi yetu ya Zanzibar inasimamia kikweli. Kwa sababu sheria tunatunga nyingi sana lakini baada ya kuzitunga haitumiki mipango miji. Utakuta kwamba sehemu nyingi majumba yamejengwa kiholela. Hivi sasa kuna sehemu za njia za

barabara zimekuwa nyembamba kwa kujengwa ujenzi ambao uliokuwa hauna mpango. Kwa ushauri wangu naiomba serikali kupitia Wizara hii ya Ardhi, ihakikishe inasimamia ardhi kisawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile Wajumbe wengi wamechangia na wamesisitiza sana utumiaji wa ardhi na mimi nasisitiza tena na naiomba Wizara ihakikishe inatumia sheria kutokana na ujenzi holela.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango wangu huu mfupi nakushukuru na naunga mkono Mswada huu mia kwa mia.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na sitokuwa na mchango mkubwa sana kwa vile watu wengi wamechangia katika michango yao, wengi sana wameipongeza wizara kuhusiana na kuletwa Mswada huu ambao ni Mswada uliokamilika vizuri na uliopangika vizuri. Kwa hivyo na mimi sitokuwa na mchango mkubwa isipokuwa tu naomba niwashukuru wote wale waliochangia na pia niwaombe kwamba Mswada huu waupitishe bila ya pingamizi yoyote.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo nataka niwaelezee tu kwamba wengi waliochangia wamegusia sana suala zima la matumizi mabaya ya ardhi hususan katika suala la ardhi ndogo ambayo tuliyonayo hapa Zanzibar. Ni kweli kwamba yapo matumizi mabaya ya ardhi kwa baadhi ya wananchi. Kuna baadhi ya wananchi huvamia katika vyanzo vya maji kwa kujenga nyumba holela pamoja na kuvamia maeneo bila ya ridhaa ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane katika kulilinda hili, kwani naamini kwamba kuundwa kwa Kamisheni hii tutajitahidi kuyafuatilia haya na kujitahidi kuhifadhi, lakini pia kwa vyovyote itakavyokuwa ili waweze kufanikiwa vizuri katika utendaji wao wa kazi basi tuhakikishe kwamba Wawakilishi tunashirikiana na Kamisheni hii ili kulinda uvamizi wa maeneo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile limezungumziwa suala zima la kuhusu baadhi ya wananchi kuchukua hatua ya kujipimia viwanja wenyewe. Hili kwa kweli ni tatizo na lipo maeneo mengi tumefuatilia na tumeyagundua matatizo kama hayo, hususan katika maeneo ya Tunguu kuna watu wanajipimia viwanja wenyewe bila ya kusubiri Idara husika au kupeleka ripoti kwenye Idara husika na wakashughulikiwa katika masuala ya kupimiwa viwanja na hatimaye hukosekana aidha mipango miji na watu wakasababisha kujenga nyumba pasipokuwa na utaratibu mzuri. Kwa hivyo vile vile na hili niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi sote tuwe wachunga katika kulichunga hili.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi nimesema kwamba sitochangia sana isipokuwa naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi tena kuja kusimama mbele ya Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi na kutoa ufafanuzi wa hapa na pale katika mazungumzo mbali mbali ambayo Waheshimiwa hawa wamechangia.

Mhe. Naibu Spika, napenda kwanza kabla sijatoa ufafanuzi niwatambue wale ambao wamechangia katika Wizara hii au katika Mswada huu. Mhe. Naibu Spika, wachangiaji waliochangia ni kama hawa wafuatao:

1) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
2) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3) Mhe. Marina Joel Thomas
4) Mhe. Asaa Othman Hamad
5) Mhe. Ali Salum Haji
6) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
7) Mhe. Muhammed Haji Khalid
8) Mhe. Muhammed Mbwana Hamad
9) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
10) Mhe. Rufai Said Rufai
11) Mhe. Mgeni Hassan Juma
12) Mhe. Saleh Nassor Juma
13) Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
14) Mhe. Abdi Mossi Kombo
15) Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

Mhe. Naibu Spika, mazungumzo yalikuwa ni mengi na michango ilikuwa ya maana sana na yametajwa mambo mengi kwa pamoja ambayo ni ya kawaida katika kushughulikia masuala mazima ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, inaonesha kwamba wajumbe wanakubaliana na hili wazo la kuleta Kamisheni ya Ardhi kwa mara nyengine baada ya ile iliyokuwepo zamani kuondoshwa na sheria ile ikafutwa sasa hivi ndio tunaandika sheria mpya kabisa ya kuunda Kamisheni ya Ardhi, nimetiwa moyo sana na michango ya Wajumbe kwamba hili wamekubaliana nalo.

Mhe, Naibu Spika, kabla sijazungumza mchango wa Wajumbe mmoja mmoja nataka nizungumzie kwamba ardhi Zanzibar wote wamekubali kwamba ni ndogo na ni kweli kwamba ardhi yetu ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watu namna tunavyoongezeka, lakini nataka niseme tu kwamba ardhi ni ndogo inahitaji kulindwa na inahitaji kuleta manufaa kwa wananchi wetu. Hili ni suala muhimu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye miaka ya 1982, ilikuwepo *proposal* ya kuupanga mji wa Zanzibar ili uweze kuchukua watu wengi katika eneo dogo badala ya mji huu kutawanyika kama ulivyotawanyika sasa hivi. Hivi juzi tu kulikuwa kuna wataalamu kutoka *World Bank,* walikuja hapa Unguja wakatembelea na Pemba. Pia wakapendekeza *Master plan* ya kutumia ardhi yaani *Land Plan. Master Plan* hiyo Mhe. Naibu Spika, wameshatukabidhi na kwa kweli tunakaribia hivi sasa hivi kuifikisha kwa wananchi kuwapa taaluma ya nini tumepanga katika matumizi ya ardhi. Hili linakwenda pamoja na michango ya Wajumbe waliozungumza kwamba ardhi ya Zanzibar haina mpango.

Mhe. Naibu Spika, ardhi ya Zanzibar inayo mpango na muda si mrefu wataufahamu mpango wa ardhi ya Zanzibar namna ulivyopangwa sasa hivi kutumika kwake. Mpango huo umeeleza maeneo ya mji yatafikia wapi, maeneo ya kilimo yatapatikana wapi, maeneo ya utalii yapo sehemu gani. Yote yamepangwa katika mpango huu mpya wa matumizi ya ardhi, mjini na mashamba, Unguja na Pemba. Hili nashukuru sana kwamba limekuwa.

Mhe. Naibu Spika, isipokuwa kuna tatizo na hili ndio nataka nilizungumze mimi. Moja katika changamoto ambayo tunapambana nayo sisi ni kuyatumia maeneo ya kilimo. Nikisema kilimo sikusudii mpunga tu, nakusudia mpunga, mgomba, muhogo, viazi vitamu na kadhalika. Pia na mazao ya biashara kama mikarafuu, minazi na mazao ya matunda kama miembe, michungwa na miti mengineyo.

Maeneo haya Mhe. Spika, ni kweli sasa hivi yamevamiwa sana na watu wanakata miti hii kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Mimi naomba Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wajitahidi kulinda suala hili lisitokezee. Hapa kuna mtindo unatumika, watu waliopewa eka za serikali wanaziuza viwanja. Hili ni kosa wanaojua sheria ya eka, ukiisoma sheria ya eka imeeleza wazi kabisa. Eka unapewa kwa ajili ya kuendeleza na unatoa ahadi hasa ndani ya mkataba wako eka kwamba ardhi ile uliyopewa kwamba itaendelea kuwa kijani na itakuwa inaleta mazao kwa manufaa ya nchi hii. Bahati mbaya watu wanaziuza viwanja.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi hapa nilijibu swali juu ya suala la utoaji wa hati za viwanja. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema na nataka maofisa wangu walielewe hilo, kwamba kiwanja chochote ambacho hakikupimwa kihalali, wameuziana wenyewe kwa wenyewe basi mimi naona ni vizuri kwamba Wizara yangu isitoe hati katika kiwanja hicho kabisa. Kwa hivyo wale wanaotaka kununua viwanja katika maeneo ambayo hayakupimwa na Serikali wanauziana wenyewe kwa wenyewe huko wasitegemee kuja Wizarani na kupata hati ya kiwanja kile, hatutoi hati, kwa sababu ya kuilinda ardhi. Na maofisa wangu naomba hili walitekeleze vizuri kabisa, wasikubali kumruhusu mtu kutoa hati katika kiwanja ambacho hakikupimwa rasmi na Serikali, ni kiwanja tu kipo hakikupimwa rasmi na Serikali, kiwanja hicho hukijui *unit* gani, hukijui ni *block* ni namba ngapi lakini watu wanajenga huko halafu wanakuja huku wanalalamika hatupati hati kumbe vile wanavamia maeneo ya kilimo.

Mimi sitaki tufike kiwango katika nchi hii ikawa hatuwezi hata kuvumbua chakula chetu katika ardhi yetu tuliyonayo. Hili ni suala Mhe. Naibu Spika, nimeona niliseme mwanzo kabisa ili nisije nikasahau katika kuzungumzia masuala hayo. Kwa hivyo wale wanaonunua viwanja kutoka katika eka wasitegemee kupata hati kutoka katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Viwanja vyote vitapimwa na Serikali na vitatengenezwa na Serikali na wanaendelea na kazi hiyo hivi sasa kwa madhumuni ya kugawa. Sasa wanaouziana huko na huko wenyewe kwa wenyewe Mhe. Naibu Spika, hili litakuwa ni tatizo kusema kweli. Naona kwamba Wizara yangu nitasimamia kipindi hiki chote kwamba tusitoe kiwanja katika ardhi ambayo ni ya eka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu amezungumzia marekebisho yaliyomo katika sheria hii, marekebisho mazuri, tunayapokea na tutayafanyia kazi. Isipokuwa kuna rekebisho moja tu ambalo jana Mhe. Mwanasheria Mkuu alilitolea ufafanuzi lile la kwamba Waziri anaweza kutunga, anasema Waziri atunge Kanuni ile ndio kama alivyoizungumza jana Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo ile itabakia kama ilivyopitishwa katika mswada ambao umepita jana, lakini mengine nataka kufanya marekebisho kwamba tulipokuwa na Kamati tuliulizana sana juu ya suala la Ofisi ya Msajili wa Ardhi kwamba ikae pamoja na Idara ya Ardhi au iwe peke yake. Ushauri tulioupata kutoka Mwanasheria Mkuu kwamba ni vizuri Msajili abakie chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara moja kwa moja badala ya kuwa chini ya Idara ya Ardhi, huo ndio ushauri ambao tumeupata na hivyo marekebisho hayo kama yamo maana yake yanakaa sawa katika kiwango hicho kwamba Msajili wa Ardhi atabakia chini ya Wizara ya Ardhi na hatokuwa chini ya Kamisheni ya Ardhi kama ilivyo sasa hivi. Halikadhalika kuna suala la Mahkama ya Ardhi nayo pia itakuwa moja kwa moja imejitegemea haitakuwa chini ya Kamisheni ya Ardhi, hili ni rekebisho moja ambalo nimependa kulizungumza.

Mhe. Makame Mshimba amewapongeza watu wa Kamati kwa marekebisho mazuri waliyoyafanya. Halafu amezungumzia hoja fulani inayohusu mtu aliyechukua ardhi na ku-*forge* hati za saini ya Waziri. Mhe. Naibu Spika, kazi hii ni ngumu sana na ni ngumu kwa sababu tuko katika maisha sasa hivi ya utandawazi na tuko katika maisha ya teknolojia ya kisasa.

Mhe. Naibu Spika, saini yako kupatikana sasa hivi si tabu hata kidogo, ukishaiweka kwenye karatasi ni rahisi watu kuifanyia *scanning*, wanai-*scan* na wanaiweka wanapotaka na wanatengeneza *document* na saini yako inakuwa *scanned* inaonekana kabisa pale kama ni *sign* yako mwenyewe imechukuliwa vile vile ulivyoiandika mwenyewe. Hakuna lile suala la kupiga *drawing* sasa hivi ukatengeneza saini kwa kutumia kalamu, watu wana-*scan* siku hizi *signature*.

Kwa hivyo nataka kuwaambia wajumbe wenzangu si kila *sign* unayoiona inaandikwa imeandikwa na Waziri ukasema hiyo *sign* ni sahihi, hiyo *sign* pengine imekuwa *scanned* hapo. Kwa hivyo inahitaji kufuatiliwa na inahitaji kufanyiwa uchunguzi. Kwa hivyo ile kesi ambayo iliyozungumzwa na Mhe. Makame Mshimba mimi nimeifuatilia kwa ukamilifu kabisa na nimetia wasiwasi kwamba ile *sign* sidhani kama nimeitia kwa mkono wangu hata ikawa inafanana na yangu nina wasiwasi. Na nina wasiwasi huu kwa sababu aliyehusika nilimuomba alete hiyo *document* ambayo nilitia *sign* kwa mkono wangu tangu mwezi wa Januari mwaka huu, hakuileta hati hiyo mpaka mwaka umemalizika.

Januari ya mwaka jana 2014 hakuleta hati hiyo mpaka mwaka huu unamalizika kaja kuleta Januari hii 2015, mwaka mzima hati alikuwa kaificha wapi. Sasa hapa kuna wasiwasi kwamba wewe hati unasema mimi nimei-*sign* hii hati ilete basi niione, tangu mwaka huo mpaka Januari mwaka huu ndio unakuja kuileta kwamba hii sasa hivi *sign* haiwezi kukubalika, kwa sababu ilikuwa wewe kama nimekwambia uilete tarehe 5 Januari basi angalau ulete Februari, kwa sababu pengine ulikuwa umeficha, umei-*misplace* mahala huijui iko wapi, lakini baada ya mwaka mzima ndio unaileta hati.

Mhe. Naibu Spika, ile hati mimi siikubali kwa sababu angeileta mapema mimi ningeikubali kabisa, lakini kwa alivyoileta na ukumbusho nimefanya mwingi tu. Nimekuwa nikimkumbusha kila mara watu ninawatuma mfuateni, mwambieni akupeni hiyo hati aliyosema mimi nimeifuta, haleti. Hati ile Mheshimiwa ilifika wakati mimi nikaifuta tena kwa sababu sijui kama ni yangu au vipi na nikasema kabisa kiwanja kile ninakirejesha utaratibu ule wa kawaida kwa sababu ile hati nilikuwa sikupewa mimi. Lakini leo ninasikia hiyo hati ipo baada ya mwaka mzima sijui kama ilifichwa wapi.

Sitaki kuzungumza mengi kwa sababu juzi nimepokea barua moja ya mwanasheria mmoja amefungua kesi mahkamani, tangu wakati huo tunapiga kelele hukufungua kesi unafungua kesi leo. Sitaki kuyazungumza mengi maana yake sitaki kumpa faida huyo wakili nataka bora tuendelee kuitizama hii kesi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi yangu itatizama hii kesi ilivyo na tutatizama kama Mwanasheria ataruhusu izungumzwe tutatizama hatua gani tutapita, sitaki kutaja mambo yote ambayo ninayoyaona.

Ninazo *findings* za kutosha kabisa za uthibitisho wa ujanja huu uliofanywa kuhusu hati hii na ikifika wakati nitautoa huu uthibitisho, lakini sio kwa sababu juzi nimepata taarifa tarehe 5 Machi, ndio kenda mahkamani, tarehe 5 Machi, ndio katoa indhari tangu Januari 2014 juzi ndio anatoa indhari anakwenda Mahkamani, baada ya kushindwa kuleta

juzi ndio kavumbua hati mwaka mzima kweli hati ilikuwepo. Mimi nina wasiwasi sana katika hilo, lakini Mwanasheria Mkuu atajua vya kufanya baadaye.

Mhe. Naibu Spika, michango mengine iliyotolewa ambayo mingi ilikuwa ikinipongeza zaidi kuliko mambo mengine yaani kutupongeza Wizara mimi na maofisa wangu pale, kuwa tumefanya kazi nzuri na tumefanya uamuzi mzuri wa kuleta mswada huu ili kuanzisha Kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, dhamiri hasa ya kuleta hii ni kuondoa nguvu za mtu mmoja kushughulikia masuala ya ardhi akawa anatoa amri yeye kila kitu na anatoa uamuzi wa kila kitu. Ni bora tuunde hii Kamisheni ambayo anayeomba ardhi atapeleka maombi yake kwenye Kamisheni, Kamisheni itapima itajua panapatikana kiwanja, hawa maofisa wangu wote wa ardhi, wa upimaji watathibitisha mbele ya kikao cha Kamisheni uhalali wa kile kiwanja, wakishathibitisha hilo kwamba ni halali kiwanja na Kamisheni ikiona panastahiki kutolewa kutokana na mradi ule ndio wataleta kwa Waziri kwa ajili ya kutiliwa saini, kuliko sasa hivi ukafanya na mtu mmoja, watu wawili na ndio madhumuni ya Kamisheni hii, kupunguza migogoro ya ardhi ikiwezekana kuiondoa kabisa isitokee tena migogoro ya ardhi. Vyombo hivi tunavyoviunda tutajitahidi kuvitafutia vitendea kazi kama alivyoshauri Mhe. Makame Mshimba.

Ninamshukuru Mhe. Makame Mshimba kama alivyosema tunao wataalamu, wataalamu wa ardhi tunao tatizo linatokea sijui kunakuja shetani gani matatizo yakatokea hapa na pale. Wataalamu wa ardhi kweli tunao na tutaendelea kuwatumia hawa hawa.

Mhe. Marina amezungumzia juu ya migogoro kuwepo na amezungumza sana kwamba masheha na halmashauri hawahusiki na suala la kugawa ardhi. Kama mtu anakwenda kununua kiwanja kwa Sheha kuna ujumbe unatolewa na Makombora kila siku. Makombora kauziwa kiwanja na Sheha na mwengine kauziwa kiwanja na Diwani, sasa anapigiwa simu Diwani kuulizwa habari ya kiwanja diwani anawajibu mtajuana wenyewe. Ule ni ujumbe makusudi umeletwa kwamba mtajuana wenyewe yeye keshauza, kwa hivyo haambiwi tena. Sasa wananchi wajitahidi sana wasinunue viwanja ovyo ovyo kwa Masheha au kwa Madiwani au kwa Halmashauri, wasinunue viwanja, sheria inakataza kabisa kununua viwanja kutoka katika maeneo hayo.

Ujenzi katika maeneo yasiyostahiki alivyosema Mhe. Marina tutajitahidi na nafikiri hii Kamisheni itashughulikia masuala hayo, kutoa elimu imo hata kwenye hii sheria yenyewe kuna kifungu kinazungumzia kwamba, kilizungumzwa hapa na Mhe. Ali Salum Haji juu ya kuratibu elimu ambacho ni kifungu cha 4(2)(j) kinazungumzia suala la kuratibu masuala ya elimu yaani kutoa elimu. Kwa hivyo kimo humu humu kifungu cha kutoa elimu.

Mhe. Asaa Othman nakushukuru sana kwa mawaidha yako mazuri na kututahadharisha, ametutahadharisha sana kwamba ardhi yetu ni ndogo sisi viongozi tusichukuwe maeneo makubwa tukawaacha tunaowaongoza hawana hata pa kulima.

Nashukuru sana kwa mawaidha haya Mhe. Asaa ameyaeleza na hiyo *commitment* aliyoihimiza tutajitahidi maana viongozi wenyewe ndio sisi hapa, *commitment* hiyo nafikiri tutajitahidi kuwa nayo sote tuliopo hapa, kwa sababu sote ndio viongozi, hili suala hili halimuhusu kiongozi mmoja, linaanzia tangu kwa Waziri mpaka kwenda chini huko, kila kiongozi anatakiwa awe *committed* katika suala hili. Na amesema kwamba mtu yeyote anayeghushi hati aondolewe katika kazi. Mheshimiwa hiyo jitihada tunaifanya sana tukiwagundua watu wanafanya mazonge mazonge tunawaondoa katika Idara hii ya Ardhi na tunawatafutia sehemu nyengine kwenda kufanya kazi, hilo tunajitahidi sana.

Amehimiza vile vile kwamba *open space* zisivamiwe. Ni kweli kabisa *open space* zisivamiwe kwa sababu watoto wetu ndio mwahala mwa kucheza na pia amezungumzia suala la pahala pa kujengwa pajulikanwe ndio hilo suala la *land use plan* ambayo ipo tayari sasa hivi imeshatengenezwa. *World Bank* wamesaidia na tumeshaipata. Mhe. Asaa amesema ana imani sana na kuundwa kwa Kamisheni hii, kwa hivyo inaelekea kaunga mkono moja kwa moja.

Mhe. Ali Salum Haji amezungumzia juu ya ardhi walikuwa wana tatizo na kama kwamba mwenyewe hajulikani, sasa hivi kwa sababu tutakuwa na Kamisheni ya Ardhi, mwenye ardhi atajulikana kwamba ni Serikali moja kwa moja, hiki chombo cha Serikali kitalinda ardhi kwa niaba ya Serikali na sasa hakutokuwa tena nafasi ya kufanya

ujanja wa hapa na pale. Kama mtu anataka kuwa *corrupt* watu wa ardhi basi itabidi ende kwenye Kamisheni nzima akai-*corrupt* kila mtu apate chake, ndio itakavyokuwa, haiwezi kufanyika vyengine vyovyote tena.

Pia amehimiza Mhe. Ali Salum Haji kwamba *open space* nazo zisijengwe ziachwe kama zilivyo.

Mhe. Bikame amezungumza miamala. Miamala kwa kizungu ni *transaction* sijui kwa Kiswahili nizitaje vipi ni moja katika njia na taratibu za kufanya biashara. Sasa sijui tuite vipi kwa Kiswahili, lakini ni kwamba unapokwenda kutaka hati ya ardhi kwanza kuna pesa za kununua hiyo fomu yenyewe kama unataka kuhaulisha ndio muamala wa kwanza huo. Kuna suala la kutoa pesa kwa ajili ya kuandikiwa hiyo hati, kupimiwa lile eneo unalipa vile vile na kuandikiwa ile hati ina malipo yake hiyo ndiyo inayoitwa miamala.

Miamala ndio hizo pesa ambazo unazilipa mbali ya lile suala la *lease, lease* linakwenda kwenye ZRB moja kwa moja, lakini kuna pesa zinakusanywa pale pale katika Idara ya Ardhi na Usajili moja kwa moja pale unapopimiwa zile ada unazolipa ndio miamala yenyewe ndio biashara yenyewe ile.

Amekemea sana juu ya suala la kujenga katika maeneo ya kilimo. Nakubaliana na wewe Mhe. Bikame na sisi ndio viongozi wenyewe nadhani tutashughulikia suala hilo. Halafu kuna watu wanachukua ardhi wanaiweka bure bila kuitumia, nimesikia wito wake Mhe. Bikame kuna ardhi najua iko Micheweni pale inamsumbua sana lakini asiwe na wasiwasi atalipata jibu baada ya muda mfupi sana tu na watu wa Micheweni inawasumbua ardhi hiyo. Kwa sababu wanasema imechukuliwa lakini haina lililofanywa na watu hawana pa kulima, nimemfahamu vizuri aliposema suala hili pamoja na kuwa nilitoka nje kidogo lakini huko nje nilikuwa ninamsikiliza yeye anavyosema, kwa hivyo niliyakamata yote hayo.

Halafu akasema kwa nini katika hii Kamisheni ya Ardhi hamna mtu wa Mazingira, hata ikiwa humu hamna mtu wa mazingira lakini hii Idara ya Ardhi na Idara ya Mazingira wanafanya kazi pamoja, pamoja na kuwa wako Wizara mbali mbali lakini wanafanya kazi pamoja. Kwa hivyo mashirikiano yapo na mara nyingi wanavyofanya, hata walipoamua suala la ukanda wa ufukwe walishauriana pamoja kuomba ukanda ufukwe uwe una upana fulani kutoka mahala panapojaa maji mpaka kwenye mpaka ambako mtu anatajiwa aanze kujenga. Kwa hivyo hawa wanafanya kazi pamoja.

Halafu aliuliza hili suala la hizi fedha zitapatikana kutoka kwa wakodishwaji wakubwa, pesa za wakodishwaji wakubwa hatuzipati sisi Idara ya Ardhi zinakwenda kwenye bajeti, zinaletwa hapa wakati wa bajeti kutoka kwenye ZRB, sisi tunapata zile za kidogo kidogo kupima kiwanja, kutengeneza hati hizo ndizo tunazopata sisi, zile za wakubwa hatupati sisi kabisa.
Pia amezungumzia juu ya suala la utaalamu angalau wa miaka 7, kuna wenzio wamependekeza kwamba miaka 5. Mimi nakubaliana na ushauri wa kwamba angalau mjumbe wa bodi awe utaalamu wa miaka 5 hii nakubaliana na ushauri huo. Tutapunguza kutoka 7 tufanye miaka 5. Kuna wajumbe wengine walizungumza suala hili, tunakubaliana kwamba akishapata uzoefu mtu utawala wa miaka 5 basi moja kwa moja anaweza kuwa mjumbe katika bodi hii. Mwenyekiti ana sifa zake, Mwenyekiti sifa zake mbali yeye lakini ukija hawa wajumbe wa bodi ndio ana hizi sifa za kwamba uzoefu na utaalamu angalau wa miaka 5 katika masuala ya ardhi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, ametoa historia ya kabla ya Mapinduzi na baada ya Mapinduzi. Mheshimiwa ninakubaliana naye kwamba kabla ya Mapinduzi ardhi hii ilimilikiwa na wachache na sasa hivi ardhi ni mali ya Serikali. Na alizungumzia kwamba tunakosa mipango mema ya matumizi ya ardhi ndio nimeshamwambia kwamba kwa kweli hivi sasa tunayo tayari mipango ya ardhi na tutaitangaza muda si mrefu na watu wataipata.

Idara za Kamisheni zipo, je, hii Kamisheni itakuwa chini ya nani. Kamisheni itakuwa chini ya Wizara na ndiyo maana kuna baadhi ya vifungu katika sheria hii vimemtaja kwamba Waziri atakuwa anatoa maelekezo katika Kamisheni hii, kwa hivyo itakuwa moja kwa moja iko chini ya Wizara.

Kazi za Kamisheni amezungumza Mhe. Mohammed Haji Khalid, ukaguzi na upimaji. Nasema ni ile sehemu ya upimaji na ramani tunapozungumzia upimaji wa ardhi sio wa viwanja tu lakini na nchi yenyewe kuitengenezea ramani nao pia ni upimaji kwa kipimo maalum. Kwa hivyo hiyo ni Idara ya Ukaguzi na Upimaji ambayo ndiyo inayotengeneza ramani; mipaka ya Wilaya, mipaka ya Mkoa hiyo ndio Idara ya Ukaguzi na Upimaji ambayo inashughulikia masuala hayo.

Mawasiliano na Taasisi zinazotumia ardhi hilo ni suala muhimu kabisa. Mhe. Mohammed Haji tutazishughulikia. Na sheria zinazoendana na sheria hii ziletwe Barazani zifanyiwe marekebisho. Nimeshaahidi kabisa kwamba hizo tutazileta Barazani na kufanya marekebisho.

Kinga inahitaji watu kupatiwa elimu kwa wananchi, suala la elimu limo hata katika kazi za Kamisheni.

Halafu Mhe. Mohammed Mbwana Hamad ametoa indhari kwamba ardhi ikitumiwa vibaya vizazi vyetu vitakuwa na matatizo na kukosa maeneo mazuri ya kuishi. Ni kweli Mhe. Mohammed Mbwana suala hili tunalipokea na kwa sababu sisi ndio viongozi wenyewe tuiunge mkono Kamisheni hii na baadaye tuje tuisaidie ili ardhi ipate ulinzi wa uhakika kabisa. Amezungumza hatuna maeneo tuliyoyatenga kwa madhumuni ya kilimo, ujenzi na michezo, nimeshasema kwamba *master plan* ya ardhi ipo tayari na utaipata baada ya muda mfupi.

Halafu kuna watu wanajikatia viwanja wenyewe nimeshasema kabisa ukiuziwa kiwanja katika eneo ambalo umejipimia mwenyewe kwa sababu hicho kiwanja hakikufika utaratibu wake unaotakiwa katika kupima viwanja huo ni utapeli wa aina yake ambao watu wanakubali wanauziwa viwanja. Nasema upimaji wanaotumia watu wenyewe si upimaji wa kutolea hati kwa sababu ni upimaji ambao kitaalamu tunaweza kuita *demarcation* tu basi, yaani upimaji wa kuweka viwanja na kutia mipaka *beacon* bila ya kupima rasmi yaani *coordination*, upimaji unaoelezea eneo kwa ufasaha wake katika lugha ya upimaji, upimaji ni lugha maalum. Sio kuweka kijiwe tu ukasema kijiwe na msumari ndio ikawa ushapima kiwanja hicho hujakipima, upimaji una viwango vyake. Una viwango sahihi vya kitaifa na kimataifa vya kuweza kugawa na kutoa hati kwa maeneo ya mijini na usahihi na unahitajika upatikane katika shughuli za upimaji. Viwanja vya *demarcation* havina usahihi kwenye kuchora na ndio maana kama ikibidi kutoa hati inatolewa *provisional of occupancy* yaani ikitokea matumizi ardhi ile unatumia tena, inatoka hati ya muda haitoki hati ya kudumu moja kwa moja. Ni utambulisho tu sio utaratibu wa kupata matumizi kwa ajili ya muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Wanu amependekeza kuna vifungu vihamishwe kutoka katika sehemu nyengine kuleta katika sehemu nyengine. Mimi ninamshauri kwa sababu marekebisho mengi yameshafanywa na Kamati na tumeshayakubali isipokuwa yale mawili, ningemuomba Mhe. Wanu hili akatuachia likakaa vile ilivyokaa hivi sasa hakuna matatizo yoyote.

Pia amesema suala la *gender issue* kwamba lazima wanawake wapate. Tunakubali kukirekebisha kifungu kile cha wateule watatu angalau mmoja awe mwanamke. Kama nilivyosema jana angalau mmoja wale wanaoteuliwa na waziri awe mwanamke. Hii angalau maana yake inawezekana wakawa wawili wanawake, inawezekana wakawa wote watatu wanawake, lakini angalau mmoja yaani asikosekane mwanamke ndio maana yake katika lugha ya kisheria, kwamba angalau mmoja awe mwanamke katika uteuzi wa waziri. Hii nakubaliana nayo ambayo Mhe. Mgeni pia aliizungumza hiyo, hii inatoa nafasi kwa wanawake kupata wakati mwengine nafasi mbili au zote tatu wakati mwengine wanazipata wao, kwa sababu ni kwamba haikufunga kuliko ukaifunga kabisa wakati huo wanaume watupu, basi angalau mmoja awe mwanamke wanaweza wakawa wawili lakini angalau mmoja awe mwanamke.

Mhe. Rufai Said Rufai ameshukuru sana kwa kuweka chombo hiki na ametoa mawaidha mengi kabisa ya namna ya chombo hiki kinavyotakiwa kifanye kazi na amevisifu vingi kabisa namna vilivyoshughulikia suala zima la ardhi, lakini amezungumzia kwamba uwepo mpango wa kurejesha ardhi wakati tunapochimba mawe au tunapozoa mchanga. Nafikiri katika sheria ya mazingira juzi kifungu hiki kimo katika sheria ya mazingira ya juzi, utaratibu gani anayechimba mchanga atatakiwa kurejesha ardhi ile irudi kama ilivyo zamani. Hii ni kazi ya Idara ya Mazingira, kwa hivyo hiyo Mhe. Rufai itashughulikiwa moja kwa moja katika sheria ile ya mazingira.

Suala la elimu nimeshakubali wananchi watapatiwa elimu na amesema uzoefu wa hawa wanaotoka ndani ya bodi angalau miaka mitano. Nakubaliana na wewe tutachukua angalau miaka mitano.

Mhe. Mgeni Hassan Juma yeye ametoa pongezi vile vile na akasema katika uteuzi tusiwaache twende kwenye shahada angalau ya pili. Nakubaliana na rai yake ni nzuri sana, lakini ukitizama kimataifa hasa tunaanza kumtambua mtu kwenye shahada ya kwanza. Kwa hivyo, si kama shahada ya pili hachukuliwi, atachukuliwa, kwa sababu akiwa pana shahada ya kwanza na shahada ya pili wanalingana, basi huyo shahada ya pili ndio anafaa kuchukuliwa

kusema kweli. Hiyo ndio jitihada itabidi ifanyike katika suala hili kuliko tukaifunga moja kwa moja kwenye shahada ya pili haizuii hiyo.

Halafu suala la kuidhinisha bajeti tukitaka kupeleka taarifa za matumizi nafikiri katika sheria hii kuna kifungu kwamba Kamisheni itabidi kila baada ya muda ipeleke taarifa ya matumizi kwa Mhe. Waziri na pia itakuwa inafanyiwa *auditing* kama kawaida na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataikagua hii Kamisheni na itakuwa inafanyiwa *auditing* kama kawaida.

Suala la *gender* nakubaliana naye vile vile na suala la elimu nakubaliana naye nimeshasema limo katika sheria hii vile vile. Yeye ameongeza kitu kimoja kwamba elimu iwe pamoja na wajumbe wa bodi isiwe elimu yenyewe inatolewa kwa wale watendaji tu, watendaji wapatiwe elimu na wajumbe wa bodi nao wapatiwe elimu. Nakubaliana na rai yake hii *inshaallah* na nafikiri wanaohusika na utekelezaji wa suala hili watatekeleza. Na ni kweli kuna baadhi ya bodi wanapatiwa nafasi ya kupata mafunzo angalau wanakwenda mahala wanakaa wiki mbili, wiki tatu kupata uzoefu wa sehemu nyengine, nchi nyengine wanapelekwa vile vile kama Baraza la Wawakilishi linapoondolewa hapa wakati mwengine unapelekwa nje ya nchi, wakati mwengine unapelekwa Tanzania Bara basi na hii ni nzuri kabisa Mhe. Mgeni ameipendekeza.

Mhe. Saleh Nassor Juma amezungumzia kwamba mswada huu ni mkombozi wa wakulima. Nakubaliana naye kabisa ni mkombozi wa wakulima kamisheni hii ikifanya kazi yake vizuri basi hizi halat halat za ndani ya ardhi zitapungua na hazitakuwepo kabisa zitaondoka kabisa. Kwa hivyo, nakubaliana naye.

Mheshimiwa amesikitika sana kwamba walikuwa wana ardhi kule, lakini ardhi yote imejengwa na ndio iliyomsaidia yeye katika kusoma ardhi ile, lakini sasa hivi yote haipo. Nampa pole sana Mhe. Saleh Nassor Juma lakini nafikiri *master plan* yetu itakayokuja itatoa nafasi ya sehemu za kilimo na wananchi watapata sehemu za kilimo vile vile kama walivyokuwa wakipata zamani. Bila shaka tukitekeleza *land use plan* tukubali kuna maeneo ya majumba yatavunjwa kwa sababu yamo katika maeneo ya kilimo, lazima itabidi majumba yavunjwe. Ukitaka kujenga nchi lazima ule hasara wakati mwengine maana unaweza ukasema *master plan* itatekelekezaje, itatekelezwa hapa hapa, hapo hapo Mwembelandu ndio patatengenezwa *master plan* ya mji, hapo hapo Kwahani ndio patengenezwe *master plan* ya mji humo humo ndio inamotekelezwa.

Mzee Karume alipotengeneza *master plan* akatuonesha mfano hapa alitengeneza mule mule. Alijenga Kikwajuni, ikisha akaenda tena Kilimani, akaja akajenga Michenzani akawaondoa watu akawahamishia Kilimani, wakaenda Kilimani kule Michenzani wakapata kusimamisha majumba. Kwa hivyo, ndio huo utaratibu wa kujenga nchi hakuna mwengine humu humu, na majumba yetu ndimo itakapopita *master plan* na ndimo mtakamojengwa majumba ya kisasa humo humo sio mwengine. Inabidi ipatikane fedha tu na tuombe Mungu yapatikane hayo mafuta tuweze kuwahamisha watu hapa kuwapeleka hapa, lazima ujenge nyumba ya kuweza kumtoa hapa mtu kumuhamishia hapa katika kutengeneza *master plan* ile kama alivyokwishafanya Mzee Karume. Mzee Karume alituonesha njia maana alijenga Kilimani, akajenga Chake-Chake, akajenga Wete, akajenga Micheweni, akajenga mpaka huku Kengeja Kusini alituonesha mfano. Kwa hivyo, ilikuwa mfano huu tuufuate twende nao katika kujenga nchi yetu na sasa hivi tumeshatanabahi itabidi lazima tupite kule kule hatuna njia nyengine.

Mhe. Mwanaidi Kassim alizungumzia sana juu ya Idara ya Ardhi waifanyie marekebisho juu ya suala la Ofisi ya Msajili kwamba inajitegemea. Ni kweli hata Mwanasheria Mkuu ameshauri kwamba Ofisi ya Msajili aachiwe peke yake ajitegemee isiwe pamoja na Idara ya Ardhi kama ilivyo sasa hivi.

Halafu Mhe. Abdi Mossi Kombo ardhi iliyokosa mipango sehemu nyingi zimejengwa. Nakubaliana naye ni kilio cha watu wengi kabisa na sasa hivi tunakuja na *master plan*.

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema *master plan* au *land use plan* tutaisimamia sisi, sisi wenyewe viongozi tuliopo hapa ndio tutakaoisimamia, tuondoe muhali tu basi, tujue kwamba tukishapewa kila mtu akishajua hapa pa kilimo pawe na kilimo, hapa pa ujenzi pana ujenzi, hapa pa wafugaji pawe na ufugaji, tuwe hivyo tu.
Mhe. Naibu Spika baada ya maelezo hayo pengine naweza kuwa nimeacha baadhi ya maneno ya hapa na pale Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa kwa jumla niwahoji wale wanaokubaliana na hoja aliyotoa Mhe. Waziri wanyooshe mkono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Kamisheni ya Ardhi ya 2015

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Kamisheni ya Ardhi

Kifungu 3 Kuanzishwa Kamisheni ya Ardhi
Kifungu 4 Kazi za Kamisheni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 Uwezo wa Kamisheni pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Uongozi wa Kamisheni

Kifungu 6 Muundo wa Kamisheni pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 Bodi ya Kamisheni
Kifungu 8 Wafanyakazi wa Kamisheni
Kifungu 9 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Muda wa Bodi
Kifungu 11 Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Uwezo wa Bodi
Kifungu 13 Uteuzi na sifa za Katibu Mtendaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 Sekretarieti
Kifungu 15 Vikao vya Bodi
Kifungu 16 Ajenda za vikao
Kifungu 17 Muhuri wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18 Kumbukumbu za taarifa za Bodi
Kifungu 19 Ripoti za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 Posho kwa Wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 Pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano

Masharti ya Fedha

Kifungu 22 Kanuni za Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23 Bajeti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24 Fedha za Kamisheni pamoja na marekebisho yake

Kifungu 25 Ripoti ya kila mwaka pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Sita

Masharti Mengineyo

Kifungu 26 Makosa na adhabu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27 Kanuni
Kifungu 28 Marekebisho ya sheria ya uhaulishaji ardhi
Kifungu 29 Kubakiza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mkono, waliokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kamisheni ya Ardhi ya 2015

(Kusomwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na mambo yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji waliokubaliana na Mhe. Waziri wanyooshe mkono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Kamisheni ya Ardhi ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa ushirikiano wenu na kuweza kupitisha mswada wetu huu, sasa tumebaki na mswada wa Waziri wa Habari kwa kuwa waligaiwa Waheshimiwa mswada hivi mchana tumependekeza kwamba Mhe. Waziri awasilishe na hotuba ya Mwenyekiti twende nyumbani tukasome kesho tutaanza michangio baada ya maswali na majibu. Kwa hivyo, namwita Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuwasilisha mswada wake.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ya 2015

(Kusomwa Mara ya Pili)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusitoke tusikilize hotuba, Mhe. Hamza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya kuanzisha Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo na kufuta Sheria ya Baraza la Sanaa na Muziki Nam. 6 ya mwaka 1983 na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa na maonesho Nam. 1 ya mwaka 2009.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kwa niaba ya Shirika la Magazeti ya Serikali naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu aiweke mahala pema peponi roho ya aliyekuwa Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Magazeti na Mjumbe wa Baraza hili Tukufu Marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin aliyefariki hivi karibuni. Aidha, naomba Mwenyezi Mungu awape subra wafiwa wote.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nitoe shukrani za kipekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uweshaji na Habari chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Bubwini kwa kuupitia mswada huu na kutoa marekebisho, michango na maoni yao ambayo yamesaidia sana kuimarisha Rasimu ya Sheria ya Kuanzisha Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar.

Vile vile nachukua fursa hii kuwashukuru wanaohusika wote walioshiriki katika maandalizi ya mswada huu kwa kutoa maoni yao ambayo yamesaidia kufanikisha kutungwa kwa mswada huu wa sheria. Kwa hakika wahusika mbali mbali walitoa ushauri, maoni na marekebisho mengi sana ambayo hayakuathiri maudhui na maana ya mswada halisi. Kwa vile marekebisho yalikuwa mengi tuliona ni busara zaidi kuyakubali na kuchapisha upya yaliyozingatia maoni tuliyopewa.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya mswada huu ni kuanzisha sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na kufuta Sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki, Zanzibar na Sheria Nam. 1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa na Filamu na Sanaa za Maonesho, Zanzibar.

Mswada wa sheria unaopendekezwa una lengo la kuunganisha majukumu ya Baraza la Sanaa na Muziki na yale ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ili kusimamia vyema na kwa ufanisi zaidi majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kudumisha mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari na kuutumia utamaduni kama njia bora ya kupunguza umasikini kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko mengi yaliyotolewa na yanayoendelea kutolewa na jamii, wageni na wafanyabiashara wakiwemo sekta ya utalii. Malalamiko haya yalianza kujitokeza tokea mwanzoni mwa mwaka 2000. Kuna bughudha ambazo zinatokana na utekelezaji wa sheria hizo. Mambo makuu yanayolalamikiwa ni pamoja na ghasia zinazosababishwa na ngoma zinazopigwa katika makaazi ya watu hadi usiku wa manane na pia kuwashirikisha watoto wenye umri usiopaswa kuwemo kwenye ngoma hizo.

Pili, kushindwa kulinda silka na maadili kwa kutodhibitiwa maonesho ya sanaa yenye vitendo viovu.

Tatu, kushindwa kukabiliana na athari za utandawazi.

Mhe. Naibu Spika, sababu kubwa zilizopelekea kuandaliwa kwa mswada huu zinatokana na mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na yale ya kisayansi na teknolojia yaliyozifanya sheria zilizopo kuonekana kupitwa na wakati.

Aidha, sheria hizo zimekuwa zikigongana na sheria nyengine na pia kuibuka malalamiko mengi kutoka kwa jamii yanayotokana na bughudha wanazopata wananchi katika utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika, rasimu ya sheria inayopendekezwa ina sehemu kumi na moja kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza inaelezea masharti ya awali na inaundwa na vifungu viwili vinavyozungumzia jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria na ufafanuzi wa maneno.

Sehemu ya Pili inahusu uundwaji wa Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ambayo imeundwa na vifungu 13 vinavyoelezea uanzishwaji wa Baraza, muhuri wa Baraza, muundo wa Baraza, sifa za Mwenyekiti wa

Baraza, kazi za Baraza, uwezo wa Baraza, mikutano ya Baraza, maamuzi ya Baraza, muda wa Baraza, malipo kwa Wajumbe wa Baraza, kuajiri wafanyakazi wa Baraza, sekreterieti ya Baraza na majukumu ya Baraza.

Sehemu ya Tatu inaelezea uongozi wa Baraza na imeundwa na vifungu 18 vinavyoelezea Katibu Mtendaji wa Baraza, sifa na kazi za Katibu Mtendaji, Katibu wa Baraza, Mrajis, sifa na majukumu ya Mrajis, Rufaa, maombi ya usajili, ada na malipo, kuanzishwa kwa kamati za wilaya za sanaa na sensa ya filamu na utamaduni, mkaguzi wa utamaduni wa wilaya, sifa za mkaguzi wa utamaduni wa wilaya, majukumu ya mkaguzi wa utamaduni wa wilaya na uwezo wa mkaguzi wa utamaduni wa wilaya.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Nne inafafanua utaratibu wa maombi ya kibali na inaundwa na kifungu kimoja kinachoelezea utoaji wa kibali.

Sehemu ya Tano inaelezea maonesho ya machapisho na usambazaji wa mabango ya matangazo na inaunda vifungu viwili vinavyozungumzia maonesho, machapisho na usambazaji wa mabango ya filamu na ukatazaji wa maonesho na machapisho au usambazaji mabango ya maonesho.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Sita inaelezea leseni ya usalama wa nyumba ya maonesho na inaundwa na vifungu saba zinavyoelezea leseni ya vikundi vya utamaduni, kwenda kinyume na masharti ya leseni, usalama wa majengo ya maonesho, leseni za majengo ya maonesho na usalama wa watu wanaohudhuria maonesho hayo. Uwezo wa mkaguzi kuingia katika nyumba za maonesho, maelezo ya picha za filamu na uwezo wa kufanya ukaguzi.

Sehemu ya Saba inafafanua wajibu wa utoaji huduma za mtandao wa *internet* na inaundwa na vifungu viwili vinavyoelezea utaratibu na utoaji wa huduma ya mtandao wa *internet*.

Sehemu ya Nane inaelezea katazo la picha za ngono na inaundwa na vifungu vitatu vinavyoelezea makatazo ya picha za ngono, picha za ngono za watoto na kutaifisha na kuharibu picha za ngono.

Sehemu ya Tisa inahusu masharti ya fedha na inaundwa na vifungu vitatu vinavyoelezea fedha za Baraza, bajeti na ukaguzi wa hesabu.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Kumi inaelezea makosa na adhabu na inaunda vifungu viwili vinavyoelezea makosa na adhabu na ukatazaji wa umiliki wa filamu na machapisho.

Sehemu ya Kumi na Moja inahusu masharti mengineyo na inaundwa na vifungu viwili vinavyoelezea kuhusu uwezo wa waziri kutunga kanuni na kufuta na kubakiza uhalali wa matumizi ambayo yalifanywa katika sheria hizo mbili.

Mhe. Naibu Spika, katika ufikaji wa hoja hii ya mswada huu naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubali mambo yafuatayo:

Kwanza, kuanzisha sheria mpya itakayojulikana kwa jina la Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Pili, kufuta Sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki la Zanzibar; na

Tatu, kufutwa kwa Sheria Nam. 1 ya mwaka 2009 ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu nikiwa mzima wa afya, ili kuwasilisha mchango wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Mswada wa Kuanzisha Baraza la Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, aidha napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuweza kukutana tena leo hii ili kuujadili na hatimaye kuupitisha Mswada huu kwa lengo la kulinda na kuendeleza utamaduni wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu pia ziwafikie Wajumbe wa Kamati na makatibu wa kamati, watendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Wanasheria wetu wa Baraza na wa serikali kwa mashirikiano yao ya kutosha; kwa kutoa michango na kutupa ufanunuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari napenda kuchukua fursa hii kuungana na wenzetu kumuombea dua na kutoa mkono wa pole kwa ndugu na jamaa wote kwa kifo cha aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Magomeni, marehemu Salmin Awadh Salmin kilichotokea hivi karibuni. Mwenyezi Mungu awajalie subra familia, ndugu na jamaa wote wa marehemu pamoja na kuilaza roho ya marehemu mahala pema peponi. Amin.

Mhe. Naibu Spika, ni vyema kuwatambua Wajumbe wa Kamati ambao walihusika kwa namna moja au nyengine kwa kuupitia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar. Wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Mohammed Ali - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Bakari Makame - Mjumbe
4. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe
5. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mjumbe
6. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
7. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
9. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu; na
10. Ndg. Salum Khamis Rashid - Katibu

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya kuletwa Mswada huu ni kufuta Sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Sheria Nam. 1 ya mwaka 2009 ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Utamaduni kwa lengo la kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar, itakayosimamia vyema na kwa ufanisi zaidi majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kudumisha mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari na kuutumia utamaduni kama njia bora ya kupunguza umasikini.

Mhe. Naibu Spika, hapo awali sheria zilizokuwepo zilikuwa na malengo sawa ya kuanzishwa kwa sheria hii, lakini kwa sababu ya maendeleo ya kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na hata ya kisayansi na teknolojia sheria hizo zimeonekana kushindwa kusimamia vyema mabadiliko hayo yanayotokea siku hadi siku.

Kamati yetu inakiri kuwa ni kweli utamaduni na maadili yetu yanazidi kuporomoka siku hadi siku, kutokana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja tofauti ndani na nje ya nchi na athari zake zinaonekana katika rika zote; watoto na vijana ambao ndio tegemeo la Taifa la kesho. Kamati yetu inaiunga mkono serikali kuona kuwa ipo haja ya kuanzisha sheria mpya ambayo itaendana na mabadiliko yote yanayotokea katika jamii yetu ili kulinda, kuhifadhi na kudumisha mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari.

Aidha, mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakiupitisha pia utasaidia kulinda heshima ya Zanzibar kama ilivyokuwa hapo zamani, katika suala zima la utamaduni ambao unaendelea kupotea kwa kasi kubwa katika jamii yetu na hivyo kuanza kupoteza heshima ya Wazanzibari. Ni dhahiri na ni jambo lisilopingika kuwa, utamaduni na maadili ya Wazanzibari yanazidi kuporomoka, na kuporomoka kwa maadili yetu ni kuipoteza heshima ya Wazanzibari ambayo inasifika ulimwenguni kote.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaitaka serikali katika kutekeleza sheria hii, ihakikishe kwamba maeneo yote yanayohusika na maonesho ya taarabu au ngoma zozote zile, au maeneo yanayopigwa *disco* hususan katika maeneo ya kambi za majeshi, polisi au vikosi yanafuata masharti ya sheria hii na kanuni zake; kwa sababu inaonekana kuwa

ni maeneo ambayo yako huru sana na jambo kubwa zaidi ni kuwa vijana wetu huwa wanakwenda sana katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inasisitiza sana kuwa, kwa kuwa mswada huu umekuja kufuta Sheria Nam. 6 ya 1983 ya Baraza la Sanaa na Sheria Nam. 1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Utamaduni, kwa sababu ya kushindwa kukidhi mahitaji kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii yetu. Sasa kwa sheria hii inayokuja tuone kuwa ni kweli imekidhi haja ya kukabiliana na mabadiliko hayo katika jamii yetu na ni kweli kuwa kulikuwa na haja ya kufuta sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika, kimsingi kamati yetu imeukubali na kuunga mkono mswada huu. Hata hivyo, imefanya marekebisho katika baadhi ya vifungu kwa lengo la kusaidia kuufanya uwe bora mswada huu. Marekebisho hayo ni ya kimaandishi na yale ya kuongeza au kuondoa maneno katika baadhi ya vifungu.

Mhe. Naibu Spika, wizara baada ya kushauriana na kamati iliona ni vyema kwa kuwa mswada ulikuwa na marekebisho mengi kutoa nakala nyengine mpya ya mswada ambao utajumuisha marekebisho ya wizara na ya kamati. Hata hivyo, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo kamati inaona yangelifaa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kamati imependekeza katika jina refu la mswada huu lisomeke:

"Mswada wa Kufuta Sheria ya Baraza la Sanaa na Muziki, Namba 6 ya 1983 na Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho, Namba 1 ya 2009 na Kuanzisha Sheria Mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo".

Sababu za mapendekezo haya, tunafahamu kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri Namba 7 ya mwaka 1984, kifungu cha 10 kinaeleza kuwa; jina refu sio sehemu ya sheria. Licha ya kuwa jina refu sio sehemu ya sheria lakini madhumuni makuu ya kuweka jina refu kwenye sheria ni kutoa maelezo kwa urefu yanayohusu sheria hiyo ili kumuwezesha msomaji kwa kusoma jina hilo kuelewa malengo makuu ya kuanzishwa sheria hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 48 kinachosomeka *"Iwapo mtu yeyote akithibitika kutenda kosa chini ya sheria hii, Baraza litataifisha na kuharibu vifaa vyote vinavyohusiana na picha za ngono"*.

Katika kifungu hiki kamati imependekeza marekebisho, kwani Baraza halitakuwa na uwezo wa kutaifisha au kuharibu vifaa hivyo na badala yake huu ni uwezo wa Mahakama. Kwa hivyo, kamati ilipendekeza isomeke kama ifuatavyo: *"Iwapo mtu yeyote akithibitika kutenda kosa chini ya sheria hii, na iwapo akipatikana na hatia, Mahakama itataifisha na kuharibu vifaa vyote vinavyohusiana na picha za ngono."*

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako ili kuwasilisha maoni ya Kamati na tuna imani Waheshimiwa Wajumbe watauchangia, wataujadili na hatimaye kuupitisha mswada huu kwa lengo la kuufanya uwe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa hotuba yako kwa niaba ya kamati. Sasa Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa mswada tumepewa hivi leo kwa hivyo muda uliobakia tutarudi nyumbani kwenda kuusoma ili kesho tupate muda mzuri wa kuja kuchangia.

Kwa hivyo, kwa kuwa muda wetu haujafika namuomba Mwanasheria Mkuu atoe hoja ili tuweze kuahirisha kikao hiki.

KUAHIRISHA KIKAO KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwenye orodha ya leo zimemalizika, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa kifungu cha 23 na 64 cha Kanuni kuahirisha kikao hiki hadi kesho saa tatu asubuhi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mwanasheria Mkuu wanyooshe mkono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru tena kwa mara ya pili, baada ya shukurani hizo naahirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Ijumaa, tarehe 13/03/2015 saa tatu za asubuhi.

(Saa 12:13 kikao kiliahirishwa hadi tarehe 13/03/2015 saa 3:00 asubuhi)